# Ushahidi wa Kurani

Na

Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad[as] wa Qadian

# Ushahidi wa Kurani

Tafsiri ya Kiswahili ya ***Shahadatul-Qur'an*** (Kiurdu)
Swahili translation of ***Shahaadatul-Qur'an*** (Urdu)

Mwandishi:
Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad[as] wa Qadian

Mfasiri:
Sheikh Yusuf Athumani Kambaulaya

Chapa ya Kwanza (Kiurdu): 1893
Chapa ya Kwanza (Kiswahili): 2018

© Islam International Publications Ltd.

Kwa Maelezo Zaidi:
Tanzania:
Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya, Tanzania
Mtaa wa Bibi Titi Mohamed S.L.P. 376, Dar es Salaam.
Simu: +255222110473 Fax: +255222121744

Kenya:
E.A. Ahmadiyya Muslim Mission
P.O. Box 40554 Nairobi Kenya Simu: +254222111031

Kimechapwa na Ahmadiyya Printing Press
Dar es Salaam, Tanzania / Nairobi, Kenya

Cover design by: Usman Nasir Choudhary

ISBN: 978-1-84880-558-3
10 9 8 7 6 5 4 3 2 1

# Maelezo ya Mwenezi

Twaweka mbele ya wasomaji tafsiri ya Kiswahili ya kitabu 'Shahadatul Quran' — Ushahidi wa Kurani — kilichoandikwa na Seyidna Ahmad[as], Mwanzilishi wa Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya.

Sababu ya kuandika kitabu hiki ilikuwa ni kwamba Bwana mmoja wa Amritsar aliyeamini kifo cha Nabii Isa[as] lakini hakuamimi kuwa Masihi yeyote atatokea katika umati wa Mtume[saw]. Huyo bwana akamwandikia Seyidna Ahmad[as], mnamo Agosti 1893, kuna dalili gani ya kuhakikisha kuwa U Masihi Mau'udi, ama kuna hoja ipi inayotulazimisha tumsubiri Masihi yeyote ujaji wake. Bwana huyo hakuamini bishara za ujaji wa Masihi zilizomo ndani ya Hadithi, kwani Hadithi zilikusanywa muda mrefu baada ya Mtume[saw] kufariki.

Seyidna Ahmad[as] amemtolea jawabu toshelevu ndani ya kitabu hiki. Na akaongeza kusema kuwa kama bado yeye

hajatosheka, niko tayari kudhihirisha ishara kumhusu yeye, sharti akipenda hivyo. Baada ya jawabu hili, bwana huyo akanyamaa. Lakini jibu la swali lake likawa na baraka, kwani wengi watafutao ukweli wakanufaika na kuongozwa kwenye haki.

Kitabu hiki kimefasiriwa kwa Kiswahili na Sheikh Yusuf Athumani Kambaulaya na ilidurusiwa na Sheikh Muzaffar Ahmad Durrani, na kisha Sheikh Adnan Hashimi. Hatimaye nikaichunguza tafsiri hii kwa kulinganisha na matini ya Kiurdu kwa uangalifu.

Sheikh Ansar Hussain alisaidia kuzipanga herufi zake kwa kompyuta na Syed Tanwir Mujtaba akashughulikia fometi yake. Mwenyezi Mungu Awapatie ujira bora wote waliosaidia kwa njia hii au ile.


Twaomba, Mwenyezi Mungu Aifanye tafsiri hii iwe na baraka ya kuwanufaisha watafutao ukweli. Amin.

Jamil R. Rafiq

Wakilut Tasnif Tahrike Jadid

Rabwah, Pakistan 25 Machi 2018

## Picha ya ukurasa wa nje
## ya chapa ya kwanza


الحمد للہ والمنت کہ رسالہ طیبہ مبارکہ

المسماۃ بہ

شہادۃ القرآن علی

نزول المسیح الموعود

فی آخر الزمان

مطبع پنجاب پریس سیالکوٹ میں باہتمام

منشی غلام قادر صاحب

فصیح کے چھپا

قیمت

Jalada la chapa ya kwanza

Sifa zote njema ni za Mwenyezi Mungu
na ni hisani yake kwamba kijitabu kizuri
kilichobarikiwa kiitwacho

**Ushahidi**
**wa Kuran**

Juu ya kushuka
kwa Masihi Mau'udi

Katika zama za
mwisho

Kilichochapwa katika kiwanda
cha Panjab Press Sialkot
chini ya usimamizi wa
Munshi Ghulam Qadir Fashihi.

Bei: Anna 6 Nakala: 700

## Tangazo la Vitabu

Hivi
sasa vitabu vilivyopo
miongoni mwa vitabu vyangu
vimeelezwa hapa chini:

| | |
|---|---|
| Baraahine Ahmadiyya, sehme ya 4 | Rupia 4 |
| Surma Chashme Aria | Rupia 2 |
| Fat'he Islam | Anna 3 |
| Taudhihe Maraam | Anna 4 |
| Izalae Auhaam | Rupia 3 |
| Aina Kamaalate Islam | Rupia 2 |
| Tafsir Sura Faatiha pamoja na Kasida kwa Kiarabu * | Anna 6 |
| Tuhfa Baghdaad (Kiarabu) | Anna 3 |
| Barakatud Du'aa | Anna 4 |

Gharama ya posta ni mbali na bei

Mtangazaji
Mimi
Ghulam Ahmad Qadiani

* Pamoja na tafsiri hii kuna zawadi ya Rupia 1000 kwa wanazuoni watakaoweza kuandika mfano wake.

بِسۡمِ اللّٰہِ الرَّحۡمٰنِ الرَّحِیۡمِ[1]

اَلۡحَمۡدُ لِلّٰہِ وَ السَّلَامُ عَلٰی عِبَادِہِ الَّذِیۡنَ اصۡطَفٰی[2]

# MASIHI MAU'UDI

Bwana mmoja, jina lake Ataa Muhammad, ananiuliza katika barua yake ya Agosti 1893 kuwa ipo dalili gani juu ya jambo hili kuwa u Masihi Mau'udi, au sisi twawajibika na kulazimika kumsubiri Masihi yeyote?

Kwanza kabisa yafaa kukumbuka hapa kuwa imani ya mpinzani huyo ni kuwa Nabii Isa[as] kwa hakika ameishafariki kama ilivyomo ndani ya Kurani Tukufu kwa uwazi kabisa, lakini yeye anakataa kuwa katika umati huu yuko anayetarajiwa kuja kwa jina la Isa. Anakubali kuwa bishara hii imo ndani ya Hadithi za Mtume[saw], lakini anafikiri Hadithi haziaminiwi. Anasema kuwa Hadithi zimekusanywa baada ya kupita muda mrefu na nyingi zaidi ni mkusanyiko wa aina ya *Ahaad*, hivyo hazifikirii

---

[1] Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema, Mwingi wa Ukarimu.

[2] Sifa zote njema zinamhusu Mwenyezi Mungu, na salamu ziwafikie watumishi wake Aliowachagua.

habari za Masihi Mau'udi zilizothibitika katika Hadithi kuwa ni kweli iliyohakikishwa. Basi habari zinazoelezwa tu sawa na Hadithi anaziona si chochote na ni upuuzi mtupu, ambazo machoni mwake hazina uthibitisho wowote. Hivyo, mahali hapa ni lazima kumjibu sawa na akili yake. Kwa hiyo, ibainike kuwa katika suala hili kwa hakika kuna mambo matatu yanayohitaji uchambuzi.

La kwanza ni kwamba je habari za ujaji wa Masihi Mau'udi zinazopatikana ndani ya Hadithi si zenye kutegemewa kwa sababu maelezo ya Hadithi yako mbali kabisa na daraja la yakini?

La pili ni kwamba je ndani ya Kurani Tukufu mmetajwa chochote kuhusu bishara hii au hapana?

La tatu ni kuwa kama bishara hii ni hakika iliyokwishathibitika, basi kuna ithibati gani ya jambo hili kuwa mimi ndimi niliyetimiza bishara hii?

Hivyo, miongoni mwa mambo hayo matatu, tunalichambua hilo la kwanza. Basi, ibainike kuwa hakuna yeyote duniani anayekataa kuwa ndani ya

Hadithi mna bishara iliyo wazi ya kumhusu Masihi Mau'udi, bali Waislamu karibu wote wanaafikiana juu ya jambo hili kuwa sawa na Hadithi lazima atakuja mtu mmoja atakayeitwa Isa bin Mariamu. Bishara hiyo imo ndani ya vitabu vya Hadithi vya Bukhari, Muslim, Tirmidhii n.k. kwa wingi kiasi hiki kwamba zatosha kumtuliza mwenye tabia ya uadilifu, na mtu analazimika kuiamini habari iliyoelezwa katika Hadithi hizo zote kwa usawa kuwa Masihi Mau'udi mmoja atakuja. Ingawaje ni kweli kuwa mara nyingi kila Hadithi ikichukuliwa peke yake haizidi daraja la *Ahaad*, lakini hakuna ubishi katika jambo hili kuwa Hadithi zote za Mtume[saw] zilizokusanywa kwa njia mbalimbali kwa kuzitazama zote hizo kwa pamoja, bila shaka yoyote inathibitika kwa yakini kabisa kuwa Mtume[saw] alitoa habari ya ujaji wa Masihi Mau'udi. Na kisha tunapozijumuisha Hadithi zilizomo mikononi mwa Masuni pamoja na zile Hadithi zinazotegemewa na madhehebu mengine ya Kiislamu, mathalan Mashia na

menginyeyo, basi nguvu ya mfululizo huu usiokatika wa wasimulizi inazidi kuthibitika zaidi. Na kisha pamoja na hizo vinapoangaliwa vitabu mamia vya Masufii, hivyo navyo vinashuhudia jambo hili. Kisha baada ya hayo, tunapoangalia nje ya Islam kwenye vitabu vya watu wa Kitabu, yaani Wakristo, kwao pia habari hii ipo. Na pamoja na hayo, uamuzi huu wa Hadhrat Masihi[as] uhusikanao na kushuka kwa Eliya kutoka mbinguni yafahamika pia kutokana na Injili kwamba habari za aina hii hazichukuliwi kidhahiri. Lakini habari hizi za ujaji wa Masihi Mau'udi zaonekana zimeenea katika kila zama kwa nguvu kiasi hiki kwamba hakutakuwa na ujahili mkubwa zaidi ya huu kwamba kusimuliwa kwake kwa mfululizo wa wasimulizi usiokatika ikataliwe. Nasema kweli kabisa kwamba kama vitabu vya Islam, ambavyo habari hii imefululiza kuenea kwavyo vikiratibiwa vya kila karne na kukasanywa pamoja, basi vitabu kama hivyo vitakuwa maelfu bila kupungua. Naam, ni vigumu kumfahamisha jambo hili yule mtu

ambaye hana habari katu ya vitabu vya Kiislamu. Na kwa hakika wapingao kama hao huwa, kwa bahati yao mbaya, watu wasiokuwa na habari hata kwamba hawanayo busara hii kuwa tukio fulani linathibitika kwa nguvu na uimara kiasi gani. Basi, vivyo hivyo bwana mpinzani huyo amepata kusikia kwa mtu fulani kwamba Hadithi nyingi ziko kwenye daraja la *Ahaad*, na kwa hiyo bila kusita akaamua kwamba kwa kuitenga Kurani Tukufu, mengine yote yaliyoaminiwa ya Kiislamu ni dhana tu zisizo na msingi ambazo si za yakini hata kidogo. Lakini kwa hakika huku ni kudanganyika sana ambako athari yake ya kwanza ni maangamio ya dini na imani. Kwani, kama ni kweli kuwa maandiko mengine yote waliyonayo Waislamu minghairi ya Kurani Tukufu, hayo yote ni mkusanyiko wa uongo, udanganyifu, uzushi, dhana na wasiwasi, basi labda katika Islam itabakia sehemu yake ndogo tu. Kwani maelezo yote ya dini yetu tumeyapata kupitia Hadithi za Mtume[saw]. Kwa mfano, sala hii tunayosali mara tano kila siku, ingawa inathibitika

kutoka ndani ya Kurani Tukufu kuwa ni faradhi, lakini inathibitika wapi kuwa Alfajiri ina rakaa mbili za faradhi na rakaa mbili za suna, tena rakaa nne za faradhi za sala ya Adhuhuri na rakaa nne na rakaa mbili za suna, rakaa tatu za faradhi za sala ya Maghribi na rakaa nne za faradhi za sala ya Isha. Vivyo hivyo tunahitaji kabisa Hadithi za Mtume[saw] kujua maelezo ya Zaka. Kadhalika kuna maelezo mengi sana yanayohusu ibada, muamala, mapatano n.k., nayo yanajulikana sana hata kwamba kuyaandika ni kupoteza tu muda na kurefusha maneno. Isitoshe, chimbuko na chanzo cha historia ya Islam ni Hadithi tu hizi za Mtume[saw]. Kama maelezo ya Hadithi yasipotegemewa basi haitupasi hata kuamini kwa yakini kuwa kwa hakika Hadhrat Abu Bakr[ra], Hadhrat Umar[ra], Hadhrat Uthman[ra] na Hadhrat Ali[ra] walikuwa masahaba wa Mtume Muhammad[saw] ambao baada ya Mtume[saw] kufariki walipata Ukhalifa kwa utaratibu huo, na walifariki dunia pia kwa utaratibu huo. Kwani, tusipoamini maelezo ya Hadithi, basi hakuna sababu ya

kusema kwa yakini kuwa watawa hawa walikuwepo, na kwa hali hii itayumkinika kuwa majina yote haya yawe ya kubuni tu na kwa kweli hakuna Abu Bakr[ra] aliyekuwepo wala Umar[ra], wala Uthman[ra] wala Ali[ra], maana sawa na kauli ya mpinzani Mian Ataa Muhammad, Hadithi zote hizi ni *Ahaad*, na popote ndani ya Kurani Tukufu majina haya hayakutajwa, basi kwa mujibu wa kanuni hii yakubaliweje! Kadhalika jina la baba yake Mtume[saw] kuwa Abdullah na jina la mamake kuwa Aamina na jina la babu yake mzaa baba kuwa Abdul Muttalib, tena jina la mmoja wa wakeze Mtume[saw] kuwa Khadija[ra] na jina la mwingine kuwa Aisha[ra] na mwingine kuwa Hafsa[ra], na jina la yaya wake kuwa Halima, na Mtume[saw] kwenda pangoni Hiraa kufanya ibada, na baadhi ya masahaba kuhamia Uhabeshi, na Mtume[saw] kukaa Makka miaka kumi baada ya kutumwa, kisha vita vyote kupiganwa visivyokuwa na dalili wala alama yoyote ndani ya Kurani Tukufu ambapo mambo yote haya yanathibitika kutoka katika Hadithi tu, sasa je matukio yote haya yakataliwe

tu kwa vile Hadithi si chochote kile? Kama hii ni kweli, basi haitawezekana kwa Waislamu kuelezea hata sehemu yoyote ya maisha matakatifu ya Mtume[saw]. Inatakiwa iangaliwe kuwa maisha ya Bwana wetu[saw] yalikuwaje alipokuwa anaishi Makka kabla ya kupewa unabii, kisha ni mwaka gani alianza kutoa mahubiri na wito wa unabii, na kwa utaratibu gani watu wakaingia ndani ya Islam, na kwa miaka kumi alipoishi Makka makafiri walimtesa namna gani, kisha kwa nini na kwa sababu zipi vita vilianza, na ni vita vingapi ambamo Mtume[saw] mwenyewe alishiriki, na katika uhai wa Mtume[saw] Islam ilikuwa imekwishaenea ndani ya nchi zipi, na je Mtume[saw] aliwahi kuwaandikia wafalme wa zama zile barua za kuwahubiri au hapana, na kama aliwaandikia, matokeo yake yalikuwa nini? Kisha baada ya Mtume[saw] kufariki wakati wa Hadhrat Abu Bakr Siddik[ra], Uislamu ulipata ushindi gani na kulikuwa na matatizo gani. Na katika zama za Hadhrat Faruuk[ra], Islam ilipata ushindi katika nchi zipi. Mambo yote haya yanajulikana kwa kupitia Hadithi na

kauli za masahaba. Hivyo, kama Hadithi si kitu chochote, basi kujua hali za wakati ule sio vigumu tu bali itakuwa muhali kabisa. Na katika hali hii wapinzani watapata ndani ya matukio ya kuhusu Mtume[saw] na masahaba, mwanya wa kuzusha mambo na sisi tutawapa nafasi kubwa ya kufanya mashambulizi, na itabidi tuamini kuwa maelezo yoyote ya matukio yanayopatikana ndani ya Hadithi na maelezo ya maisha ya Mtume[saw] si chochote na hayakutokea, mpaka hapo kwamba hata majina ya masahaba pia kwa hakika hayathibitiki. Hivyo basi, kufikiria kuwa kwa njia ya Hadithi hatuwezi kupata ukweli wenye yakini kabisa ndiyo kana kwamba kuangamiza sehemu kubwa ya Uislamu kwa mikono yetu wenyewe. Bali jambo la msingi na lililo sahihi ni kuwa chochote kilichobainishwa na Hadithi lazima kikubaliwe sharti kisigongane waziwazi na Kurani Tukufu. Kwani, imekwisha kubaliwa kwamba tabia ya asili ya mtu ni kusema kweli, na mtu anaongopa anapolazimishwa na sababu fulani, maana hiyo ni

kinyume cha asili yake. Na zile Hadithi ambazo kiitikadi na kimatendo zikawa zatekelezwa daima na makundi mbalimbali ya Kiislamu, kukataa usahihi wa hizo na kufululiza kwazo ni aina fulani ya umajununi na kichaa. Mathalani, kama leo mtu ahoji kuwa sala tano wanazosali Waislamu nyakati tano, idadi ya rakaa zake ni jambo linalotia shaka, maana kwa mfano, haikutajwa ndani ya aya yoyote ya Kurani Tukufu kuwa msali rakaa mbili wakati wa Alfajri, kisha rakaa mbili za sala ya Ijumaa na rakaa mbili mbili za sala za Idi mbili. Na Hadithi zenyewe ni *Ahaad* ambazo hazifai kuleta yakini, je mtu anayehojiana hivyo atakuwa ni mwenye haki? Kama rai za aina hii kuhusu Hadithi zikubalike, kwanza kabisa sala zitaondolewa, maana Kurani Tukufu haikueleza namna ya kusali, sala hizi zinasaliwa tu kwa kuzitegemea Hadithi. Sasa kama mpinzani akitoa hoja hii hii kuwa Kuran Tukufu haikufundisha njia ya kusali, na njia waliyojipangia Waislamu inakataliwa kwa vile Hadithi hazistahili kuaminika, basi tukikubali jambo hili

kwamba Hadithi si chochote tunaweza kujibuje hoja hii isipokuwa kuikubali tu. Bali katika hali hii hata sala ya jeneza pia ya Kiislamu itakuwa ni upuuzi tu, kwani ndani ya Kurani Tukufu haikuelezwa popote kuwa kuna sala ya aina hii pia isiyokuwa na rukuu na sijida. Sasa hebu angalieni na fikirieni kuwa kwa kuziondoa Hadithi itabaki nini ya Islam. Na jambo lenyewe hili ni matokeo ya upungufu wa kufikiri kuwa idhaniwe kuwa Hadithi ndiyo tu kuyategemea maelezo ya mtu mmoja au wawili na kuyafikiria eti ndiyo kauli ya Mtume[saw]. Bali hakika yenyewe ni kuwa utaratibu wa Hadithi ni tawi la utaratibu wa mfuatano wa matendo. Mathalani, muhadithina waliwashuhudia mamilioni ya watu wanasali rakaa tatu za faradhi za sala ya Magharibi na rakaa mbili za Alfajri na kwamba katika kila rakaa lazima wanasoma sura Fatiha, na pia wanasema Amina kwa sauti au kimoyomoyo, na wanasoma katika *Ka'da* ya mwisho *Attahiyyatu* na sala ya Mtume[saw] na dua kadhaa na hutoa salamu pande zote mbili kumalizia sala, basi

kwa kuangalia utaratibu huu wa ibada, muhadithina wakapata hamu na shauku kuwa utaratibu huu wa ibada waufikishe mpaka kwa Mtume Muhammad[saw] na wathibitishe kupitia Hadithi sahihi *marfu'a muttasila*. Ingawa ni kweli kuwa hawakufanya juhudi kubwa ya kuleta njia elfu moja au elfu mbili za *isnadi* kwa madhumuni ya kila Hadithi moja moja, lakini je hili pia ni kweli kuwa waasisi wa sala walikuwa ni Muhaddithina, na kabla ya hapo sala ilikuwa haipo duniani, na dunia ilikuwa haina habari yoyote ya sala, na baada ya karne kadhaa sala ilianzishwa kutokana na kuziamini Hadithi moja au mbili? Hivyo basi, ninasema kwa nguvu sana kuwa huu utakuwa ni udanganyifu mkubwa kama ikidhaniwa kuwa uthibitisho wa rakaa na namna inavyosaliwa sala ulitegemea Hadithi moja au mbili ambazo kwa mtazamo wa dhahiri zaonekana ni aina ya *Ahaad*. Kama huu ndio ukweli, basi kwanza kabisa faradhi za Islam zinakabili maombolezo makubwa yasio na tiba ambayo kuyafikiria ni jambo la kwanza kwa

anayeitwa Mwislam mwenye ghera. Lakini ikumbukwe kuwa mawazo kama hayo ni ya watu wale tu ambao kwa kuzinduka hawakuangalia historia na matukio, kawaida za dini na ibada za Kiislamu kuwa kwa nini na kwa njia zipi mambo hayo yamefikia daraja ya mambo ya yakini.

Hivyo basi, iwe wazi kuwa ili kuipata yakini hii, silsila ya mazoea na desturi za kaumu ni mfano mzuri wa kutuliza. Mathalani, Hadithi zinazothibitisha kuwa sala ya Alfajri ina rakaa kadha na sala ya Magharibi ina rakaa kiasi kadha, ingawaje Hadithi kama hizo ni mbili au tatu tu na sio zaidi ya daraja ya *Ahaad*, lakini je kabla ya utafiti na uchunguzi huu watu walikuwa hawasali? Na je baada ya utafiti wa Hadithi hizo na kupata maelezo ya wasimuliaji ndipo sala zikaanzishwa? Bali mamilioni ya watu walikuwa wakisali kama kawaida. Na hata kama usingekuwepo utaratibu wa *Isnaad* za Hadithi, hata hivyo kutokana na mfululizo wa matendo haya ilikwishathibitika kwa yakini kuwa mafundisho ya kudumu ya Islam kuhusu sala sikuzote, karne baada

ya karne, yaliendelea kuwa haya haya. Naam, *Isnaad marfu*'a *muttasila* za Hadithi zikaing'arisha silsila hii. Hivyo basi, kama Hadithi zikiangaliwa kwa kanuni hii, itakuwa ni kosa kubwa kuzichukulia Hadithi nyingi hizo kuwa *Ahaad* ambazo zimetiliwa nguvu na mfululizo wa matendo. Na kwa kweli hili ndilo kosa kubwa sana lililowapeleka mbali na ukweli wa Islam wale watu wa zama hizi wasioamini uwepo wa Mungu. Hao wanadhani kuwa suna zote za Islam, desturi, ibada na historia vinavyorejeshwa kwenye Hadithi, hivyo vimeimarika kwa msingi wa Hadithi tu chache, ilhali hili ni kosa lao kubwa sana. Bali utaratibu wa matendo alioanzisha Mtume wetu Muhammad[saw] yeye mwenyewe uliisha enea kwa mamilioni ya watu kiasi kwamba hata kama wasingekuwepo duniani Muhadithina, hata hivyo utaratibu huo usingepungukiwa kitu. Kila mmoja analazimika kukubali kuwa Mwalimu huyu Mtukufu na Mjumbe Mtakatifu[saw] wa Allah hakuyawekea mipaka mafundisho kuwa watu wawili au wanne wafundishwe

hayo, na waliobaki wote wasiwe na habari zake. Kama ingekuwa hivyo, Islam ingeharibika kiasi hiki kwamba isingelirekebika kwa mkono wa Muhaddithi yeyote yule awaye. Ingawa, Maimamu wa Hadithi waliandika maelfu ya Hadithi kuhusiana na mafundisho ya dini, lakini swali lenyewe ni hili kuwa ni Hadithi gani isiyokuwa inatekelezwa hata kabla ya wao kuiandika na dunia ilikuwa haina habari ya madhumuni yake! Kama yapo mafundisho ya namna hii, au tukio la aina hii, au itikadi kama hii ambayo msingi wake waliuweka Maimamu wa Hadithi tu kutokana na riwaya fulani ambayo athari na alama yake yoyote haionekani katika mfululizo wa matendo yaliyokubaliwa na mamilioni ya watu wala haikutajwa habari yake yoyote ndani ya Kurani Tukufu, bila shaka hiyo iliyo mojawapo ya *Ahaad* ambayo imejulikana baada ya miaka 100 au 150, lazima itakuwa imeanguka chini kabisa kutoka kwenye daraja ya yakini, na lolote litakalosemwa kuhusu kutokutegemewa kwake litakuwa sawa. Lakini Hadithi kama hizo kwa kweli

hazihusikani sana na dini na historia ya Islam, bali ukifikiri utakuta kuwa wataalamu wa Hadithi wamezitaja kidogo sana Hadithi kama hizo ambazo hazipo kabisa katika silsila ya mfululizo wa matendo. Hivyo, si sawa katu kama vile baadhi ya wasiofahamu wanavyodhania kuwa mamia ya mambo ya lazima ya dini hata sala na saumu pia ulimwengu umejifunza kutokana tu na Hadithi za Imam Bukhari, Muslim n.k. Je mpaka miaka mia moja au mia moja na hamsini watu waliendelea bila dini? Je watu hao hawakuwa wanasali, hawakutoa zaka, hawakuhiji na mambo yote kuhusu itikadi za Islam yaliyoandikwa ndani ya Hadithi hawakuyajua? La hasha! Sivyo kabisa!! Na yeyote mwenye kudhania hivyo, upumbavu wake ni wa kushangaza ajabu. Hivyo, kama kabla ya zama za wataalamu wa Hadithi, Bukhari na Muslim, Islam ilikuwa imestawi jinsi ilivyokuwa baada ya vitabu vya maimamu hao, basi ni utovu wa adabu sana na ni kinyume kabisa cha akili kutumia nguvu kwa kuitakidi kuwa Islam imestawi kwa kutegemea tu riwaya za karne

ya pili ambazo katika zama hizi zinaitwa Hadithi. Na masikitiko yenyewe ni haya kuwa licha ya wapinzani, hata waumini wa dini yetu wasiojua nao pia wamedanganyika. Wao wanafahamu kwamba baada ya muda fulani, sawa na riwaya za Hadithi, watu wamekubalishwa mambo mengi ya dini ya Kiislam, ambao hawakuwa na habari nayo kabisa kabla ya kuandikwa Hadithi. Bali ukweli wenyewe ulio dhahiri shahiri ni kuwa kama Maimamu wa Hadithi wamewafanyia watu hisani kidogo, basi ni hii tu kuwa yale mambo yaliyokubaliwa na dunia kwa ajili ya kutekelezwa tangu awali, Maimamu hao walifanya utafiti na uhakiki wa *isnaad* zao na wakaonesha kuwa wanayokubali Waislamu katika zama hizi au wanayotenda siyo mambo yaliyoingia katika Islam kama bidaa, bali ni maneno na matendo yale yale ambayo Mtume[saw] aliwafundisha masahaba, radhi ya Mungu iwe juu yao.

Inasikitisha kuwa kukosea kuelewa jambo hili sahihi na la kweli, wenye mtazamo finyu wamefanya kosa kubwa

ambalo kwa sababu yake mpaka sasa hao wanazitazama Hadithi kwa jicho la chuki kubwa. Ingawa ni kweli kuwa sehemu ile ya Hadithi iliyo nje ya silsila ya kutekelezwa kwa kauli na amali na haisadikishwi na Kurani Tukufu, haiwezi kutambulika kuwa katika daraja ya yakini kamili, lakini ile sehemu ya pili iliyoingia katika utekelezwaji, na mamilioni ya watu tangu mwanzo wameendelea kuilinda kwa matendo yao, ichukuliweje kuwa yenye dhana na mashaka? Mfululizo wa matendo ya watu, ambao umetambulikana kuanzia watoto mpaka kwa baba zao, na kutokea baba zao mpaka kwa babu zao, na kutokea babu mpaka baba wazazi wa babu, na athari na nuru zake zikaonekana tangu mwanzo wake, basi haiwezi kubakia nafasi ya shaka hata chembe.

Na mtu hana njia nyingine pasipo kuchukulia mfululizo wa utekelezaji kama huu kuwa miongoni mwa mambo ya yakini ya daraja ya kwanza. Kisha pamoja na silsila ya mfululizo wa utekelezaji, Maimamu wa Hadithi wakaimarisha silsila nyingine na wakafikisha *isnaad* ya

mfululizo wa utekelezaji hadi Mtume Muhammad[saw] kupitia kwa wasimulizi wasema kweli washika dini, juu ya hayo kuleta upingamizi ni kazi ya watu ambao hawakujaliwa busara ya kiimani wala akili ya kibinadamu. Sasa baada ya utangulizi huu, ibainike kuwa bishara iliyomo ndani ya Hadithi kuhusu Masihi Mau‘udi siyo tu kwamba Maimamu wa Hadithi wameiandika kwa sababu ya riwaya chache, bali imethibitika kuwa tangu mwanzo kiitikadi bishara hii ilikuwa imeshaingia ndani ya mishipa ya damu za Waislamu, kana kwamba kadiri Waislamu walivyokuwepo duniani wakati huo, kiasi hicho hicho cha ushahidi ulikuwepo juu ya usahihi wa bishara hii, kwani kiitikadi walikuwa wanaikumbuka kuanzia hapo awali. Na Maimamu wa Hadithi, Imamu Bukhari na wengineo, kama kuna jambo walilofanya kuhusu bishara hii kwa juhudi zao ni hili tu kuwa walipoikuta bishara hii imeenea ndani ya mamilioni ya Waislamu na inatajwa sana, basi wao sawa na kanuni yao wakagundua chanzo cha mfululizo huo wa kauli hii ya

Waislamu na kuhakikisha *isnaad* yake kwa masimulizi sahihi ya Hadithi *marfu'a muttasila* yanayopatikana mengi ndani ya vitabu vyao. Mbali na hii, hakuna sababu, Mungu Apishe mbali, kuwa huu ni uzushi, Waislamu walikuwa na haja gani ya uzushi huu? Na kwa nini waliafikiana juu yake? Ni kitu gani kilichowalazimisha waelekee kuzua uzushi huu? Kisha tunapoangalia kuwa upande wa pili pia zinapatikana Hadithi nyingi za aina hii ambamo mmetolewa bishara hii kuwa katika zama za mwisho maulamaa wa umati huu watakuwa na sifa za Kiyahudi, na uaminifu, ucha Mungu na utakaso wa ndani utawatoka na katika zama hizo dini ya msalaba itakuwa na nguvu sana na utawala wa dini ya msalaba na ufalme wake utaenea karibu dunia nzima, hapo dalili madhubuti zinapatikana zinazothibitisha usahihi wa Hadithi hizi. Kwani, hakuna shaka kuwa bishara hii imekwishatimia katika zama hizi. Wanazuoni wetu wa zama hizi kwa kweli wameishashabihiana na Wayahudi, na dola na utawala wa Kikristo umeenea duniani kiasi hiki kwamba

mfano wake haupatikani katika zama zilizopita. Basi, ikiwa sehemu moja ya bishara hiyo inatimia waziwazi bila wasiwasi wowote, sasa ukweli wa habari ya pili una shaka gani? Hili ni jambo linalokubaliwa na kila mwenye akili kuwa, kwa mfano, kama Hadithi moja iwe katika *Ahaad*, na haipo katika mfululizo wa matendo, lakini iambatane na bishara moja, na itimie katika wakati wake, au sehemu yake moja itimie, hapo hakutabakia shaka yoyote ndani ya usahihi wake. Mathalan, Hadithi kuhusu Moto wa Hijazi iliyoandikwa ndani ya *Sahihaini* — Sahihi Bukhari na Sahihi Muslimu— haina shaka yoyote kuwa ni miongoni mwa Hadithi za *Ahaad*, lakini bishara hiyo ikatimia barabara baada ya kupita miaka mia sita ambayo hata Waingereza wamekiri kutimia kwake. Na ikatimia katika zama ambapo mamia ya miaka ilikwishapita baada ya kutungwa na kuenezwa kwa vitabu hivyo. Basi, je tunaweza kuwa na rai juu ya Hadithi hizi kuwa *Ahaad,* hivyo haziwezi kukubalika? Kwani, ikiwa ukweli wake umekwisha julikana, basi hapo kuwaza wazo hili moyoni

ni ujinga mbovu na wenye kuchukiza.

Hivyo basi, fikirieni juu ya bishara kumhusu Masihi Mau'udi kuwa ndani yake pia mlikuwa na maneno haya pengine waziwazi na pengine kwa kuashiria, kwamba yule Masihi Mau'udi atakuja katika wakati ambapo dola na nguvu ya Wakristo itakuwa imeenea duniani kote. Garimoshi litakuwa linatumika, na sehemu kubwa za ardhi zitatumika kwa kilimo, na watu wataelekea sana kwenye kilimo mpaka maksai wa kulimia watapanda bei, mifereji itakuwa mingi sana ardhini, na kulingana na hali za kidunia zitakuwa zama za amani. Hivyo, tunaona kuwa bishara hii imetimia katika zama zetu, maana utawala wa Kikristo katika zama hizi umefikia kilele kiasi hiki kana kwamba madola na tawala zingine mbele yake hazipo tena. Garimoshi, mifereji na kilimo kwa wingi tumeviona sisi wenyewe kwa macho yetu. Sasa fikirieni kuwa je katika bishara hii hamna mambo ya ghaibu ambayo yapo nje ya uwezo wa mwanadamu? Je hali hii ya kuanguka kwa Uislamu ilikuwa inajulikana wakati

ule ambapo panga za Waislamu zilikuwa zinawaangukia makafiri mithili ya radi? Je miongoni mwa wanadamu yupo mwenye uwezo wa kutoa habari ya ghaibu ya njia mpya ya usafiri ambayo hapo awali haikuwepo? Inueni macho muone na fikirieni kwa makini kuwa je bishara hii si miongoni mwa zile bishara adhimu ambazo uhakika wake na kudhihiri kwake huwa ndani tu ya elimu ya Mwenyezi Mungu, na ujanja wa kibinadamu na mbinu dhaifu za viumbe haziwezi kusababisha shaka yoyote. Ibainike kuwa bishara hizi zina mtiririko wa ajabu na kwa utaratibu fasaha wa daraja ya juu kabisa na muundo imara kwa kupambwa na maarifa ya kina na elimu za ndani na mambo ya ghaibu ambao mwanadamu hawezi kuifikia kamwe shani yake tukufu. Kwa mfano, kwanza alieleza zile bishara za kuhusu zama za maendeleo ya Islam, na kuhusiana na bishara hizo akasema Kisra ataangamia na baada yake hakutakuwa na Kisra, na Kaisari ataangamia na baada yake hakutakuwepo Kaisari, na Islam itapata maendeleo, itaenea na itaingia ndani ya kila kaumu. Na

akasema tena kuwa zama za mwisho zitaufikia umati huu ambapo maulamaa wengi wa umati huu watafanana na Wayahudi, uaminifu na ucha Mungu utawaondoka. Fatuwa za uongo, udanganyifu na hila itakuwa ndiyo dini yao. Watazingirwa ndani ya tamaa za kidunia na watashabihiana sana mno na Wayahudi mpaka hapo kwamba kama Myahudi yeyote aliwahi kuzini na mama yake nao pia watafanya hivyo. Na katika zama hizo, taifa la Kikristo litaenea duniani na litayashinda mataifa mengine, na mapenzi ya dini yatapoa mioyoni na kwa sababu ya kuvuma kwa hewa za sumu, dini ya Islam itaingia katika hatari zifululizazo zisizokatika. Ndipo misiba itatokea na maafa yatazidi, na ucha Mungu utaondoka mioyoni mwa Waislamu. Itakuwa bora mtu aishi peke yake na atosheke kwa kunywa maziwa ya mbuzi na asilitaje jina la Jamaat ya Waislamu. Na akasema, ukiona hali kama hii, basi yaache madhehebu yote, ukaishi kutafuna mizizi ya mti mpaka kukata roho yako. Kisha akatoa habari ya kuja Masihi Mau'udi na akasema kuwa

dini ya Kikristo itafikia mwisho wake kwa mkono wake. Akasema, yeye atauvunja msalaba wao, na hakusema kuwa yeye ataukanyagilia mbali utawala wao. Hii ilikuwa inaashiria kwenye jambo hili kuwa ufalme wa Masihi Mau‘udi utakuwa wa kiroho na yeye hatahusika kamwe na madola ya kidunia, bali yeye atapigana kwa nguvu za baraka zake na kwa silaha za miujiza yake ataingia katika medani hata ataivunja adhama na nguvu ya msalaba, na atafichua ubovu wa itikadi za Ukristo zenye nuksi zisizo na baraka, kwani nuru yake itang'aa kama upanga. Na kama vile radi inavyoanguka, ndivyo atakavyoliangukia giza la kufuru hata kwamba watafutao haki wataelewa kuwa Mungu Aliye Hai Yuko pamoja na Islam. Bishara zote hizi ndani ya Hadithi zinatiririka mfano wa mto, na zinahusiana zenyewe kwa zenyewe kiasi kwamba kuikadhibisha moja inalazimu kukadhibisha ya pili; na kuikubali moja inalazimu kuikubali ya pili pia. Basi katika bishara kama hizi zinazofululiza, zenye utaratibu, zilizo imara na zenye nidhamu, nani anaweza

kutilia shaka isipokuwa yule tu aliyepungukiwa maarifa kuwazidi wendawazimu? Je yuko yeyote mwenye busara anayeweza kufikiria hata kwa sekunde moja kuwa bishara hizi maelfu kwa maelfu zenye mambo yasiyo ya kawaida ni uzushi tu wa mwanadamu? Ukweli wenyewe ni kuwa mambo makubwa yaliyoratibiwa kwa nidhamu kubwa hayawezi kukataliwa kamwe, maana kuyakataa hayo inalazimu yatokee mapinduzi makubwa na inabidi kuibadili dunia nzima. Isitoshe, ndani ya bishara hizi mna alama hii kubwa ya ukweli wake kuwa yale yaliyoandikwa humo kuhusu mabadiliko ya kidunia na kwa dhahiri yalionekana hayawezekani, mambo yote hayo yameishatimia. Maana kuanzia tu karne ya kumi na tatu, maafa ya ndani ya na nje yalianza kuzidi mpaka kufikia mwisho wa karne ya kumi na tatu, kana kwamba dini, heshima na enzi ya Kiislamu vikawa vimefikia mwisho, na mabalaa yakaishukia dini ya Waislamu na dunia yao, kana kwamba ulimwengu wao ukabadilika kabisa. Tukiyaweka mabalaa haya mbele ya macho yetu

tunapozingatia bishara hizo walizoandika Imam Bukari na Muslim miaka karibu elfu moja na mia iliyopita kutoka sasa, na wakaziandika katika zama zile wakati jua la Islam lilipokuwa linang'aa utosini, na kwa uzuri hali yake ya ndani ikaufanya hata uzuri wa Yusufu kuionea wivu, na hali yake ya nje kwa adhama yake ilikuwa inamtia aibu hata mfalme Alexander wa Roma, hapo kwa kukumbuka wahyi kamili mtakatifu wa Mtume wetu Mtukufu na adhma yake na jalali yake na nguvu yake tukufu, joto letu la kiimani huchemka kwa jazba na hujikuta tunalia bila kutarajia. Subhanallah! Alikuwa ni Nuru gani huyu ambaye miaka elfu moja na mia tatu hapo kabla akadhihirishiwa mapema namna umati wake utakavyokuwa mwanzoni na kutastawi kimwujiza na kwa vipi katika zama za mwisho utaanguka chini mara moja, na kisha kwa vipi katika karne chache taifa la Kikristo litapata ushindi duniani kote. Ikumbukwe kuwa kuhusiana na zama hizo Mtume[saw] akizungumzia Masihi Mau'udi akatoa habari iliyoandikwa ndani ya Sahihi

Muslim na akasema: ليتركن القلاص فلا يسعى عليها yaani, katika zama za Masihi Mau'udi usafiri wa ngamia utaachwa, hakuna atakayempanda na kumtumia kwa usafiri. Hiyo ilikuwa inaashiria kwenye usafiri wa garimoshi ambalo baada ya kuvumbuliwa hilo hakutakuwa na haja tena ya usafiri wa ngamia. Na ngamia ametajwa kwa vile miongoni mwa njia za usafiri huko Uarabuni, usafiri wa ngamia ulikuwa mkubwa wa kupakia vitu vya nyumbani na kupandwa. Na kikubwa kinapotajwa kidogo chaingia humo chenyewe. Hivyo, maana yake ilikuwa ni kuwa katika zama hizo usafiri fulani utapatikana utakaoshinda pia hata ngamia, kama mnavyoona kuwa baada ya kuvumbuliwa garimoshi, karibu kazi zote zilizofanywa na ngamia sasa zinafanywa na magarimoshi. Basi, bishara gani itakuwa safi na ya wazi zaidi kuliko hii. Kurani Tukufu pia imeeleza habari za zama hizi kama isemavyo وَإِذَا الْعِشَارُ عُطِّلَتْ[3] yaani zama za mwisho ni zile

[3] Sura At-Takwiir, 81:5.

ambapo ngamia ataachwa. Hii pia inaashiria kwenye garimoshi. Hadithi ile na aya hii, zote zinaelezea habari hii moja. Na kwa vile ndani ya Hadithi hiyo imeelezwa kwa uwazi kuhusiana na Masihi Mau'udi, lazima hoja yapaswa kutolewa kuwa aya hii pia inaelezea hali ya zama za Masihi Mau'udi, na kwa kifupi inaashiria kwenye Masihi Mau'udi. Pamoja na ishara hizi bayana zing'aazo kama jua, watu wanatia shaka kuhusu bishara hizi. Sasa waadilifu wafikirie wenyewe kuwa kutilia shaka bishara zenye mambo ya ghaibu yaliyoshuhudiwa kwa macho kutimia kama sio upumbavu, ni nini basi?

Kiasi nilichoandika kuhusu bishara juu ya Masihi Mau'udi kwa mujibu wa Hadithi, mimi nina yakini kuwa chatosha kumtuliza mtu ambaye baada ya kuupata ukweli hataki tena kuupinga bila haki. Hapa sikunukuu maneno yenyewe ya Hadithi wala sikuandika muhtasari wa Hadithi zote, maana Hadithi hizo ni maarufu na zinaongelewa na watu wote kiasi kwamba hata wanafunzi wadogo wadogo wa vijijini pia wanazijua. Na kama

Hadithi zote zinazohusikana na habari hii ningeziandika ndani ya kitabu hiki kidogo, basi mimi labda hata baada ya kuandika *juzuu*[4] kumi pia nisingekamilisha. Lakini mimi ninawaelekeza wasomaji kuwa lazima waviangalie kwa makini vitabu vyenyewe vya Sihah Sitta au tafsiri zake wakajue kuwa kwa wingi namna gani na kwa maelezo ya nguvu kiasi gani Hadithi za aina hii zinapatikana.

Hoja ya pili iliyohitaji uchambuzi ilikuwa ni hii kuwa ndani ya Kurani Tukufu mmegusiwa chochote kuhusu Masihi Mau'udi au hapana? Maamuzi yaliyotolewa na dalili dhahiri ni haya kuwa maelezo yake lazima yamo ndani ya Kurani Tukufu. Na hakuna shaka yoyote kuwa mtu yule atakayefikiria kwa makini juu ya bishara zinazohusu zama za mwisho za umati huu zilizomo ndani ya Kitabu hiki Kitukufu, basi yeye akiwa anao moyo kifuani mwake wenye ufahamu na ulio hai, hatakuwa na njia nyingine ila kukubali kuwa ndani ya Kurani Tukufu

---

[4] *Juzuu* moja katika zama zile katika istilahi ya uchapaji ilimaanisha kurasa 16. Mwenezi.

kwa yakini kabisa mna habari za kuja msuluhishi mmoja ambaye kwa maneno mengine ndiye lazima awe anaitwa jina la Masihi Mau‘udi na si jina jingine. Ili kuielewa habari hii yapasa kuziangalia kwanza aya hizi kwa pamoja, kwa mfano aya hizi:

وَالَّتِيْٓ اَحْصَنَتْ فَرْجَهَا فَنَفَخْنَا فِيْهَا مِنْ رُّوْحِنَا وَجَعَلْنٰهَا وَابْنَهَآ اٰيَةً لِّلْعٰلَمِيْنَ ○
اِنَّ هٰذِهٖٓ اُمَّتُكُمْ اُمَّةً وَّاحِدَةً ۖ وَّاَنَا رَبُّكُمْ فَاعْبُدُوْنِ ○ وَتَقَطَّعُوْٓا اَمْرَهُمْ
بَيْنَهُمْ ۭ كُلٌّ اِلَيْنَا رٰجِعُوْنَ ○[5]

حَتّٰٓى اِذَا فُتِحَتْ يَاْجُوْجُ وَمَاْجُوْجُ وَهُمْ مِّنْ كُلِّ حَدَبٍ يَّنْسِلُوْنَ ۔[6]

وَاقْتَرَبَ الْوَعْدُ الْحَقُّ فَاِذَا هِيَ شَاخِصَةٌ اَبْصَارُ الَّذِيْنَ كَفَرُوْا يٰوَيْلَنَا قَدْ كُنَّا
فِيْ غَفْلَةٍ مِّنْ هٰذَا بَلْ كُنَّا ظٰلِمِيْنَ ۔[7]

Yaani Mwenyezi Mungu Alimpa muongozo mama yule aliyejilinda utupu wake kwa mtu mgeni basi Mwenyezi Mungu Akampulizia roho yake na akamfanya yeye na mwanaye kuwa ishara kwa dunia. Na Mungu Akasema kuwa umati huu wenu ni umati mmoja tu, nami ni Mola na Mlezi wenu. Kwa hiyo niabuduni mimi tu.

5 Sura Al-Ambiyaa, 21: 92-94. Mwenezi.

6 Angalieni Ezekieli, 38 na 39, aya 5, 6. Raudhatus Safaa: Bayana mlango wa 4, 5, 6. Tafsir Ma‘alim. Mwandishi.

7 Sura Al-Ambiyaa, 21:97-98. Mwenezi.

Lakini wao wakawa makundi makundi na jambo lao wakalifanya vipande vipande na wakaleta hitilafu baina yao, na mwishowe kila mmoja atarejea kwetu tu. Na makundi yote yatakuwa katika hali hiyo hiyo mpaka hapo watakapofunguliwa Yajuja na Majuja, nao toka kila mahali palipoinuka watakuja mbiombio. Na mtakapoona kuwa Yajuja na Majuja wamekuwa na nguvu duniani, basi fahamuni kuwa ahadi ya kweli ya kuenea dini ya kweli duniani imekurubia. Na ahadi ile ndiyo hii:

هُوَ الَّذِيْٓ اَرْسَلَ رَسُوْلَهٗ بِالْهُدٰى وَدِيْنِ الْحَقِّ لِيُظْهِرَهٗ عَلَى الدِّيْنِ كُلِّهٖ
وَلَوْ كَرِهَ الْمُشْرِكُوْنَ ۟ۧ[8]

Kisha Akasema kuwa wakati wa kudhihiri ahadi hii macho ya makafiri yatakodoleka nao watasema "Ole wetu, sisi tulikuwa katika mghafala, bali tulikuwa wadhalimu". Yaani, haki itadhihiri kwa nguvu sana na makafiri wataelewa kuwa wako katika hatia. Muradi

---

[8] Yeye ndiye Aliyemtuma Mtume Wake kwa mwongozo na dini ya haki ili kuifanya ishinde dini zote, ijapokuwa washirikina wachukie. Sura As-Saff, 61:10. Mwenezi.

wa aya zote hizi ni kuwa katika zama za mwisho dini nyingi zitaenea duniani, na kutakuweko na madhehebu mengi. Kisha mataifa mawili yatajitokeza yatakayokuwa ya Kikristo nayo yatapata kila aina ya maendeleo ya juu. Nanyi mtakapoona dini ya Kikristo na madola ya Kikristo yameenea duniani, basi jueni kuwa wakati wa kutimia ahadi umekaribia.

Kisha katika sehemu nyingine akasema:

فَإِذَا جَآءَ وَعۡدُ رَبِّي جَعَلَهُۥ دَكَّآءَۖ وَكَانَ وَعۡدُ رَبِّي حَقّٗا ۝ وَتَرَكۡنَا بَعۡضَهُمۡ يَوۡمَئِذٖ يَمُوجُ فِي
بَعۡضٖۖ وَنُفِخَ فِي ٱلصُّورِ فَجَمَعۡنَٰهُمۡ جَمۡعٗا[9]

Yaani, itakapokaribia ile ahadi ya Mwenyezi Mungu, Mwenyezi Mungu Atauvunjavunja ule ukuta unaowazuia Yajuja na Majuja, na ahadi ya Mwenyezi Mungu ni ya kweli. Siku hiyo, yaani katika zama za utawala wa Yajuja na Majuja, Tutawapa muhula makundi mbalimbali ili wagongana wao kwa wao, yaani kila kundi litataka kulishindisha dhehebu lake na dini yake dhidi ya makundi mengine. Na kama vile wimbi hutaka

---

[9] Sura Al-Kahf, 18: 99-100. Mwenezi.

kukikandamiza kitu kile linachoangukia, vivyo hivyo mfano wa wimbi baadhi ya makundi hayo yatayaangukia mengine ili kuyakandamiza, na upande wowote hautaacha nafasi yoyote. Kila kundi litafanya juhudi ya kuifikisha dini yake kileleni. Watakuwa ndani ya vita hivyo litakapopulizwa baragumu kwa amri ya Mwenyezi Mungu, ndipo tutayakusanya makundi yote kwenye dini moja.[10] Kupulizwa baragumu hapa kunaashiria kuwa kufuatana na desturi za Mwenyezi Mungu wakati ule msuluhishi mmoja kutoka kwa Mwenyezi Mungu

[10] Maelezo ya Pembeni: Kuhusu aya hizi mtu mwenye uzoefu mdogo asifikirie kuwa baada ya sehemu hizo zote mbili imetajwa jahanamu, na muktadha wa maelezo kwa dhahiri unaonyesha kuwa kisa hiki kinaongelea habari za akhera. Lakini ikumbukwe kuwa ni njia ya kawaida ya Kurani Tukufu — na kuna mifano yake mamia katika Neno lake Takatifu — kuwa pamoja na habari moja ya kidunia inaunganishwa habari ya akhera, na kila sehemu ya maneno ina dalili ya kupishana na sehemu nyingine. Na ndivyo staili hii ilivyojaa Kurani Tukufu. Kwa mfano, uangalieni tu muujiza wa kupasuka mwezi. Hiyo ilikuwa ni ishara moja, lakini pamoja nayo imeongelewa habari ya kiyama. Kwa sababu hiyo baadhi yao wasio na ujuzi wasipojali dalili wanasema kuwa tukio hili la mwezi kupasuka halikutokea bali litatokea siku ya kiyama. Mwandishi.

atazaliwa akisaidiwa na misaada ya kimbingu, na moyoni mwake itapulizwa roho ya uhai, na uhai huo utapenya ndani ya wengine. Ikumbukwe kuwa neno baragumu daima huashiria kwenye mabadiliko makubwa sana. Yaani, Allah anapowahamisha viumbe wake kutoka hali moja kwenye hali nyingine, basi wakati wa mabadiliko haya huitwa kupulizwa baragumu. Na wazionao kashfi huhisi pia uwepo wa baragumu hili kimwili pia. Na haya ni ya maajabu ya ulimwengu ule, ambayo siri zake hazitobolewi kwa yeyote minghairi ya wajitenganao na dunia. Kwa vyovyote, kutokana na aya hizo inathibitika kuwa katika zama za mwisho Ukristo na dola la Kikristo litakuwa na nguvu duniani na migogoro mingi ya kidini itazuka baina ya mataifa mbalimbali. Taifa moja litataka kulikandamiza taifa jingine, na katika zama kama hizo mataifa yote yatakusanywa kwenye dini ya Kiislamu kwa kupulizwa baragumu. Yaani kwa mujibu wa desturi ya Mwenyezi Mungu itapatikana nidhamu ya kimbingu na atafika Msuluhishi mmoja wa kimbingu. Na kwa hakika

jina la Msuluhishi huyu huyu ni Masihi Mau'udi. Kwani, kwa kuwa chanzo cha fitina kitakuwa ni Wakristo, na Mungu Atakusudia kuvunja adhama ya msalaba wao, kwa hiyo yule aliyetumwa kuwaita Wakristo akapewa jina Masihi na Isa kulingana na hali ya wale watu wanaoitwa. Na hekima nyingine ndani yake ni hii kuwa Wakristo walipomfanya Hadhrat Isa kuwa Mungu na kunasibisha kwake mambo kadha ya uzushi na kueneza maelfu ya udanganyifu ardhini na kuzidisha daraja yake kupita kiasi, hapo ghera ya Yule Aliye hai, Mpweke, Asiye na kifani ikataka kumtuma kutoka ndani ya umati huu mja wake mmoja na kuonyesha mwujiza wa kudra ili ithibitike kuwa kumfanya mtu kuwa Mungu ni ujinga. Yeye Humteua Amtakaye na huweza kumnyanyua mtu na kumfikisha mpaka mbinguni. Hapa ifahamike pia kuwa katika zama za ufisadi Msuluhishi anapokuja, wakati wa kudhihiri kwake mtawanyiko wa nuru hutokea kutoka mbinguni. Yaani pamoja na kushuka kwake, nuru pia hushuka ardhini na kuziteremkia nyoyo

zilizo tayari kuipokea, ndipo dunia sharti inao uwezo huelekea kwenye wema na heri, na kila moyo hujawa na shauku ya kufanya utafiti na uchunguzi, na kwa sababu zisizojulikana kila tabia yenye bidii inataharuki kwa kutafuta haki. Ilmuradi, upepo wa aina fulani huvuma unaoielekeza mioyo ya wafanya juhudi kuelekea Akhera na huziamsha nguvu zilizolala, na zama huonekana kana kwamba zinaelekea kwenye mapinduzi makubwa. Basi, alama hizi huwa shahidi juu ya jambo hili kuwa Msuluhishi yule ameshazaliwa duniani. Kisha, kadri msuluhishi huyo alivyo mwenye shani kubwa, harakati hizi za ghaibu zinafanya kazi kwa nguvu ndani ya mioyo ya wanaojitahidi. Kila mwenye asili ya wema huzinduka asijue nani kamzindua. Kila mwenye asili iliyo sawa anapata mabadiliko ndani mwake, asiweze kujua kuwa mabadiliko haya yamekujaje. Ilmuradi mtikisiko fulani huanzia mioyoni, na wapumbavu hufikiri kuwa huo umejitokeza wenyewe, lakini kwa hakika, nyuma ya pazia, nuru hizo huteremka pamoja na Mjumbe au

Mujadidi. Habari hii imefafanuliwa vizuri sana katika Kurani Tukufu na Hadithi na inathibitika kama Asemavyo Mwenyezi Mungu:

إِنَّآ أَنزَلْنَٰهُ فِى لَيْلَةِ ٱلْقَدْرِ وَمَآ أَدْرَىٰكَ مَا لَيْلَةُ ٱلْقَدْرِ لَيْلَةُ ٱلْقَدْرِ خَيْرٌ مِّنْ أَلْفِ شَهْرٍ تَنَزَّلُ
ٱلْمَلَٰٓئِكَةُ وَٱلرُّوحُ فِيهَا بِإِذْنِ رَبِّهِم مِّن كُلِّ أَمْرٍ سَلَٰمٌ هِىَ حَتَّىٰ مَطْلَعِ ٱلْفَجْرِ [11]

Yaani, hakika Sisi Tumekiteremsha Kitabu hiki na Nabii huyu katika usiku wa heshima. Je, unajua kuwa usiku wa heshima ni nini? Usiku wa heshima ni bora kuliko miezi elfu. Ndani yake huteremka malaika na roho mtakatifu kwa idhini ya Mola wao. Na wakati huo huwa wa amani kwa kila jambo mpaka Alfajiri ipambazuke. Sasa, ingawa kwa itikadi ya kidhahiri ya Waislamu, Lailatul Kadri ni jina la usiku uliobarikiwa, lakini Mwenyezi Mungu alivyoniarifu, uhakika wake ni huu kuwa pamoja na tafsiri inayokubalika na kaumu, Lailatul Kadri pia ni zama zile ambamo giza huenea duniani, sehemu zote hutanda giza tu, ndipo giza hilo huhitaji nuru ishuke kutoka mbinguni. Basi, Mwenyezi Mungu wakati huo

[11] Sura Al-Qadr, 97: 2-6. Mwenezi.

huteremsha ardhini malaika wake wenye nuru na roho mtakatifu pia kwa mteremko unaoafikiana na hali ya shani ya malaika. Ndipo Roho Mtakatifu hufungamana na yule Mujaddid na Msuluhishi ambaye akiteuliwa anatumwa kuita kwenye haki, na malaika hufungamana na wale wote walio wasikivu, waongofu na wafanyao juhudi, na huwavutia kwenye wema na kuweka njia za wema mbele yao, ndipo wema na usalama huenea, na huendelea kuwa hivyo mpaka dini inapofikia upeo wa mafanikio uliokadiriwa.

Sasa inatakiwa iangaliwe kuwa Mwenyezi Mungu Amekwisha sema katika sura hii iliyobarikiwa kwa maneno ya uwazi kabisa kuwa wakati anapokuja Msuluhishaji kutoka kwa Mwenyezi Mungu, basi lazima huteremka malaika kutoka mbinguni wanaoiamsha mioyo ndipo kwa kuteremka kwao mioyo hupata joto la mwelekeo kwenye wema na haki. Basi, kudhani kuwa joto hilo huzalika lenyewe bila ya kudhihiri kwa Msuluhishi ni kinyume cha Neno la Mungu na kanuni yake ya

kudumu, na matamshi kama hayo hutoka katika vinywa vya wale tu wasiotambua siri za Mungu na wanafuata dhana zao zisizo na msingi wowote. Bali hizi ni alama maalum za kuzaliwa kwa Muslih Mtakatifu na ni mfano wa chembe ambazo zinalizunguka jua. Naam, kutambua hakika yake si kazi ya kila mtu. Mtazamo wenye moshi moshi wa mtu wa kidunia hauwezi kuigundua nuru hiyo. Machoni pake kweli za dini ni jambo la kichekesho tu, na anaona maarifa ya kiungu kuwa ni mambo ya kipumbavu.

Na aya nyingine zinazozungumzia alama za zama hizi za mwisho, yaani aya zile zinamoelezwa kwanza habari za giza la kiardhi kutanda sana na kisha zimetolewa alama za kuteremka mwanga wa kimbingu ni hizi:

إِذَا زُلْزِلَتِ الْأَرْضُ زِلْزَالَهَا وَأَخْرَجَتِ الْأَرْضُ أَثْقَالَهَا وَقَالَ الْإِنْسَانُ مَا لَهَا يَوْمَئِذٍ تُحَدِّثُ أَخْبَارَهَا بِأَنَّ رَبَّكَ أَوْحَىٰ لَهَا[12]

Yaani, zama za mwisho zitawadia itakapotetemeshwa ardhi kwa mtetemeko wa kutisha kwa kiwango kilicho

---

[12] Sura Az-Zilzaal, 99:2-6. Mwenezi.

sawa na hali yake. Yaani, watu watapata mabadiliko makubwa, wataelekea kwenye mambo ya anasa na mapenzi ya dunia. Kisha Akasema kuwa ardhi itatoa mizigo yake yote. Yaani, elimu za kiardhi, hila za kidunia na ujanja na vipawa vya kidunia alivyojaliwa binadamu, vyote hivyo vitadhihirika. Na ardhi anamoisha mwanadamu itatoa sifa zake na kwa njia ya elimu ya fizikia na kilimo, sifa zake nyingi zitajulikana. Migodi itadhihiri, shughuli za kilimo zitazidi sana. Ilimuradi, ardhi itarutubika sana, mashine za namna namna zitavumbuliwa mpaka mtu atasema kuna nini hii? Elimu hizi mpya mpya na fani mbalimbali mpya na viwanda vipya vipya vinavumbuliwaje!! Ndipo ardhi, yaani mioyo ya wanadamu itasimulia habari zao kwa hali kuwa mambo yote haya mageni yanayotokea siyo kutoka kwetu bali ni wahyi wa aina fulani kutoka kwa Mwenyezi Mungu, kwani haiyumkiniki kuwa mwanadamu aweze kwa juhudi zake kuzalisha elimu za ajabu kiasi hiki.

Na ikumbukwe kuwa aya nyingine za Kurani Tukufu

zihusikanazo na Akhera zilizounganishwa na aya hizi, kwa hakika zimejumuishwa sawa na suna ile ya Mungu iliyokwisha elezwa hapo kabla, waila hakuna shaka kabisa kuwa maana halisi za aya hizi ni zile nilizoeleza. Na kielekezi madhubuti juu yake chenye kuamua ni kuwa kama aya hizi zitafsiriwe kwa maana zake za kidhahiri, hapo zitatokea fujo kubwa. Yaani, kama tukitafsiri kwamba wakati fulani, juu ya uwepo wa watu waliopo duniani, ardhi itapatwa na matetemeko makali ya kupindua juu kuwa chini na chini kuwa juu, basi hilo ni miongoni mwa mambo yasiyoyumkinika, yasiyowezekana kabisa. Aya inasema wazi kwamba mtu atasema ardhi imepatwa na nini? Sasa kama ni kweli kuwa ardhi itapinduliwa chini juu, basi mtu atakuwa wapi atakayeiuliza ardhi? Maana, yeye tayari atakuwa amekwisha angamia pamoja na tetemeko la kwanza. Elimu za hisia haziwezi kukataliwa kwa vyovyote vile. Basi, kutoa maana ambayo ni potofu na kinyume na dalili zilizopo ni kama kwamba kuidharaulisha Islam

na kuwapa wapinzani mwanya wa kuleta upingamizi. Basi maana halisi na ya kweli ni ile tu tuliyoieleza sasa hivi. Sasa ni dhahiri kuwa mabadiliko haya, fitina na matetemeko katika zama zetu yamedhihiri kutoka kwa Wakristo tu ambayo mfano wake haupatikani katika dunia. Basi hii ni dalili ya pili inayoonyesha kuwa taifa hili ndilo taifa la mwisho lililopangiwa fitina za aina aina kuenea kwa mkono wake, ambalo likaonyesha duniani mambo ya aina aina ya udanganyifu. Na kama ilivyoandikwa kwamba dajali atadai unabii na pia atadai uungu, basi mambo yote haya mawili yamedhihirika kwa taifa hili. Dai la unabii kwa njia hii kwamba mapadri wa taifa hili wamejasiri kuviingilia vitabu vya Manabii, na kuviingilia pasipo hofu kana kwamba wao ndio Manabii, wakaelekeza maandishi ya vitabu walikotaka, na wakaandika maelezo sawa na matakwa yao na kila mahali wakajiingiza na kuzusha; wakayaficha yaliyokuwepo, na wakayadhihirisha yasiyokuwepo. Na wakasisitiza kwa nguvu sana tafsiri zao potofu kana kwamba wahyi

umewateremkia na wao ndio manabii. Hivyo, daima inaonekana kwamba wakati wa majadiliano na midahalo yao kwa makusudi tu hutoa majibu ya kijinga na yaliyo mbali na ukweli, kana kwamba wanafanyiza Injili mpya. Kadhalika vitabu vyao pia vinaelekeza kwenye Isa mpya na Injili mpya, na hawaogopi katu wakati wa kusema uongo. Nao kwa njia ya ujanja wameandika mamilioni ya vitabu juu ya dai lao hili la uongo, kana kwamba wameishamuona Hadhrat Isa akijikalia kiti cha Kiungu. Na wakatoa madai ya kiungu hivi kwamba wakajiingiza katika kazi za Mungu kupita kiasi, na wakataka kwamba katika dunia pasiwepo na siri hata moja wasiyoifikia hakika yake. Wakatamani kuchukuwa kazi zote za Mwenyezi Mungu mikononi mwao, kwa njia yoyote wajipatie 'mtambo' wa Kiungu hata kwamba kama ikiwezekana wawe na madaraka juu ya jua kuchwa na kucha. Kunyesha mvua na kutonyesha kuwe ni kwa sababu ya mbinu yao, na kusiwepo na jambo lolote lisilowezekana kwa. Dai la kuwa Mungu ni nini tena?

Ni kujaribu kujiingiza katika kudra mahususi za Mungu, na kuwa na shauku ya kujichukulia mahali pa Mungu. Watu wale wanaozipinga Hadithi kuhusiana na Masihi Mau'udi na Hadithi zinazohusu dajali wanatakiwa wafikirie sana hapa kuwa kama bishara hizo zisingekuwa kutoka kwa Mwenyezi Mungu na ungekuwa ni utungo tu wa binadamu, isingeyumkinika kutimia barabara na sawasawa kabisa. Je hii pia ilikuwa katika fikara ya mtu kuwa taifa hili la Kikristo katika zama fulani litajibidiisha sana na kutumia ulaghai kwa kumfanya mtu kuwa Mungu na halitamwachia Mungu daraja lolote mahususi kwa Mungu katika uchumbuzi wao wa kifalsafa. Angalieni, punda wa dajal ambaye umbali baina ya masikio yake mawili, imeandikwa kuwa pima 70, huo unawiana mara nyingi na mabehewa ya garimoshi. Na kama iliyoelezwa ndani ya Kurani Tukufu na Hadithi kuwa katika zama zile usafiri wa ngamia utaachwa, ndivyo tuonavyo kuwa usafiri wa garimoshi ndio umeushinda usafiri huo wote, na sasa huo unahitajika kidogo sana, na pengine

hautahitajika kabisa baada ya muda mfupi. Vivyo hivyo tumeona kwa hakika kuwa wataalamu na wanafalsafa wa taifa hili wamedhihirisha fitina ambazo mfano wake haupatikani tangu Hadhrat Adam hadi sasa. Basi, wakaingilia katika unabii pia na uungu vilevile. Sasa uwe uthibitisho gani zaidi juu ya ukweli wa Hadithi hizo kuliko huu kwamba bishara ziliyoelezwa ndani ya hizo imetimia tayari. Na ndani ya aya hizi za Kurani Tukufu, yaani

إِذَا زُلْزِلَتِ الْأَرْضُ زِلْزَالَهَا[13]

kwa hakika kuna ishara kwenye zama hizi hizi za kidajali ambayo hata mwenye akili ndogo sana anaweza kuelewa. Na aya hii inaeleza wazi kabisa kuwa watu hawa wataendelea kiasi gani katika elimu za ardhi.

Kisha katika alama za zama hizo ambapo elimu na fani zitatolewa kutoka ardhini, imeeleza baadhi ya uvumbuzi na sanaa kama mfano, nao ndio huu:

---

[13] Sura Az-Zilzaal, 99:2. Mwenezi.

وَإِذَا الْأَرْضُ مُدَّتْ وَأَلْقَتْ مَا فِيهَا وَتَخَلَّتْ[14]

ardhi itakapotanuliwa, yaani ardhi itasafishwa na idadi ya watu kuongezeka, na ardhi itatoa yote yaliyomo ndani mwake na kubaki tupu. Yaani nguvu zote za ardhi zitadhihirika kama ilivyokwisha elezwa huko nyuma.

وَإِذَا الْعِشَارُ عُطِّلَتْ[15]

yaani wakati huo ngamia jike wataachwa na hawatakuwa na hadhi yoyote. عِشار (‘ishaar) ni ngamia jike mwenye mimba, ambaye hupendwa sana na Waarabu. Ni dhahiri kuwa aya hii haina uhusiano wowote na kiyama, kwani kiyama siyo mahali ambapo ngamia dume na jike wapandane ikatungwe mimba. Bali hii yaashiria kuvumbuliwa garimoshi. Sharti ya kuwa ‘mwenye mimba’ imetajwa ili iwe dalili ya kutukia habari hii duniani humu pasipo kufikiria Akhera hata kidogo. وَإِذَا الصُّحُفُ نُشِرَتْ[16] Na wakati ambapo vitabu vitaenezwa na kutawanywa. Yaani, njia za kueneza vitabu zitapatikana.

[14] Sura Alinshiqaaq, 84:4-5. Mwenezi.
[15] Sura At-Takwiir, 81:5. Mwenezi.
[16] Sura At-Takwiir, 81:11. Mwenezi.

Hii inaashiria kwenye viwanda vya uchapaji na posta kwamba katika zama za mwisho hivyo vitakuwepo kwa wingi sana. وَإِذَا النُّفُوسُ زُوِّجَتْ[17] Na nafsi zitakapounganishwa. Hii inaashiria kwenye uhusiano baina ya mataifa na nchi mbalimbali. Maana yake ni kwamba katika zama za mwisho kwa sababu ya njia kadha kufunguliwa na utaratibu wa posta na telegramu, uhusiano baina ya mataifa utazidi, taifa moja litakutana na taifa jingine, uhusiano wa mbali na mwungano wa uhusiano wa kibiashara utaimarishwa na uhusiano wa urafiki utazidi. وَإِذَا الْوُحُوشُ حُشِرَتْ[18] Wakati wanyama watakapokusanywa pamoja na watu. Yaani mataifa yasiyostaarabika yatarejea kwenye ustaarabu na utu, na watu duni watapata daraja za kidunia na heshima, na kwa sababu ya elimu na fani za kidunia kuenea hakutakuwa na tofauti kati ya wenye heshima na watu duni. Bali watu duni watakuja juu mpaka ufunguo wa utajiri na utawala utakuwa mkononi

---

[17] Sura At-Takwiir, 81:8. Mwenezi.
[18] Sura At-Takwiir, 81:6. Mwenezi.

mwao. Madhumuni haya yamo pia ndani ya Hadithi moja. وَاِذَاالۡبِحَارُ فُجِّرَتۡ[19] Wakati mito itakapopasuliwa, yaani, mifereji itaenea ardhini na ukulima utazidi sana. وَاِذَا الۡجِبَالُ نُسِفَتۡ[20] Na milima itakapovunjiliwa mbali, na hapo zitatengenezwa barabara kwa waendao kwa miguu na kwa usafiri na pia kwa ajili ya kutandaza reli. Kisha ikaeleza alama za giza na ikasema اِذَاالشَّمۡسُ كُوِّرَتۡ[21] wakati jua litakapofunikwa. Yaani, giza la ujahili na maasi litaenea duniani. وَاِذَاالنُّجُوۡمُ انۡكَدَرَتۡ[22] Nyota zitakapochafuka. Yaani nuru na ikhlasi ya wanazuoni itatoweka. وَاِذَاالۡكَوَاكِبُ انۡتَثَرَتۡ[23] Na nyota zitakapoanguka. Yaani wanazuoni wacha Mungu watakuwa wamefariki, kwani haiwezekani kuwa nyota zianguke ardhini na watu waendelee kuishi. Ikumbukwe kuwa utabiri kama huu umo katika Injili pia kwamba Masihi Mau'udi atakuja wakati nyota ziatkapoanguka ardhini na nuru ya jua na mwezi itakapotoweka. Bishara

[19] Sura Alinfitaar, 82:4. Mwenezi.
[20] Sura Al-Mursalaat, 77:11. Mwenezi.
[21] Sura At-Takwiir, 81:2. Mwenezi.
[22] Sura At-Takwiir, 81:3. Mwenezi.
[23] Sura Alinfitaar, 82:3. Mwenezi.

hizi haziwezi kuchukuliwa kidhahiri, na hakuna mtu mwenye akili anayeweza kutoa rai kuwa kwa kweli mwanga wa jua uondoke na nyota zote zianguke ardhini na hata hivyo ardhi iendelee kukaliwa na watu kama kawaida, na katika hali hii Masihi Mau'udi aje. Mungu Alisema tena [24]إِذَا السَّمَآءُ انشَقَّتْ Wakati mbingu zitakapopasuka. Kadhalika Akasema [25]إِذَا السَّمَآءُ انفَطَرَتْ Na sawa na hii Injili pia imetoa habari ya kufika kwa Masihi Mau'udi. Lakini aya hizi hazimaanishi kwamba kweli mbingu itapasuka au nguvu zote zitalegea, bali muradi wake ni kwamba kama vile kitu kilichopasuka hakiwezi kufaa tena, vivyo hivyo mbingu pia itakuwa kana kwamba haifai. Baraka hazitashuka kutoka mbinguni, na dunia itajaa kiza. Kisha Akasema [26]وَإِذَا الرُّسُلُ أُقِّتَتْ na mitume watakapoletwa katika wakati uliopangwa. Hii kwa kweli inaashiria kuja kwa Masihi Mau'udi, na inakusudiwa kueleza kwamba yeye atakuja barabara katika wakati uliowekwa. Ikumbukwe

[24] Sura Alinshiqaaq, 84:2. Mwenezi.
[25] Sura Alinfitaar, 82:2. Mwenezi.
[26] Sura Al-Mursalaat, 77:12. Mwenezi.

kwamba katika Neno la Mungu neno RUSUL hutumika pia kwa rasuli mmoja na pia kwa asiye Rasul. Nami nimeshaeleza mara nyingi kuwa aya za Kurani Tukufu zina jiha nyingi kama inavyothibitika kutoka katika Hadithi kuwa Kurani ina dhahiri na batini pia. Kwa hiyo, kama manabii wakikusanyika katika uwanja siku ya kiyama kutoa ushahidi, tunaamini na tunasadikisha. Lakini mahali hapa baada ya kueleza alama mbaya za zama za mwisho, mwishoni akasema pia kuwa wakati ule mitume wataletwa katika wakati uliowekwa, basi dalili bayana zinashuhudia waziwazi kuwa baada ya upeo ule wa giza Mwenyezi Mungu Atamtuma Mtume wake mmoja ili iamuliwe baina ya mataifa mbalimbali. Na kwa vile imekwishathibitika kutoka katika Kurani Tukufu kuwa upotofu huo utakuwa kutoka kwa Wakristo, bila shaka Mtume huyo atatumwa kuwaita na kuwaamulia, ndiyo maana kwa mnasaba huo huyo ameitwa jina Isa, kwani yeye ametumwa kwa ajili ya Wakristo kama nabii Isa alivyokuwa ametumwa kwao

mwanzoni. Na ndani ya aya وَاِذَاالرُّسُلُ اُقِّتَتۡ[27] *alif laam* yaashiria kwenye *A'hd Kharijii*. Yaani, yule mujadid aliyeahidiwa kutumwa, kama alivyosema Mtume[saw], atatumwa katika wakati wa giza hilo la Kikristo.

Mpaka sasa aya za Kurani Tukufu tulizoziandika zinaonyesha dhahiri shahiri kuwa lazima bishara hii imo ndani ya Kurani Tukufu kuwa katika zama za mwisho Ukristo utaenea duniani sana na watu hao watakusudia kuifutilia mbali dini ya Kiislamu kutoka uso wa ardhi, na kadri watakavyoweza hawataacha kufanya kila mbinu kuistawisha dini yao. Ndipo Mwenyezi Mungu Ataelekea kuisaidia dini ya Kiislamu. Na katika wakati huo wa fitina ataonyesha namna Alivyo Mlinzi wa dini yake na Kitabu chake kitakatifu. Ndipo kwa mujibu wa desturi na suna yake, mwanga kutoka mbinguni utashuka na kila mtu mwema atavutwa kwenye mwanga huo mpaka watu wote wenye

---

[27] Na mitume watakapokusanywa katika wakati maalum. Sura Al-Mursalaat, 77:12. Mwenezi.

asili ya wema watakusanyika chini ya bendera ya dini moja. Mwenyezi Mungu Ameishasema kwa maneno ya wazi kuwa baragumu litapulizwa wakati wa kelele za vita na mahojiano. Ndipo watu wema watakusanywa katika dini moja. Na Amesema vilevile kuwa katika wakati wa giza mitume watatumwa. Sasa itamaanisha nini tena kuwa Mwenyezi Mungu Mtukufu kwanza alieleza kuwa alama ya zama za mwisho ni Yajuja na Majuja kupata nguvu, yaani Urusi na Waingereza kutawala duniani. Tena alama ya pili ni madhehebu mengi kupatikana. Na alama ya tatu ni madhehebu hayo kujadiliana, na kila moja kuliangukia jingine kama wimbi. Na alama ya nne ni kuvumbuliwa usafiri wa garimoshi. Na  alama ya tano ni kuvumbuliwa kwa mitambo ya kueneza vitabu na magazeti kama vile matbaa na telegramu. Alama ya sita ni kupasuliwa kwa mifereji. Alama ya saba ni kuongezeka kwa idadi ya watu na upanuzi wa kilimo. Alama ya nane ni

kupasuliwa kwa milima. Alama ya tisa ni kuendelea kwa elimu zote na fani za kisasa kupata maendeleo. Alama aya kumi ni kuenea kwa dhambi na giza, na kutoweka ucha Mungu, utawa na nuru ya imani. Na alama ya kumi na moja ni kutokea kwa *Daabbatul Ardhi*, yaani kuenea kwa watoao mawaidha wasio na nuru ya kimbingu hata chembe. Hao ni wadudu wa ardhi, matendo yao yapo upande wa dajali na ndimi zao ziko upande wa Islam. Yaani kimatendo wao ni watumishi wa dajali, sura zao zimegeuzwa na wanadhihirisha sura za kinyama ingawa ndimi zao ni kama za kibinadamu. Na alama ya kumi na mbili ni kuzaliwa kwa Masihi Mau‘udi ambako kiistiara kumeelezwa katika Neno la Mungu kwamba ni kupulizwa kwa baragumu. Na kupulizwa kwa hakika ni kwa namna mbili: kupulizwa kwa kupoteza (fahamu) na kupulizwa kwa mwongozo. Aya hii inaashiria kwenye habari hii:

وَنُفِخَ فِي الصُّوْرِ فَصَعِقَ مَنْ فِي السَّمٰوٰتِ وَمَنْ فِي الْاَرْضِ اِلَّا مَنْ شَآءَ اللّٰهُ ثُمَّ نُفِخَ فِيْهِ اُخْرٰى

فَإِذَا هُمْ قِيَامٌ يَنْظُرُونَ[28]

Aya hizi zina jiha mbalimblai, zinahusiana na kiyama na pia dunia hii, kama ilivyo Aya hii:

اِعْلَمُوْٓا اَنَّ اللّٰهَ يُحْيِ الْاَرْضَ بَعْدَ مَوْتِهَا[29]

Yaani, jueni ya kwamba Mwenyezi Mungu huihuisha ardhi baada ya mauti yake. Na ilivyo aya فَسَالَتْ اَوْدِيَةٌۢ بِقَدَرِهَا[30] na mabonde yakatiririka maji kwa kadri yao. Na kuhusiana na ulimwengu huu aya hizo zinamaanisha kwamba katika siku za mwisho zitakuja zama za aina mbili. Moja ni zama za upotevu. Katika zama hizo kila mtu wa ardhini na wa mbinguni, yaani kila mtu mwovu na mwema atapata kughafilika ila alindwaye na Mwenyezi Mungu. Kisha zitakuja zama za pili za uongofu, hapo mara wote watasimama ghafla, nao wataangaza. Yaani, mghafala utatoweka na

[28] Tafsiri: Na litapulizwa baragumu, ndipo watazimia waliomo mbinguni na waliomo ardhini ila yule Amtakaye Mwenyezi Mungu. Tena litapulizwa mara nyingine, ndipo watasimama wakiangalia. Sura Az-Zumar, 39:69. Mwenezi.

[29] Sura Al-Hadid, 57:18. Mwenezi.

[30] Sura Ar-Ra'd, 13:18. Mwenezi.

maarifa yataingia mioyoni. Wenye bahati mbaya watatambua ubaya wao ingawaje hawataamini.

Mbali na aya hizi, ndani ya Kurani Tukufu kuna aya nyingi zinazoelezea juu ya zama za mwisho na juu ya kuja kwa Masihi Mau'udi. Lakini machimbuko ya maana hizi zenye mibaraka ni mepesi ambayo mtu mwenye elimu ya juu juu hawezi kuelewa, na ufahamu mdogo hauwezi kuzipata maana hizi nyepesi. Basi miongoni mwa aya hizo kuna aya hii:

إِنَّآ أَرْسَلْنَآ إِلَيْكُمْ رَسُولًا شَاهِدًا عَلَيْكُمْ كَمَآ أَرْسَلْنَآ إِلَىٰ فِرْعَوْنَ رَسُولًا[31]

Sasa ni dhahiri kuwa neno *Kama* linaashiria kuwa Mtume wetu s.a.w. ndiye mfano wa Musa[as]. Ndani ya Torati, mlango wa Kumbukumbu la Torati[32] imeandikwa kuwa Mtume[saw] ndiye mfano wa Musa[as]. Na ni dhahiri kuwa kumithilishwa huku ni kumithilishwa kikamilifu siyo kumithilishwa kwa kasoro, maana kama

---

[31] Sura Al-Muzzammil, 73:16. Tafsiri yake: Hakika Sisi Tumewatumieni Mtume aliye shahidi juu yenu, kama Tulivyompeleka Mtume kwa Firauni. Mwenezi.

[32] Kumbukumbu la Torati, 18:18. Mwenezi.

kufananishwa huku ni kwa kasoro hapo Mtume[saw] peke yake hatahusikana na kufanana huko, kwani manabii wengi watathibitika wenye kufananishwa huko walioinua upanga kwa idhini ya Mwenyezi Mungu na wakapigana vita pia kama Hadhrat Musa na wakapata ushindi kwa njia ya ajabu. Lakini, je hawa wanaweza kuwa wasadikishaji wa bishara hii? La hasha. Hivyo basi, Mtume[saw] wetu anaweza kuhusikana na bishara hii hapo tu ambapo kumithilishwa huko kuwe kikamilifu. Na sehemu mojawapo ya sehemu zeneye shani kubwa ni hii pia ya kuwa baada ya Mwenyezi Mungu kumpa nabii Musa utume, Akampa heshima na neema ya kuweka katika sheria yake silsila ya Ukhalifa wa dhahiri na batini iliyofululiza kwa muda mrefu iliyoendelea miaka elfu moja na kumi na minne na kuishia kwa nabii Isa[as]. Katika kipindi hicho mamia ya wafalme na watu walioteremshiwa wahyi walipatikana chini ya sheria ya nabii Musa. Na daima Mwenyezi Mungu Aliendelea kuwasaidia wafuasi wa sheria ya nabii Musa kwa njia ya

ajabu na kumbukumbu hizi zilihifadhiwa katika vitabu vya historia, kama Anavyosema Mwenyezi Mungu:

وَلَقَدْ آتَيْنَا مُوسَى الْكِتَابَ وَقَفَّيْنَا مِن بَعْدِهِ بِالرُّسُلِ [33]

ثُمَّ قَفَّيْنَا عَلَىٰ آثَارِهِم بِرُسُلِنَا وَقَفَّيْنَا بِعِيسَى ابْنِ مَرْيَمَ وَآتَيْنَاهُ الْإِنجِيلَ وَجَعَلْنَا فِي قُلُوبِ الَّذِينَ اتَّبَعُوهُ رَأْفَةً وَرَحْمَةً [34]

Yaani, Bila shaka Tulimpa Musa kitabu na tukawafuatisha mitume wengi baada yake. Kisha baada ya hao wote tukamtuma Isa mwana wa Mariam na kumpa Injili na Tukauweka upole na rehema katika mioyo ya wale waliomfuata, yaani si kwa upanga bali kwa kujinyenyekeza na kwa khulka njema walikuwa wanawaita watu kwenye dini. Ndani ya aya hii kuna ishara hii kuwa ingawa sheria ya Musa ilikuwa ya kijalali, na malaki ya watu waliuawa kwa amri ya sheria hii, na watoto wachanga karibu laki nne wakauawa, lakini Mwenyezi Mungu Alitaka kuimalizia silsila hii kwa rehema, na kutoa miongoni mwao watu ambao si kwa upanga, bali kwa elimu na khulka njema na nguvu yao takatifu walete wanadamu

[33] Sura Al-Baqara, 2:88. Mwenezi.
[34] Sura Al-Hadiid, 57:28. Mwenezi.

kwenye njia iliyonyoka.

Sasa kwa vile ni lazima kufanana kuwe katika neema, na kufanana kikamilifu kuliweza kuthibitika hapo tu ambapo kufanana kuthibitike katika neema, basi ndiyo maana ikawa kwamba kama vile nabii Musa[as] alivyojaliwa watumishi wa sheria yake mpaka kwa miaka elfu moja na kumi na minne waliokuwa mitume kutoka kwa Mungu na waliofunuliwa na Mwenyezi Mungu, na silsila hii ikaishia kwa Mtume ambaye aliwaita watu si kwa upanga, bali kwa rehema na khulka njema, kadhalika Mtume wetu[saw] alijaliwa watumishi wa sheria ambao sawa na Hadithi:

علماء امتی کانبیاء بنی اسرائیل[35]

walikuwa wanafunuliwa funuo na wakaongea na Mungu. Na kama vile katika zama za mwisho, za sheria ya Musa[as], alivyotumwa Hadhrat Masih[as] aliyewaita watu kwenye haki si kwa upanga, bali

---

[35] Wanazuoni wa umati wangu ni kama manabii wa Wana wa Israeli. Mwenezi.

kwa khulka njema na upole, ndivyo Mwenyezi Mungu Alivyomtuma Masihi Mau'udi ili naye pia awaite watu kwenye njia iliyonyoka kwa khulka njema na upole na kwa nuru za kimbingu. Na kama vile Hadhrat Masihi alivyokuja karibu miaka mia moja na kumi na minne baada ya Hadhrat Musa[as], ndivyo Masihi Mau'udi huyu pia alivyodhihiri mwanzoni mwa karne ya kumi na nne. Hivyo silsila ya Muhammad[saw] ikalingana barabara na silsila ya Musa[as]. Na kama ikisemwa kuwa katika silsila ya Musa[as] manabii waliendelea kuja kuihami dini, na Hadhrat Masihi pia alikuwa nabii, basi jibu lake ni kwamba katika kutumwa, Nabii na Muhaddath wana hadhi moja. Na kama Mwenyezi Mungu Alivyowaita manabii jina *Mursal*, ndivyo alivyowaita Muhaddathina pia jina *Mursal*. Kwa kuashiria kwenye jambo hili Mungu Anasema ndani ya Kurani:

وَقَفَّيْنَا مِنْ بَعْدِهٖ بِالرُّسُلِ[36]

Haikusemwa [37]وقفّينا من بعده بالانبياء . Basi hii inaashria kwenye jambo hili kuwa *Rusul* muradi wa ni *Mursal,* wawe Rasul au Nabii au Muhaddath. Kwa vile Seyidna Mtume[saw] ni Khatamul Ambiyaa, na hakuna nabii awezaye kuja baada yake, kwa hiyo katika sheria hii *Muhaddath* amewekwa badala ya Nabii, na aya hii ndiko inakoashiria:

ثُلَّةٌ مِّنَ الْاَوَّلِيْنَ وَ ثُلَّةٌ مِّنَ الْاٰخِرِيْنَ[38]

Kwa vile neno ثُلّة limetumika katika sentensi zote mbili, hivyo hapa inathibitika kabisa kuwa Muhaddathina wa umati huu kwa idadi na urefu wa zama zao ni sawa na mitume wa umati wa Musa[as] na ndiko aya hii ya pili inakoashiria, nayo ndiyo hii:

وَعَدَ اللّٰهُ الَّذِيْنَ اٰمَنُوْا مِنْكُمْ وَ عَمِلُوا الصّٰلِحٰتِ لَيَسْتَخْلِفَنَّهُمْ فِي الْاَرْضِ كَمَا اسْتَخْلَفَ الَّذِيْنَ

---

[36] Na Tukawafuatisha *Rusul* baada yake. Sura Al-Baqara, 2:88. Mwenezi.

[37] Na Tukawafuatisha manabii baada yake. Mwenezi.

[38] Tafsiri: Jamii kubwa miongoni mwa wa kwanza, na jamii kubwa miongoni mwa wa mwisho. Sura Al-Waaqi‘a, 56:40-41. Mwenezi.

مِنْ قَبْلِهِمْ وَلَيُمَكِّنَنَّ لَهُمْ دِينَهُمُ الَّذِي ارْتَضَىٰ لَهُمْ وَلَيُبَدِّلَنَّهُم مِّن بَعْدِ خَوْفِهِمْ أَمْنًا
يَعْبُدُونَنِي لَا يُشْرِكُونَ بِي شَيْئًا[39]

Yaani, Mwenyezi Mungu Amewaahidi walioamini miongoni mwenu na kufanya vitendo vizuri, bila shaka Atawafanya makhalifa katika ardhi kama Alivyowafanya wale waliokuwa kabla yao. Na kwa yakini Atawaimarishia dini yao Aliyowapendelea na Atawabadilishia amani baada ya hofu yao. Wataniabudu, hawatanishirikisha na chochote. (Juzu 18, Sura Nuur). Sasa angalieni kwa makini kuwa ndani ya aya hii pia mna ishara ya wazi ya kumithilishwa. Kama kumithilishwa huku siyo kikamilifu, basi maneno yote haya hayana maana, maana ukhalifa uliendelea katika sheria ya Musa kwa karne kumi na nne siyo kwa miaka thelathini tu, na mamia ya makhalifa wa kiroho na wa kidhahiri wakapatikana, sio wanne tu kisha ndio ukawa mwisho.

Na kama ikisemwa kuwa neno "*Minkum*" linaashiria kwamba Makhalifa hao watokane na masahaba tu, kwa

[39] Sura An-Nuur, 24:56. Mwenezi.

vile katika "*Minkum*" masahaba wanaambiwa, basi hili ni kosa dhahiri, na atalisema jambo hili yule tu ambaye hajasoma Kurani kwa makini wala hajatambua njia za usemaji wake. Kwani, kama ni kweli kuwa msemaji anaposema 'ninyi' katika mazungumzo, yeye anamaanisha watu wale tu waliopo katika zama zile walio na imani, hapo Kurani nzima itavurugika. Kwa mfano, aya hiyo hapo juu inafanana na aya nyingine ambamo kidhahiri wanaambiwa wale watu waliomwamini Hadhrat Musa na waliokuwa hai wakati huo, bali kuna dalili zilizo wazi zinazoonyesha kuwa walioagizwa ni hao hao tu. Aya zenyewe ni hizi:

قَالَ سَنُقَتِّلُ اَبْنَآءَهُمْ وَ نَسْتَحْيٖ نِسَآءَهُمْ وَ اِنَّا فَوْقَهُمْ قٰهِرُوْنَ۔ قَالَ مُوْسٰی لِقَوْمِهِ
اسْتَعِيْنُوْا بِاللّٰهِ وَ اصْبِرُوْا اِنَّ الْاَرْضَ لِلّٰهِ يُوْرِثُهَا مَنْ يَّشَآءُ مِنْ عِبَادِهٖ وَ الْعَاقِبَةُ
لِلْمُتَّقِيْنَ۔ قَالُوْٓا اُوْذِيْنَا مِنْ قَبْلِ اَنْ تَاْتِيَنَا وَ مِنْ بَعْدِ مَا جِئْتَنَا قَالَ عَسٰی
رَبُّكُمْ اَنْ يُّهْلِكَ عَدُوَّكُمْ وَ يَسْتَخْلِفَكُمْ فِي الْاَرْضِ فَيَنْظُرَ كَيْفَ تَعْمَلُوْنَ[40]

(Juzuu 9, Sura Al-A'raaf).

Yaani, akasema Firauni kuwa tutawaua wavulana wa

[40] Sura Al-A'raaf, 7:128-130. Mwenezi.

Banii Israili na kuwaacha wanawake wao, na bila shaka sisi ni wenye nguvu juu yao, ndipo Musa akawaambia kaumu yake, ombeni msaada kwa Mungu na subirini. Hakika ardhi ni ya Mwenyezi Mungu, Atairithisha kwa Amtakaye katika watumishi wake, na mwisho mwema ni kwa wamchao. Ndipo wakasema watu wa Musa, tuliudhiwa kabla hujatufikia na pia baada ya wewe kutujia. Musa akasema, huenda Mola wenu Atamwangamiza adui wenu na kuwafanyeni makhalifa katika nchi, na Aone jinsi mtakavyofanya.

Sasa katika aya hizi ni wazi kabisa kuwa wanaoambiwa ni wafuasi wa Musa waliokuwa hai mbele yake, nao walilalamikia dhuluma za Firauni na kusema kuwa sisi tuliteswa kabla yako pia na baada ya kuja kwako vilevile. Na hao ndio walioambiwa subirini na vumilieni mateso haya, Mwenyezi Mungu Atawaelekeeni kwa rehema na Atawaangamiza adui zenu na Atawafanyeni makhalifa ardhini. Lakini wanahistoria wanafahamu na wasomi wa vitabu vya Kiyahudi na Kikristo wanajua fika kuwa

ingawa adui wa taifa hilo, yaani Firauni, aliangamia mbele ya macho yao, lakini wao wenyewe hawakupata ukhalifa wa dhahiri wala wa batini, bali wengi wao walihilikishwa kwa sababu ya uasi wao, na kwa miaka arobaini walitangatanga jangwani wakafia humo. Kisha baada ya kuangamia kwao, ukhalifa ulianza ndani ya vizazi vyao, wakatokea ndani yao wafalme wengi, na makhalifa wa Mungu kama Daudi na Suleiman wakazaliwa katika taifa hili hili hata kwamba mfululizo huu wa ukhalifa ukaishia kwa Hadhrat Masihi katika karne ya kumi na nne. Basi, ni dhahiri kuwa maagizo yanapotolewa kwa taifa lililopo sio muradi wake kuwa agizo hilo liishie kwa watu waliopo wakati huo. Bali katika matumizi ya Kurani Tukufu pengine watu fulani wanaambiwa lakini wanaoambiwa hasa ni watu wengine waliokwishapita au watakaokuja baadaye. Kwa mfano Mwenyezi Mungu Mtukufu ndani ya Sura Al-Baqara Akiwaambia Wayahudi waliokuwepo anasema:

يٰبَنِيْٓ اِسْرَآءِيْلَ اذْكُرُوْا نِعْمَتِيَ الَّتِيْٓ اَنْعَمْتُ عَلَيْكُمْ وَ اَوْفُوْا بِعَهْدِيْٓ اُوْفِ بِعَهْدِكُمْ ۚ وَ اِيَّايَ

فَارْهَبُونِ[41]

Yaani, Enyi wana wa Israeli, ikumbukeni neema ile Tuliyowaneemesheni, na itekelezeni ahadi Yangu ili Nami Nitekeleze ahadi yenu, na Niogopeni Mimi.

Sasa ni dhahiri kuwa Wayahudi wa zama za Mtume[saw] ni wale waliopigwa dhila juu yao, wao hawakuteremshiwa neema yoyote wala hawakuahidiwa wamwamini Khatamul Ambiyaa[saw]. Kisha Mwenyezi Mungu Akasema:

وَإِذْ نَجَّيْنَاكُمْ مِنْ آلِ فِرْعَوْنَ يَسُومُونَكُمْ سُوءَ الْعَذَابِ يُذَبِّحُونَ أَبْنَاءَكُمْ وَيَسْتَحْيُونَ نِسَاءَكُمْ وَفِي ذَٰلِكُمْ بَلَاءٌ مِنْ رَبِّكُمْ عَظِيمٌ ۔ وَإِذْ فَرَقْنَا بِكُمُ الْبَحْرَ فَأَنْجَيْنَاكُمْ وَأَغْرَقْنَا آلَ فِرْعَوْنَ وَأَنْتُمْ تَنْظُرُونَ[42]

Yaani kumbukeni ule wakati tulipowaokoeni kwa watu wa Firauni. Waliwapeni adhabu za aina aina, waliwachinja wavulana wenu na kuwaacha hai wanawake wenu na katika hayo lilikuwemo jaribio kubwa kutoka kwa Mola wenu. Na kumbukeni wakati ule tulipoipasua bahari kwa ajili yenu mara tu mlipofika pale na tukawaokoeni

[41] Sura Al-Baqara, 2:41. Mwenezi.

[42] Sura Al-Baqara, 2:50-51. Mwenezi.

na tukawaangamiza watu wa Firauni hali mkitazama. Sasa yapasa kufikiria kuwa miongoni mwa matukio haya hakuna tukio hata moja lililotokea kwa Wayahudi waliokuwepo katika zama za Mtume[saw], wala hawakuteswa kwa mikono ya Firauni, hakuna aliyewaua wavulana wao wala hawakuvushwa kutoka ndani ya mto wowote ule. Kisha Mwenyezi Mungu Anasema:

وَ اِذْ قُلْتُمْ يٰمُوْسٰى لَنْ نُّؤْمِنَ لَكَ حَتّٰى نَرَى اللّٰهَ جَهْرَةً فَاَخَذَتْكُمُ الصّٰعِقَةُ
وَ اَنْتُمْ تَنْظُرُوْنَ۔ ثُمَّ بَعَثْنٰكُمْ مِّنْۢ بَعْدِ مَوْتِكُمْ لَعَلَّكُمْ تَشْكُرُوْنَ۔
وَ ظَلَّلْنَا عَلَيْكُمُ الْغَمَامَ وَ اَنْزَلْنَا عَلَيْكُمُ الْمَنَّ وَ السَّلْوٰى[43]

Yaani, kumbukeni wakati mlipomwambia Musa hatutaamini kwa kusema kwako mpaka tumuone Mwenyezi Mungu kwa macho yetu, ndipo ikawaangukieni radi, hali mnaona. Kisha mkafufuliwa ili mpate kushukuru. Na tukawatilieni kivuli kwa mawingu na tukawateremshieni Manna na Salwa. Sasa ni dhahiri kuwa nabii Musa alifariki miaka elfu mbili kabla ya kuzaliwa Wayahudi wanaoambiwa

---

[43] Sura Al-Baqara, 2:56-58. Mwenezi.

hayo na Kurani Tukufu na hao hawakuwepo asilani katika zama za Musa[as], basi wangeliwezaje kumwuliza Hadhrat Musa swali kama hilo? Wapi waliangukiwa na radi na wapi wakala Manna na Salwa? Je walikuwepo katika zama za Hadhrat Musa ndani ya miili mingine kisha wakaja tena katika zama za Mtume[saw] ndani ya miili tofauti!! Kama si hivyo, basi hakuna tena muradi wake mwingine ila tu kuwa si lazima kwamba wanaoambiwa tukio fulani wawe ndio wale wale wanaoambiwa hasa. Kuhusu Neno la Mungu na Hadithi za Mtume[saw] kuna kanuni hii kuwa pengine tukio moja linanasibishwa kwa mtu au taifa fulani, lakini kwa kweli tukio hilo huwa linamhusu mtu au taifa jingine, na ujaji wa hadhrat Isa bin Mariamu unahusikana na kanuni hii hii. Kwani, ndani ya baadhi ya Hadithi habari fulani ya zama za mwisho imenasibishwa kwa Isa bin Mariamu ilhali yeye alikwisha fariki. Basi tukio hili pia limenasibishwa kwa Hadhrat Masih kama lilivyonasibishwa kwa

Wayahudi wa zama za Mtume[saw] tukio la kusalimika kwao kwa mikono ya Firauni, na kula Manna na Salwa, kuangukiwa na radi na kuvuka mto, na habari ya لَنْ نَّصْبِرَ عَلٰى طَعَامٍ وَّاحِدٍ[44] ilhali hayo yalikuwa ni mambo yaliyohusikana na Wayahudi wa awali waliokwisha kufa mamia ya miaka kabla yao. Kwa hiyo, kama mtu asipofikiria kiakili akifasiria aya hizo na ang'ang'anie tu kwa maneno ya dhahiri, basi hapo kwa uchache utathibitika kuwa imani ya *Tanasukh*[45] ni kweli, waila iliwezekanaje Mwenyezi Mungu anasibishe kitendo cha mtendaji fulani kwa mtu asiyehusika na kitendo hicho, ilhali yeye Mwenyewe anasema لَا تَزِرُ وَازِرَةٌ وِّزْرَ اُخْرٰى[46] Tena, kama watu

[44] Tafsiri: Na kumbukeni mliposema: Ewe Musa, hatutaweza kusubiri juu ya chakula cha namna moja. Sura Al-Baqara, 2:62. Mwenezi.

[45] Tanasukh ni imani ya Waaria na baadhi ya dini nyingine. Maana yake, mtu afapo, roho yake huzaliwa upya mara kwa mara kwa sura mbalimbali kuafikiana na amali zake alizopata kutenda, kama vile sura ya nyani, mbwa, nguruwe na kadhalika. Mwenezi.

[46] Tafsiri: Wala hatabeba mbebaji mzigo wa mwingine. Sura Banii Israaiil, 17:16. Mwenezi.

wa Musa walimwasi Musa na radi ikawaangukia, au walimwabudu ndama na wakateremshiwa adhabu, basi taifa hilo la pili lililozaliwa miaka elfu mbili baadaye lilihusika vipi na matukio hayo? Ingawa kuanzia Hadhrat Adam mpaka sasa waliotangulia ni kama mababu wa waliokuja baadaye lakini dhambi ya mtu mmoja haiwezi kubebeshwa mtu mwingine. Basi, Mwenyezi Mungu kusema ndani ya Kurani. Tukufu kuwa ninyi mmemwasi Musa[as] na mkasema kuwa sisi hatutamwamini Mungu mpaka tumuone, nanyi mkateremshiwa radi kwa sababu ya dhambi hii, maneno haya yote kidhahiri yanawezaje kuwa na maana nyingine isipokuwa isemwe kuwa kwa kweli Wayahudi wote waliokuwepo katika zama za Mtume[saw] walikuwepo pia katika zama za Hadhrat Musa[as] na hao waliteremshiwa *Manna* na *Salwa* na hao ndio waliangukiwa na radi, na kwa ajili ya hao Firauni alihilikishwa, na kisha hao hao Wayahudi wakazaliwa upya *ki-Tanasukh* katika zama za

Mtume Muhammad[saw], na kwa njia hii ikawa sawa wao kuambiwa hayo. Lakini swali lazuka kuwa kwa nini isitolewe tafsiri kama hiyo iliyonyooka? Je, hii iko mbali na uwezo wa Allah? Na kwa nini inakubaliwa tafsiri yenye maelezo yasiyotakikana? Je Mwenyezi Mungu hana uwezo wa kuwahuisha Wayahudi wa zama za Hadhrat Musa au kuleta roho zao *ki-Tanasukh* kama vile — sawa na kauli ya wapinzani wetu — Yeye Atakavyomleta duniani Hadhrat Isa kwa kiwiliwili chake hasa baada ya mamia ya miaka. Kama ambavyo umekubaliwa ujaji wa roho ya Hadhrat Isa mara ya pili duniani sawa na kauli zisizo za msingi, kwa nini na kwa sababu gani tusikubali kurudi tena duniani kwa roho za Wayahudi wote kwa njia ya *tanasukh* katika zama za Mtume[saw], ambao Kurani Tukufu inatoa ushahidi waziwazi juu ya uwepo wao? Tazama Mwenyezi Mungu anasema kwa uwazi:

وَ اِذْ قُلْتُمْ يٰمُوْسٰى لَنْ نُّؤْمِنَ لَكَ حَتّٰى نَرَى اللّٰهَ جَهْرَةً

فَاَخَذَتْکُمُ الصّٰعِقَةُ وَ اَنْتُمْ تَنْظُرُوْنَ[47]

Yaani, kumbukeni wakati ambapo sio wengine bali ni ninyi ndio mliosema kuwa hatutamini kwa kusema kwako mpaka tumuone Mwenyezi Mungu kidhahiri, ndipo radi ikawashukia ilhali mliona. Katika aya hii kuna jambo jingine jepesi ya kwamba kwa vile Mwenyezi Mungu hakuwachukulia Wayahudi wa sasa ndani ya madhumuni ya aya badala ya Wayahudi waliopita, bali kwa hakika aliwataja kuwa ni wale wale waliopita zamani, kwa hiyo Kurani Tukufu ikawapa Wayahudi wa zama za Mtume[saw] majina yale yale yaliyokuwa ya Banii Israeli waliopita. Kwani, kwa vile hawa wamechukuliwa kuwa ndio wale wale, basi ikalazimika wawe na majina yale yale, kwa sababu majina ya vitu halisi ni kama sifa zisizoweza kutengana. Sifa za lazima haziwezi kujitenga na vitu halisi. Sasa fikirieni kwa makini kuwa Mwenyezi Mungu alipowaambia

[47] Sura Al-Baqara, 2:56. Mwenezi.

Wayahudi wa zama za Mtume[saw] waziwazi kuwa ninyi ndinyi mliofanya maovu katika zama za Hadhrat Musa, basi kuyaeleza vingine matini yaliyo wazi kabisa na kumteremsha Nabii Isa[as] ardhini ambaye kwa mujibu wa Kurani Tukufu amekwisha kufa ni kinyume cha uadilifu namna gani! Enyi wapenzi, kama hii ndiyo suna na desturi ya Mwenyezi Mungu ya kwamba Yeye Anawaleta tena duniani watu wa zamani, basi haijuzu kuyahepa maandiko ya Kurani yanayokariri kutoa ushahidi wa uhai wa watu waliopita ikizungumza nao. Hapo kama moyo ukishtuka kuwa tafsiri hii ingawa siyo mbali na uwezo wa Mungu, lakini ni kinyume cha akili, ndiyo maana inabidi kuelekea kwenye maelezo na kutoa tafsiri isiyo mbali na akili, basi na bishara ya ujaji wa Hadhrat Isa nayo ifasiriwe hivyo hivyo. Kwani kama kuhuika kwa Wayahudi wa zamani katika zama za Mtume[saw] wetu au roho zao kurejea tena kwa njia ya *Tanaasukh* ni kinyume

cha akili, kwa nini, basi linabuniwa wazo la kurejea Hadhrat Masihi duniani mara ya pili ambaye juu ya kifo chake aya

فَلَمَّا تَوَفَّيْتَنِيْ كُنْتَ اَنْتَ الرَّقِيْبَ عَلَيْهِمْ [48]

inatoa ushahidi kwa kupaza sauti? Je kurejea roho za Wayahudi duniani ni kinyume cha kudra ya Mwenyezi Mungu na ni dhidi ya akili, lakini kurejea Hadhrat Isa pamoja na jasadi yake ni sawa na akili sana? Kama tafsiri dhahiri ya maandiko bayana kabisa ya Kurani kwa sababu ya kuwa kinyume cha akili inaachwa na kutolewa maelezo yake, kwa nini maandiko ya Hadithi yasijuzu kuachwa maana yake ya kidhahiri? Je, Hadithi inayo shani kubwa kuliko Kurani Tukufu hata kwamba maneno ya Hadithi lazima yakubaliwa hata yakiwa kinyume kabisa na akili, lakini maneno ya Kurani yatafutiwe maelezo ya kuingia akilini?? Sasa, tukirejea kwa habari yenyewe

[48] Tafsiri: Na Uliponifisha Ukawa Mchungaji juu yao. Sura Al-Maaida, 5:118. Mwenezi.

tuliyokuwa kukizungumzia twaandika kuwa baadhi ya watu wanasema kuwa haiwahusu waaminio wote aya hii:

وَعَدَ اللّٰهُ الَّذِيْنَ اٰمَنُوْا مِنْكُمْ وَعَمِلُوا الصّٰلِحٰتِ لَيَسْتَخْلِفَنَّهُمْ فِي الْاَرْضِ

كَمَا اسْتَخْلَفَ الَّذِيْنَ مِنْ قَبْلِهِمْ [49]

kwani neno منكم — miongoni mwenu — muradi wake ni Masahaba tu, na Khilafat Rashida iliishia kwenye zama zao, na kutakuwa hamna Ukhalifa katika Islam hadi kiyama. Ndiyo kusema kwamba Ukhalifa huo ulikuwa kwa muda mfupi wa miaka thelathini tu, kisha kwa kudumu Islam ikatumbukia ndani ya dimbwi la mkosi wa kudumu. Lakini mimi nauliza, je mtu mwema anaweza kuwa na rai hii kwamba awe na itikadi kumhusu Hadhrat Musa kuwa kwa baraka ya sheria yake ukhalifa uliendelea kwa miaka 1400 barabara, lakini Nabii yule aliye mbora kuliko mitume wote na mbora wa Manabii wote ambaye sheria zake zinatanda mpaka kiyama,

[49] Sura An-Nuur, 24:56. Mwenezi.

baraka zake zikashia kwenye zama zake mwenyewe tu, na Mwenyezi Mungu Hakupenda kuwa mifano ya baraka zake idhihirike kwa muda mrefu sana kwa njia ya makhalifa wake wa kiroho. Kwa kusikia maneno kama hayo mwili wetu unatetemeka. Lakini ni masikitiko kwamba watu wale pia wanaitwa Waislamu ambao kwa ujanja na ujasiri wanatamka maneno kama hayo yasiyo na adabu, kana kwamba baraka za Islam haziendelei, bali zilikoma tangu muda mrefu.

Isitoshe, kutoa dalili hii kutokana na neno "*Minkum*" kwamba kwa vile wanaoambiwa ni Masahaba, kwa hiyo ukhalifa unaishia mpaka kwa masahaba tu, ni akili ya ajabu. Kama maelezo ya Kurani Tukufu yatolewe hivyo, basi hiyo ni hatua ya kuwazidi hata Wayahudi. Sasa iwe wazi kuwa neno "*Minkum*" limetumika ndani ya Kurani Tukufu mara 82. Kwa kuacha sehemu mbili tatu ambapo pana dalili maalum, mahali pengine pote muradi wa "*Minkum*"

ni Waislamu wote watakaoendelea kuzaliwa mpaka siku ya kiyama. Sasa kwa mfano twaziandika aya ambamo neno "*Minkum*" limetumika:

1. فَمَنْ كَانَ مِنْكُمْ مَّرِيْضًا اَوْ عَلٰى سَفَرٍ فَعِدَّةٌ مِّنْ اَيَّامٍ اُخَرَ[50] Yaani, yeyote miongoni mwenu atakayekuwa mgonjwa au safarini, basi atimize hesabu katika siku zingine. Sasa, fikirieni, je amri hii ilihusikana na Masahaba pekee au Waislamu wote wamejumuishwa humu watakaoendelea kuzaliwa mpka kiama? Kadhalika zingatieni aya zifuatazo:

2. ذٰلِكَ يُوْعَظُ بِهٖ مَنْ كَانَ مِنْكُمْ يُؤْمِنُ بِاللّٰهِ وَالْيَوْمِ الْاٰخِرِ[51] Yaani, wale tu hupewa mawaidha haya miongoni mwenu wanaomwamini Allah na siku ya mwisho.

3. وَالَّذِيْنَ يُتَوَفَّوْنَ مِنْكُمْ وَيَذَرُوْنَ اَزْوَاجًا[52] Yaani, wale wanaofishwa miongoni mwenu na kuacha wake zao nyuma.

4. وَلْتَكُنْ مِّنْكُمْ اُمَّةٌ يَّدْعُوْنَ اِلَى الْخَيْرِ وَيَاْمُرُوْنَ بِالْمَعْرُوْفِ وَيَنْهَوْنَ عَنِ الْمُنْكَرِ[53]

---

[50] Sura Al-Baqara, 2:185. Mwenezi.
[51] Sura Al-Baqara, 2:233. Mwenezi.
[52] Sura Al-Baqara, 2:235. Mwenezi.
[53] Sura Aali Imraan, 3:105. Mwenezi.

Yaani, na liwepo miongoni mwenu kundi linaloita kwenye heri na kuamuru kutenda mema na kukataza maovu.

5. أَنِّي لَا أُضِيعُ عَمَلَ عَامِلٍ مِّنكُم مِّن ذَكَرٍ أَوْ أُنثَىٰ[54] Hakika sitapoteza juhudi ya mfanya juhudi miongoni mwenu, akiwa mwanamume au mwanamke.

6. لَا تَأْكُلُوا أَمْوَالَكُم بَيْنَكُم بِالْبَاطِلِ إِلَّا أَن تَكُونَ تِجَارَةً عَن تَرَاضٍ مِّنكُمْ[55] Yaani, msiliane mali zenu kwa batili isipokuwa iwe biashara kwa kuridhiana baina yenu.

7. وَإِن كُنتُم مَّرْضَىٰ أَوْ عَلَىٰ سَفَرٍ أَوْ جَاءَ أَحَدٌ مِّنكُم مِّنَ الْغَائِطِ أَوْ لَامَسْتُمُ النِّسَاءَ فَلَمْ تَجِدُوا مَاءً فَتَيَمَّمُوا صَعِيدًا طَيِّبًا[56] Yaani, mkiwa wagonjwa au safarini au mmoja wenu ametoka chooni au mmeingiliana na wanawake na hamkupata maji, basi tayamamuni katika udongo ulio safi.

8. أَطِيعُوا اللَّهَ وَأَطِيعُوا الرَّسُولَ وَأُولِي الْأَمْرِ مِنكُمْ[57] Yaani, Mtiini Mwenyezi Mungu na mtiini Mtume na wenye mamlaka kati yenu.

9. مَنْ عَمِلَ مِنكُمْ سُوءًا بِجَهَالَةٍ ثُمَّ تَابَ مِن بَعْدِهِ وَأَصْلَحَ فَأَنَّهُ غَفُورٌ رَّحِيمٌ[58]

---

[54] Sura Aali Imraan, 3:196. Mwenezi.
[55] Sura An-Nisaa, 4:30. Mwenezi.
[56] Sura Al-Maaida, 5:7. Mwenezi.
[57] Sura An-Nisaa, 4:60. Mwenezi.
[58] Sura Al-An'aam. 6:55. Mwenezi.

Yaani, yeyote miongoni mwenu anayefanya uovu kwa ujinga, kisha akatubu baada yake na akafanya wema, basi Yeye ndiye Msemehevu, Mrehemevu.

10. فَمَا جَزَآءُ مَنْ يَّفْعَلُ ذٰلِكَ مِنْكُمْ اِلَّا خِزْيٌ فِى الْحَيٰوةِ الدُّنْيَا وَ يَوْمَ الْقِيٰمَةِ يُرَدُّوْنَ اِلٰٓى اَشَدِّ
الْعَذَابِ[59] Yaani, yeyote miongoni mwenu atakayefanya hayo atapata fedheha tu katika maisha ya dunia, naye atapata adhabu kali siku ya Kiyama.

11. وَاِنْ مِّنْكُمْ اِلَّا وَارِدُهَا[60] Yaani, wala hakuna yeyote miongoni mwenu ila ni mwenye kuifikia Jahanamu.

12. وَ لَقَدْ عَلِمْنَا الْمُسْتَقْدِمِيْنَ مِنْكُمْ وَ لَقَدْ عَلِمْنَا الْمُسْتَاْخِرِيْنَ[61]

Yaani, Tunawajua watanguliao miongoni mwenu na wenye kubaki nyuma.

Tazameni sasa sehemu hizo zote kwamba humo neno "*Minkum*" — miongoni mwenu — limetumika kwa ajili ya Waislamu wote, waliokuwepo wakati huo na watakaoendelea kuja mpaka siku ya Kiyama. Kadhalika katika sehemu zingine zote — isipokuwa

---

[59] Sura Al-Baqara. 2:86. Mwenezi.
[60] Sura Maryam. 19:72. Mwenezi.
[61] Sura Al-Hijr. 15:25. Mwenezi.

sehemu mbili, tatu — hilo limetumika kwa Waislamu wote. Kidhahiri masahaba wanatolewa amri zote, lakini kuzihusisha hizo kwa masahaba tu haijuzu isipokuwa kama ipo dalili hapo, la sivyo kila mwovu atapata kisingizio cha kusema kuwa maagizo yote kuhusu saumu na sala, hija, ucha Mungu, utakaso na kujiepusha na maasi yaliwahusu Masahaba tu, kwa hiyo, hatulazimiki kuzifuata amri za kusali na kufunga saumu na kadhalika. Na ni dhahiri kuwa mcha Mungu yeyote hawezi kuyatamka maneno haya isipokuwa aliyeachana na dini.

Mtu akifikiria moyoni kuwa aya وَعَدَ اللَّهُ الَّذِينَ آمَنُوا[62] inamaanisha watu wote, yaani shabaha yenyewe ni kujumuisha waaminio wote sio waaminio mahususi, kwa nini, basi, neno "*Minkum*" limeongezwa hapa, kulikuwa na haja gani, ingesemwa tu:

وَعَدَ اللَّهُ الَّذِينَ آمَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ لَيَسْتَخْلِفَنَّهُمْ فِي الْأَرْضِ
كَمَا اسْتَخْلَفَ الَّذِينَ مِن قَبْلِهِمْ

---

[62] Mwenyezi Mungu Amewaahidi walioamini. Sura An-Nuur, 24:56. Mwenezi.

pasipo neno "*Minkum*" , basi jibu lake ni kuwa ahadi hii ilikuwa kulingana na waaminio na watu wema waliopita kabla ya umati huu. Tuseme maelezo yake ni kwamba kabla yenu Mwenyezi Mungu Aliwafanya makhalifa wale waliokuwa waaminio na wema waliojumuisha matendo mema pamoja na imani, na Mwenyezi Mungu anaahidi, Enye Waislamu, kuwa miongoni mwenu pia Atawafanya makhalifa watakaokuwa na sifa hizo na kujumuisha matendo mema pamoja na imani. Kwa hiyo, neno "*Minkum*" siyo la ziada, bali shabaha yake ni kuashiria kwenye waaminio na watu wema wa dini ya Kiislamu, kwani kwa kuwa maneno 'wema' na 'waaminio' yaliyotumika katika aya hiyo yalihusikana na waaminio na watu wema wa nyimati za zamani na umati huu kwa usawa, hivyo kama lisingetumika neno "*Minkum*" , hapo ibara ingekuwa hafifu, si wazi wala si yenye ufasaha. Isitoshe, kwa neno *minkum* inakusudiwa vilevile kusisitiza kwamba hapo zamani pia waliofanywa kuwa makhalifa walikuwa

ni waaminio na watu wema, na miongoni mwenu pia waaminio na wema tu ndio watakaofanywa kuwa makhalifa. Basi, kama kuna macho ya kuonea, itaonekana neno "*Minkum*" halikuzidi asilani wala maneno haya kurudiwa-rudiwa. Kwa kuwa imani na matendo mema hayakuanzia kwa umati huu, hapo kabla pia walikuwepo waaminio na watu wema, basi ingewezaje kupambanuka maana hii bila ya neno "*Minkum*" . Kama ingesemwa tu kuwa "Mwenyezi Mungu Ameahidi wale walioamini na kutenda mema", isingeweza kufahamika kuwa ni waaminio gani waliotajwa hapa; je ni waaminio wa umati huu au wa nyimati zilizopita? Na kama lingekuwa neno "*Minkum*" pekee, na isingesemwa 'walioamini na kutenda mema', ingefahamika kuwa hata mafasiki na waovu nao wanaweza kuwa makhalifa wa Mwenyezi Mungu, ilhali ufalme na serikali ya mafasiki huwa kama majaribio, siyo maana yake kwamba hao ni wateule. Bali makhalifa wa kweli wa Mwenyezi Mungu, wawe makhalifa wa kiroho au wa kidhahiri, hao ndio wacha

Mungu na waaminio na watu wema.

Na wazo hili kuwa katika aya hizo tafsiri ya kawaida ya aya ya mwisho

وَمَنْ كَفَرَ بَعْدَ ذٰلِكَ فَاُولٰٓئِكَ هُمُ الْفٰسِقُوْنَ[63]

inakuwa haina maana yoyote, ni wazo la kipuzi na ni kichekesho, kwani tafsiri safi na iliyo wazi ya aya hii ni kwamba Mwenyezi Mungu baada ya kutoa habari njema ya kupatikana makhalifa, anawaonya waasi na wasiotii kuwa baada ya Ukhalifa kupatikana, makhalifa watakapokuja katika nyakati mbalimbali, basi yeyote anayewaasi na kukataa kufanya baiat, huyo ndiye fasiki. Sasa liko wapi kosa la tafsiri? Na ibainike kuwa aya hii tukufu inaafikiana na Hadithi ya Mtume[saw] alimosema

من لم يعرف امام زمانه فقد مات ميتة الجاهلية

'Yule asiyemtambua Imam wa zama zake, yeye amekufa kifo cha kijahili'. Yaani, Maimamu

---

[63] Atakayekufuru baada ya hayo, basi hao ndio wavunjao amri. An-Nuur, 24:56. Mwenezi.

watadhihiri katika kila zama, basi wasiowatambua, kifo chao kitafanana na kifo cha makafiri. Na ni bure mpinzani kutaja aya hii:

قَالَ اللّٰهُ اِنِّيْ مُنَزِّلُهَا عَلَيْكُمْ فَمَنْ يَّكْفُرْ بَعْدُ مِنْكُمْ فَاِنِّيْٓ اُعَذِّبُهٗ
عَذَابًا لَّآ اُعَذِّبُهٗٓ اَحَدًا مِّنَ الْعٰلَمِيْنَ[64]

na kusema kwamba neno "*Minkum*" — miongoni mwenu — limetumika hapa kwa watu maalum waliokuwepo wakati huo. Kwani, huko nyuma tumekwishaandika kwamba ni njia ya kawaida ya Kurani Tukufu, ambayo Kurani nzima imejaa kwayo, kwamba mazungumzo yanakuwa kwa watu kwa jumla na wanaamrishwa wafuasi wote wa umati huu na sio masahaba pekee, isipokuwa pale tu palipo dalili maalumu ya kuhusu watu maalum. Basi, katika aya hiyo hapo juu kundi moja la wanafunzi wa Yesu likamwomba kuteremshiwa chakula, basi kundi

[64] Mwenyezi Mungu Akasema: Bila shaka Mimi Nitakiteremsha juu yenu, lakini miongoni mwenu atakayekataa baada ya haya, basi Mimi Nitawaadhibu adhabu ambayo Sijamwadhibu yeyote katika walimwengu. Sura Al-Maaida, 5:116. Mwenezi.

hilo ndilo likajibiwa. Kwa hiyo dalili hii inatosha kwamba ombi likafanywa na kundi hili na likajibiwa kundi hilo hilo. Na kusema kuwa mifano mingi ya aina hii inapatikana ndani ya Kurani Tukufu ni uwongo mtupu na udanganyifu. Ndani ya Kurani neno "*Minkum*" limetumika mara 82, na kwa njia nyingine watu wameagizwa mara 600 takriban, lakini mara zote watu wote wametolewa maagizo. Kama maagizo yote yangewahusu masahaba peke yao tu, bila shaka baada ya kufariki kwa masahaba Kurani Tukufu ingebatilika. Na inayobishaniwa iliyo juu ya ukhalifa inafanana na hii aya:

لَهُمُ الْبُشْرٰى فِى الْحَيٰوةِ الدُّنْيَا[65]

Je, habari hii njema iliwahusu masahaba pekee au watu wengine fulani nao walihusikana nayo? Na kusema kwa mpinzani ya kuwa yule anayechukulia maana ya 'watu wote kwa jumla' akiacha maana hasa ya 'wale

---

[65] Tafsiri: Wao wanazo habari njema katika dunia. Sura Yunus, 10:65. Mwenezi.

wanaoambiwa' agizo fulani, ni juu yake kuthibitisha kwa nini ameachana na maana ya asili, hiyo yahakikisha kwamba licha ya Kurani Tukufu, mpinzani huyo hana habari kabisa ya njia ya kueleza ya vitabu vyote vya dini pia. Shida yenyewe ni kuwa watu wengi wenye papara huwa tayari kupinga kabla ya kufikiria kikamilifu kwa makini. Kama mpinzani alikuwa na shauku ya kuchunguza kwa nia safi, yeye alipaswa kukusanya sehemu zote zile ambapo kidhahiri masahaba wameambiwa mambo fulani kisha kuona kuwa nahau ya Kurani Tukufu mara nyingi ikoje ambapo hamna dalili ya kuchukulia maana nyingine. Kwani, ni dhahiri kabisa kwamba maana ya asili itakuwa ile tu itakayothibitika mara nyingi katika matumizi ya lugha, na kwenda kombo haitajuzu. Sasa ibainike kuwa njia hasa ya Kurani Tukufu inapoongea na waliopo ni kuwa inawajumuisha watu wote kwa jumla. Kwa hiyo amri mia sita za Kurani zinafahamika kuwahusu watu wote, sio kuwahusu masahaba tu pekee. Sasa yule aendaye upande kinyume na usemi

wa kawaida na kusema masahaba tu ndio wametolewa maagizo hayo na watu wengine hawahusikani nayo, ni juu yake kuthibitisha kauli yake kwa dalili zilizo imara. Kwa mfano, Mwenyezi Mungu ndani ya Kurani Tukufu kidhahiri Anawaambia, masahaba kuwa Mwabuduni Mungu pekee na ombeni msaada kwa subira na sala na kuleni katika yaliyo safi, msilete ufisadi, toeni zaka, simamisheni sala, na mpafanye mahali aliposimama Ibrahimu pawe pa kusalia, shindaneni katika mema, Nikumbukeni Nitawakumbuka, Nishukuruni, Niombeeni, msiseme ni wafu waliouawa katika njia ya Mungu, anayewasalimuni msiseme yu kafiri hana imani, kuleni vitu safi katika mazao ya ardhi, msimfuate shetani, mmefaradhishwa kufunga saumu, lakini aliye mgonjwa au yuko safarini afunge baadaye siku hizo, msiliane mali zenu kwa batili, shikeni ucha Mungu ili mwongoke, piganeni katika njia ya Mungu na wale wanaopigana nanyi, lakini msipite kiasi, msiruke mipaka kwani Mungu Hawapendi warakao mipaka, toeni katika njia ya Mungu

wala msijitupe kwa mikono yenu katika maangamizo, wafanyieni watu hisani kwani Mungu ndiye rafiki wa wafanyao hisani, timizeni hija na umra kwa ajili ya Mungu, chukueni masurufu kwani faida ya masurufu ni kwamba hamtawaomba wengine, yaani kuomba ni dhila, yafaa kujiepusha nayo, ingieni katika suluhu na Islam, msiwaoe wanawake washirikina mpaka waamini, na Enyi wanawake, msiolewe na washirikina mpaka waamini, tangulizieni chochote nafsi zenu, msimfanye Mungu shabaha ya viapo vyenu, msiwazuie wanawake kwa dhara, wanaokufa miongoni mwenu na kuacha nyume wake zao, hao wajizuie wasiolewe hadi miezi minne na siku kumi, mkiwapa wanawake talaka, waacheni kwa hisani, kama mkiwa na hofu, basi salini mkitembea au mmepanda, kama mkitoa sadaka kwa dhahiri ni vizuri, kwani wengine watafuata matendo yenu mema, na kama mkitoa kwa siri na kuwapa wanaohitaji, basi huo ni bora kwa nafsi zenu, mnapokopeshana deni, basi liandikeni, Mwogopeni Mungu mrudishapo deni, msipunguze

chochote ndani yake, na shahidisheni mnapouziana, na kama mkiwa safarini na hamkupata mwandishi, basi rehani ikabidhiwe mdai, na shikeni kamba ya Mungu nyote pamoja wala msifarakane, na wawepo miongoni mwenu waamrishao kutenda mema na kukataza maovu, na ukimbilieni msamaha wa Mungu, na kama mke wa mmoja wenu anakufa, mumewe atapata nusu ya mali aliyoacha mkewe sharti marehemu mke hana watoto na kama anao watoto, basi mume atapata robo ya aliyeacha mke, baada ya kutoa aliyousia.

Tumeandika amri hizo chache kama mfano tu. Sasa mwenye akili kidogo tu pia anaweza kufikiria kuwa kidhahiri masahaba wanaamrishwa hizo, lakini Waislamu wote kwa hakika wanatolewa maagizo hayo, sio masahaba tu. Ilmuradi, njia asilia na ya kweli ya Kurani, iliyojaa Kurani nzima ndiyo kwamba inawatolea maagizo Waislamu wote watakaoendelea kuzaliwa hadi kiyama, ingawaje kidhahiri yaonekana masahaba wanaambiwa hayo. Basi yule adaiye kuwa

ahadi au onyo fulani lahusikana na masahaba pekee, yeye mtu huyo anaachana na nahau ya Kurani. Na maadamu haleti uthibitisho barabara wa madai yake, yu *Mulhid*[66]. Je, Kurani ilishuka kwa ajili ya masahaba tu. Kama ahadi na maonyo yanaishia kwa masahaba pekee, basi waliozaliwa baadaye hawahusikani na Kurani.

نعوذ بالله من هذه الخرافات[67]

Na kusema kwamba sawa na Hadithi Ukhalifa utakuwa mpaka miaka thelathini, ni fahamu ya ajabu. Kurani Tukufu inasema:

ثُلَّةٌ مِّنَ الْاَوَّلِيْنَ وَ ثُلَّةٌ مِّنَ الْاٰخِرِيْنَ[68]

Basi dhidi yake kuleta Hadithi na kuifasiri kinyume cha Kurani, ni akili ya aina gani! Kama Hadithi yategemewa, basi kwanza zitekelezwe zile Hadithi

---

66 *Mulhid*: Tafsiri yake ni 'aendaye kombo'. Akanaye Mungu na asiye na dini anaitwa *Mulhid*. Mwenezi.

67 Tafsiri: Twajikinga kwa Allah katika maneno hayo ya uzushi. Mwenezi.

68 Tafsiri: Jamii kubwa miongoni mwa wa kwanza, na jamii kubwa miongoni mwa wa mwisho. Sura Al-Waaqi'a, 56:40-41. Mwenezi.

zilizopita madaraja kadha katika usahihi na yakini kuliko Hadithi hiyo. Mathalan, zile Hadithi za Sahihi Bukhari zinazotoa habari ya baadhi ya makhalifa katika zama za mwisho, hususan yule Khalifa ambaye kumhusu yeye imeandikwa ndani ya Bukhari kuwa sauti itatoka mbinguni: 'Huyu ndiye Khalifa wa Allah, Al-Mahdi.' Sasa zingatieni Hadithi hii ni ya daraja gani iliyomo ndani ya kitabu kilicho sahihi sana baada ya Kitabu cha Mungu. Lakini ile Hadithi aliyotaja mpinzani imechambuliwa na Maulamaa kuhusu usahihi wake. Je, mpinzani hajazingatia kuwa habari za kudhihiri baadhi ya makhalifa katika zama za mwisho kwamba atakuja Harithi, atakuja Mahdi, Khalifa wa Kimbingu atakuja, habari hizi zimo ndani ya Hadithi au kitabu fulani kingine? Yathibitika kutokana na Hadithi kwamba zama ni za namna tatu. Kwanza zama za Khilafat Rashida, kisha zama za upotevu ambamo watakuwepo wafalme wadhalimu, na baadaye zama za mwiho zitakazokuwa juu ya njia ya zama za Unabii, hata kwamba akasema

Mtume[saw] kuwa zama za awali na za mwisho za umati wangu zinafanana sana, haijulikani kuna baraka nyingi katika zama za awali au katika zama za mwiho.

Ibainike pia hapa kuwa Mwenyezi Mungu Anasema ndani ya Kurani Tukufu

إِنَّا نَحْنُ نَزَّلْنَا الذِّكْرَ وَإِنَّا لَهُ لَحَافِظُونَ[69]

yaani, Sisi Tumeteremsha Kitabu hiki, na Sisi ndio Tutakaokihifadhi. Ndani yake imefafanuliwa kuwa Neno hili litadumu kubaki hai, na daima dawamu wataendelea kuzaliwa watakaoyabakiza mafundisho yake mabichi na watakaowanufaisha watu kwayo. Kama lizuke swali kuwa faida ya Kurani ni nini ambayo ndiyo sababu ya kuhifadhiwa kwake kwa kweli, basi hiyo ni wazi kutoka katika aya hii

هُوَ الَّذِي بَعَثَ فِي الْأُمِّيِّينَ رَسُولًا مِّنْهُمْ يَتْلُو عَلَيْهِمْ آيَاتِهِ
وَيُزَكِّيهِمْ وَيُعَلِّمُهُمُ الْكِتَابَ وَالْحِكْمَةَ[70]

Muhtasari wa aya hii ni kuwa kuna faida mbili za Kurani

---

[69] Sura Al-Hijr, 15:10. Mwenezi.

[70] Sura Al-Jumu'ah, 62:3. Mwenezi.

ambazo kwa kuwafikishia watu alikuwepo Mtume[saw]. Ya kwanza ni hekima za Furkan, yaani maarifa na mambo ya ndani sana yenye kina ya Kurani, na pili ni athari ya Kurani inayosababisha kutakasa nafsi. Na kuihifadhi Kurani sio tu kulinda msahafu ulioandikwa, kwani mambo kama hayo hata Wayahudi na Wakristo pia walifanya mwanzoni mpaka walipiga hesabu ya hata nukta za Torati, bali hapa muradi wake ni kuhifadhi manufaa na athari za Kurani pamoja na ulinzi wa kidhahiri. Na hiyo yaweza tu sawa na suna ya Mungu hapo tu ambapo manaibu wa Mtume waje mara kwa mara ambao wanazo neema zote za utume kwa baraka za Mtume[saw] na ambao wamejaliwa baraka zote zile wanazojaliwa manabii kama ilivyoashiriwa habari hii kubwa ndani ya aya hizo. Na aya yenyewe ni hii:

وَعَدَ اللّٰهُ الَّذِيْنَ اٰمَنُوْا مِنْكُمْ وَعَمِلُوا الصّٰلِحٰتِ لَيَسْتَخْلِفَنَّهُمْ فِي الْاَرْضِ
كَمَا اسْتَخْلَفَ الَّذِيْنَ مِنْ قَبْلِهِمْ ۠ وَلَيُمَكِّنَنَّ لَهُمْ دِيْنَهُمُ الَّذِي ارْتَضٰى
لَهُمْ وَلَيُبَدِّلَنَّهُمْ مِّنْ بَعْدِ خَوْفِهِمْ اَمْنًا ؕ يَعْبُدُوْنَنِيْ لَا يُشْرِكُوْنَ بِيْ شَيْـًٔا ؕ

وَمَنْ كَفَرَ بَعْدَ ذٰلِكَ فَاُولٰٓئِكَ هُمُ الْفٰسِقُوْنَ[71]

Basi, aya hiyo kwa hakika ni maelezo ya aya hii nyingine:

اِنَّا نَحْنُ نَزَّلْنَا الذِّكْرَ وَ اِنَّا لَهٗ لَحٰفِظُوْنَ[72]

na inajibu swali hili kuwa Kurani itahifadhiwa namna gani na kwa njia ipi. Basi Mwenyezi Mungu Anasema kuwa Mimi Nitaendelea kuwatuma Makhalifa wa Mtume[saw] mara kwa mara. Neno Khalifa limechaguliwa kwa kuashiria kwamba hao watakuwa warithi wa kiroho wa Mtume[saw] na watapata sehemu za baraka zake kama ilivyofanyika katika zama zilizopita. Kwa mikono yao dini itaimarika, na baada ya hofu amani itapatikana. Yaani, hao watakuja katika nyakati ambapo Islam itakuwa na mafarakano, kisha baada ya ujaji wao watakaoasi miongoni mwao, hao ndio waovu na mafasiki. Hili ni jawabu la baadhi ya majahili

71 Sura An-Nuur, 24:56. Mwenezi.
72 Sura Al-Hijr, 15:10. Mwenezi.

wasemao je kuwaamini mawalii ni faradhi? Ni faradhi pasipo shaka, na wawapingao ndio mafasiki wakifa katika hali ya upinzani.

Sehemu hii mpinzani ameandika pia kuwa Mwenyezi Mungu Anasema:

اَلْيَوْمَ اَكْمَلْتُ لَكُمْ دِيْنَكُمْ وَ اَتْمَمْتُ عَلَيْكُمْ نِعْمَتِيْ[73]

na kisha akaleta upinzani kwamba maadamu dini imekamilika na neema imetimilika, basi hakuna tena haja ya Mujaddidi wala Nabii mwingine. Lakini, ni masikitiko kuwa mpinzani kwa kufikiria hivyo ameipinga Kurani Tukufu. Kwani, Kurani Tukufu imeahidi kupatikana kwa makhalifa katika umati huu kama ilivyopita hapo nyuma, na ikasema kuwa katika zama zao dini itaimarika, na ghasia na mashaka yatatoweka, na amani itakuwepo baada ya hofu. Sasa kama baada ya dini kakamilika tendo lolote sio sahihi, hapo ukhalifa wa miaka thelathini anaosema mpinzani pia utabatilika. Kwani, kwa

[73] Tafsiri: Leo Nimewakamilishieni dini yenu, na kuwatimizieni neema yangu. Sura Al-Maaida, 5:4. Mwenezi.

kuwa dini imekamilika, kuna haja gani ya mwingine yeyote awaye. Lakini, ni masikitiko kwamba mpinzani asiyejua ametaja aya pasipo haki:

اَلْيَوْمَ اَكْمَلْتُ لَكُمْ دِيْنَكُمْ

Lini tumesema kuwa Mujaddidina na Muhaddathina baada ya kuja wanapunguza au kuongeza chochote ndani ya dini. Bali, kauli yetu ni kuwa baada ya kupita muda fulani mafundisho matakatifu yanapopatwa na vumbi la fikara mbovu, na uso halisi wa haki unapofichika, hapo Mujaddidina na Muhaddathina na Makhalifa wa kiroho huja kuuonyesha uso ule mzuri. Mpinzani maskini amesikia kutoka wapi na kwa nani kwamba Mujaddidina na Makhalifa wakija duniani wanarekebisha dini na wanaitangua kidogo. Hapana, hawaji kuitangua, bali waja kudhihirisha mng'ao wa dini na mwanga wake. Na fikara hii ya mpinzani kwamba kuna haja gani ya ujaji wao, sababu yake ni kuwa haijali dini yake, wala hajazingatia Islam ni kitu gani, na maendeleo

ya kweli yanawezaje kupatikana na kwa njia zipi, na katika hali gani mtu anaitwa kuwa ni Mwislamu wa kweli. Ndiyo sababu mpinzani anatosheka kwa kufikiria kuwa Kuran ipo na wanazuoni wapo, na nyoyo za watu wengi zaelekea kwenye Islam, basi kuna haja gani ya Mujaddidi yeyote? Lakni nasikitika kuwa mpinzani hafahamu kwamba Mujaddidina na Makhalifa wa kiroho wanahitajika kwa umati huu jinsi manabii walivyoendelea kuhitajika tangu zamani. Hakuna awezaye kukataa kuwa Hadhrat Musa[as] alikuwa mtume na Torati yake ilikuwa imekamilika kuwafundisha Wana wa Israeli, na kama ilivyo aya: اَلْيَوْمَ اَكْمَلْتُ لَكُمْ دِيْنَكُمْ ndani ya Kurani Tukufu ndivyo zilivyo aya katika Torati zimaanishazo kuwa Wana wa Israeli wamepewa Kitabu kamili chenye jalali kinachoitwa Torati. Na Kurani Tukufu pia imeeleza sifa hii ya Torati, hata hivyo baada ya Torati mamia ya manabii walitokea miongoni mwa wana wa Israeli wasiokuwa na

kitabu kipya, bali shabaha ya manabii hao ilikuwa kuwaleta wale, waliokwenda mbali na mafundisho ya Torati, katika hizo kwenye utashi wa asili wa Torati, na kuwapatia imani iliyo hai wale walioingiwa na shaka, ukanaji Mungu na utovu wa uaminifu kidogo. Mwenyezi Mungu Mwenyewe Anasema ndani ya Kurani Tukufu:

وَلَقَدْ آتَيْنَا مُوسَى الْكِتَابَ وَقَفَّيْنَا مِنْ بَعْدِهِ بِالرُّسُلِ[74]

Yaani, Tulimpa Musa Torati, kisha baada ya Kitabu hiki Tuliwatuma mitume kadhaa ili kuyasaidia mafundisho ya Torati na kuyasadikisha. Kadhalika Anasmea katika sehmu nyingine

ثُمَّ أَرْسَلْنَا رُسُلَنَا تَتْرَا[75]

Yaani, kisha baadaye Tuliwatuma mitume mfulililizo. Basi ni dhahiri kutokana na aya hizo zote kuwa suna ya Mungu ni hii kwamba baada ya kuleta Kitabu Chake, Huwa Anatuma lazima manabii

[74] Sura Al-Baqara, 2:88. Mwenezi.
[75] Sura Al-Mu'minuun, 23:45. Mwenezi.

ili kukisaidia na kukisadikisha. Basi katika wakati mmoja manabii mia nne pia walikuja ambao hadi sasa Biblia inatoa ushahidi juu ya ujaji wao.

Siri iliyomo ndani ya kutuma mitume wengi ni hii kuwa Mwenyezi Mungu Amekwishafanya ahadi imara ya kuwa yule atakayekataa Kitabu Chake cha kweli, adhabu yake ni jahanamu ya kudumu, kama Asemavyo:

وَالَّذِيْنَ كَفَرُوْا وَكَذَّبُوْا بِاٰيٰتِنَآ اُولٰٓئِكَ اَصْحٰبُ النَّارِ هُمْ فِيْهَا خٰلِدُوْنَ[76]

Yaani, waliokufuru na kukadhibisha aya zetu, hao ndio watu wa Jahanamu, humo watadumu kukaa.

Sasa, kwa kuwa adhabu ya kukikana Kitabu cha Mungu ilikuwa ni kali sana na upande mwingine suala la Unabii na wahyi wa Mungu lilikuwa gumu mno, bali uwepo wa Mwenyezi Mungu pia ilikuwa shida kueleweka hata kwamba macho ya mtu yasipong'arika na nuru Anayojalia Mungu haikuwezekana kujipatia maarifa ya kweli na

[76] Sura Al-Baqara, 2:40. Mwenezi.

matakatifu, achilia mbali kupata maarifa ya mitume wake na maarifa ya Kitabu Chake, kwa hiyo, Urahamani wa Mungu ulitaka viumbe vipofu wasioona wasaidiwe, na kutumwa mara moja Mtume na Kitabu kusichukuliwe kutosha na kuwatupa katika Jahanamu ya kudumu wazikanao zile itikadi ambazo baada ya zama ndefu kupita hawawezi kuzifahamu zaidi ya kuwa hizo ni maandiko matakatifu na mazuri. Na kwa hakika ni jambo lililo wazi sana kwamba Yule Mungu Ambaye jina lake ni Rahmani na Rahimu Anawezaje kujichagulia kanuni hii kwamba pasipo kutimiza hoja kikamilifu Awatie katika Jahanamu ya daima watu wa nchi mbalimbali waliopata kusikia jina la Kurani na Mtume[saw] baada ya mamia ya miaka, tena hao hawawezi kufahamu Kiarabu wala hawawezi kuona uzuri wa Kurani. Dhamiri ya mtu gani yaweza kukubali kwamba pasipo kumhakishia kuwa Kurani Tukufu imetoka kwa Mungu aadhibiwe vikali hivyo. Basi, hii nidyo

sababu Mwenyezi Mungu Akatoa ahadi ya Makhalifa kuja daima ili wakipata nuru za Unabii kwa njia ya 'kivuli' waikengemeke dunia na kuwaonyesha watu uzuri wa Kurani Tukufu. Ikumbukwe pia kuwa hoja hukamilika kwa njia tofauti katika zama mbalimbali, na Mujaddidi wa zama huja na nguvu na vipawa na sifa kamilifu ambazo kuondolea mbali maovu yaliyopo hutegemea kwazo. Basi Mwenyezi Mungu Ataendelea kufanya hivyo mpaka Apendapo kuwa athari za uongofu na usuluhivu zibaki duniani. Na mambo hayo siyo bila uthibitisho, bali mifano yake ya kurejelea inashuhudia jambo hili. Hata tukiachilia mbali manabii, mitume na Muhaddathina wa nchi mbalimbali na kuangalia manabii, mitume na Muhaddathina wa wana wa Israeli pekee, twaona kwamba katika muda wa miaka elfu moja na mia nne, yaani tokea Hadhrat Musa hadi Hadhrat Masihi, maelfu ya manabii na Muhaddathina walitoka ambao wakajibidiisha

kushughulikia kuhudumia Torati. Na Kurani ni shahidi juu ya habari hii, na Biblia yashuhudia kuwa manabii hao walikuwa hawaleti Kitabu kipya wala hawakufundisha dini mpya. Walikuwa ni mahadimu wa Torati, wakadhihirika katika nyakati ambapo ukanaji Mungu, utovu wa imani, maovu na dhuluma vikatapakaa. Sasa mwenye kuzingatia azingatie kuwa kama kwa ajili ya sheria pungufu ya Musa[as] isiyokuwa kwa ajili ya mataifa yote ya dunia wala haikuwa kuendelea hadi Kiyama, Mwenyezi Mungu Aliijali na kuwatuma maelfu ya manabii kuijadidisha na mara nyingi manabii hao wakaonyesha ishara hata kwamba wana wa Israeli wakamwona upya Mungu, basi kwa nini umati huu uitwao bora kuliko nyimati zote na ulioambatana na mbora wa mitume uchukuliwe kuwa na bahati mbaya kwamba Mwenyezi Mungu baada ya kuuangalia kwa jicho la rehema na kuonyehsa nuru za kimbingu Akageuza uso wake upande mwingine. Kisha mamia ya miaka

ikapita juu ya umati huu baada ya kufariki Mtume[saw] na ukapatwa na fitina maelfu za aina aina, yakaja matetemeko makubwa makali, udajali wa namna namna ukasumbua na dunia ikaishambulia dini hii imara, na baraka na miujiza yake yote ikakataliwa, na iliyopendwa ikafanywa kuwa isiyopendwa, lakini Mungu Hakuinua macho kuiangalia wala hakuuhurumia umati huu, wala Hakufikiria kuwa hao nao ndio wanadamu wanyonge kama wana wa Israeli, na mimea yao pia kama ya wana wa Israeli inahitaji daima umwagiliaji wa kimbingu. Je Mungu Mkarimu Aweza kufanya hivyo ambaye Alikuwa Amemtuma Mtume[saw] kuondolea mbali kwa kudumu uharibifu? Je twaweza hata kudhani kuwa nyimati zilizopita zilihurumiwa na Mwenyezi Mungu na kwa hiyo baada ya kuleta Torati Akatuma maelfu ya mitume na Muhaddathina kuisaidia Torati na kuzihuisha nyoyo mara kwa mara, lakini umati huu ulighadhibikiwa kwa hiyo baada ya

kuteremsha Kurani Tukufu Akasahau mambo hayo yote na kuwaacha kwa kudumu wanazuoni waitegemee akili na ijtihadi yao. Na kuhusiana na Hadhrat Musa[as] Akasema kwa uwazi:

وَكَلَّمَ اللّٰهُ مُوْسٰى تَكْلِيْمًا ۚ رُسُلًا مُّبَشِّرِيْنَ وَمُنْذِرِيْنَ لِئَلَّا يَكُوْنَ لِلنَّاسِ
عَلَى اللّٰهِ حُجَّةٌ ۢ بَعْدَ الرُّسُلِ ۗ وَكَانَ اللّٰهُ عَزِيْزًا حَكِيْمًا ○[77]

Yaani, Mungu Akaongea na Musa, na Akawatuma ili kumsaidie na kumsadikisha mitume watoao habari njema na kuonya ili watu wasibakiwe na hoja, na waiamini Torati kwa ukweli wa moyo kwa kuona kundi la manabii waliofululiza. Na Akasema:

وَرُسُلًا قَدْ قَصَصْنٰهُمْ عَلَيْكَ مِنْ قَبْلُ وَرُسُلًا لَّمْ نَقْصُصْهُمْ عَلَيْكَ[78]

Yaani, Tulituma mitume wengi, tuliokuhadithia baadhi yao, na mitume wengine Hatukukuhadithia. Lakini Hakuwafanyia mpango huo waitafutao dini ya Kiislamu, kana kwamba ile rehema na ile fadhili iliyokuwa juu ya watu wa Hadhrat Musa haikuwa juu ya umati huu.

---

[77] Sura An-Nisaa, 4:165-166. Mwenezi.
[78] Sura An-Nisaa, 4:165. Mwenezi.

Ni dhahiri kuwa miujiza na karama za zamani baada ya kupita muda mrefu hubakia kama visa tu, na vizazi vijavyo wasipoona miujiza hatimaye wanaishuku miujiza ya zamani. Tena kwa kuwa mfano wa maelfu ya manabii upo mbele ya macho yao, kwa hiyo umati huu utavunjika moyo, na wakiwaona wana wa Israeli kuwa na bahati njema watawaonea wivu, au wakiingiwa na mawazo mabaya watazifikiria habari hizo pia kuwa ni visa tu. Na kauli hii kwamba wamekwisha pita maelfu ya manabii hapo kabla na miujiza mingi pia ilifanyika, kwa hiyo umati huu hauna haja ya miujiza, karama na baraka, basi Mwenyezi Mungu Akaunyima hayo yote, ni maneno tu wanayotamka watu ambao hawaijali imani, waila binadamu ni mnyoge sana na daima anahitaji imani kuimarishwa. Katika njia hii dalili za kubuniwa haziwezi kufaa katu mpaka ijulikane upya kuwa Mungu Yupo. Naam, imani mbovu isiyoweza kuzuia maovu inaweza kubaki kimaandiko na kiakili. Hapa ikumbukwe pia kuwa ukamilifu wa dini haumaanishi kuachilia mbali kabisa

kuitunza ipasavyo. Mathalan, kama mtu aijenge nyumba na kukitayarisha kila chumba vizuri sana na kuyatimiza mahitaji yake yote vizuri kabisa yanayohusikana na jengo, kisha baada ya muda upepo mkali uvume, mvua zinyesha na nakshi za nyumba zipatwe na mavumbi na uzuri wake ufichike, hapo mrithi wa nyumba hii apende kuisafisha na kuifanya nyeupe, lakini akatazwe kwa kuambiwa kuwa nyumba ilikwishakamilika. Basi ni dhahiri kuwa kumkataza ni upumbavu mtupu. Ni masikitiko kuwa wapinzani kama hao hawazingatii kwamba kukamilika kwa kitu ni jambo moja na kulisafisha jengo lililokamilika ni jambo jingine. Kumbukeni kuwa Mujaddidina hawapunguzi wala hawaongezi chochote katika dini. Naam, wanaiimarisha upya nyoyoni dini iliyopotea. Na kusema kwamba kuwaamini Mujaddidina sio faradhi, ni kuachana na amri ya Mwenyezi Mungu, kwani Yeye Anasema:

وَمَنْ كَفَرَ بَعْدَ ذٰلِكَ فَاُولٰٓئِكَ هُمُ الْفٰسِقُوْنَ[79]

[79] Sura An-Nuur, 24:56. Mwenezi.

Yaani, baada ya Makhalifa kutumwa, atakayewakataa, huyo atakuwa miongoni mwa mafasiki.

Sasa muhtasari wa maelezo hayo yote twaandika hapa chini kwa kifupi. Ni hivi kwamba inathibitika kutokana na hoja zifuatazo kuwa baada ya kufariki kwa Mtume[saw] waendelee warekebishaji kufika katika nyakati za ufisadi na fitina ambao wapewe jukumu hili moja miongoni mwa majukumu ya manabii kwamba wawaite watu kwenye dini ya haki na kuiondolea mbali ile bidaa iliyokwisha ingia katika dini, na kwa kujipatia mwanga wa kimbingu wawaonyeshe watu ukweli kwa kila jiha, na kuwavutia watu kwenye ukweli, upendo na utakaso kwa mfano wao mtukufu. Na hoja zenyewe ni hizi:

Ya kwanza ni kuwa kiakili ni jambo la lazima kwamba kwa kuwa mambo yanayohusikana na Mungu na maisha ya Akhera ni mepesi sana na ni ya kinadharia, kana kwamba mtu analazimika kuyaamini mambo yasiyoonekana na ni zaidi ya akili, maana hakuna mtu aliyemwona Mwenyezi Mungu wala hakuna aliyeshuhudia Pepo wala

Jahanamu, wala hakuna aliyeonana na malaika, isitoshe, maamrisho ya Mungu ni dhidi ya jazba za nafsi, na mambo yanayoipa nafsi utamu yamekatazwa na Mungu, kwa hiyo kiakili sio bora tu bali ni wajibu kuwa manabii watukufu wanaoleta Sheria na Kitabu na wanayo athari na nguvu ya kutakasa ndani ya nafsi yao, hao ama waje na umri mrefu na daima na katika kila karne wakutane na umati wao mpya na kwa kuwaleta chini ya mbawa zao za baraka wawapatie baraka na nuru na maarifa ya kiroho waliyokuwa wamewapa mwanzoni mwa zama zao, la sivyo waendelee daima kupatikana warithi wao katika nyakati za fitina na ufisadi, ambao wawe na sifa zao ndani yao na waweze kueleza kwa wahyi na ufunuo mambo yenye keto na maarifa ya Kitabu cha Mungu na kuyadhihirisha yanayosimuliwa kwa sura ya matukio yanayoshuhudiwa na kumfikisha mtafuta ukweli mpaka kwenye yakini, ili binadamu mwenye kushuku na kusahau asinyimwe kupata baraka za kweli. Kwani, ni wazi na dhahiri kabisa kuwa zama za nabii mmoja zinapofika mwisho wake

na wanakuwa wamekufa walioziona baraka zake, hapo yaliyoshuhudiwa na macho hubakia kuwa masimulizi tu. Kisha, khulka za nabii huyo na ibada za nabii huyo na subira na uimara na ukweli na uaminifu wake na misaada yote ya Mungu na karama na miujiza vilivyokuwa ni dalili za ukweli wa Unabii wake na ukweli wa madai yake vinaonekana kwa watu wa karne mpya kama visa tu, kwa hiyo ile imani na jazba ya utii inayokuwa kwa waliomwona nabii, huwa hawanayo watu wengine. Na ni dhihiri ya kwamba ukweli wa imani walioonyesha masahaba wa Mtume[saw] na kutoa dhabihu ya heshima zao katika njia za Islam kwa ikhlasi sana, mfano wake licha ya kuonekana katika karne nyingine hata katika watu wa karne yenyewe ya pili, yaani katika Tabi'ina haukupatikana. Sababu yake ilikuwa nini? Ilikuwa ni hii tu kuwa masahabara walikuwa wameuona uso wa yule mwanamume mkweli ambaye hata Makureishi wa Makkah mara walipata kutoa ushuhuda wao kuwa yu Mpenzi wa Mungu. Wakiona maombi yake ya kila siku na sijida zake kwa mahaba na kushuhudia hali ya

kujipoteza katika utii na alama za kweli za mapenzi ya hali ya juu na nuru ya Mungu kuteremka mfululizo juu ya uso wake mtakatifu, walikuwa wakisema عَشِقَ مُحَمَّدٌ عَلٰى رَبِّهٖ, yaani Muhammad ameingiwa na huba ya Mola wake. Isitoshe, masahaba hawakuona tu ukweli, mapenzi na ikhlasi, bali pamoja na ule upendo uliofurika kama mto moyoni mwa Seyidi wetu Muhammadsaw wakashuhudia pia mapenzi ya Mungu kwa sura ya misaada yake ya kimwujiza, ndipo wakatambua kuwa Mungu Yupo, na mioyo yao ikasema kuwa Mungu Yu pamoja na mwamume huyu. Wakaona maajabu mengi ya Mungu na kushuhudia ishara nyingi za kimbingu hata kwamba hawakubakiwa na shaka kwamba Yupo kwa hakika Yule Mtukufu Aitwaye Mungu, na Ambaye kila kitu kipo chini ya mamlaka yake, Ambaye hakuna kisichowezekana kwake. Ndiyo sababu wakatenda mambo ya ukweli na kujibidiisha sana mno kutekeleza mambo magumu asiyoweza mwanadamu katu mpaka shaka

zake zote zitoweke. Wakajionea wenyewe kwa macho yao kuwa Yule Mtukufu Anaridhika hapo tu ambapo mtu anaingia katika Islam na kumtii Mtume Mkarimsaw kwa moyo na roho. Ndipo baada ya yakini ya haki, utii walioonyesha na kutenda mambo kwa jazba ya utii na jinsi walivyojitupa mbele ya mwongozi wao mtukufu, hayo mambo hayawezekani mtu ayapate mpaka ule ustawi uwe mbele ya macho yake waliopata masahaba. Na kwa kuwa ni muhali kujipatia sifa hizi kamilifu bila ya njia hizo, na kupata wokovu kwa yakini pia ni muhali pasipo kwa njia ya sifa hizo kamilifu, basi ikawa hakuna budi kuwa Yule Mungu Mkarimu Aliyemwita kila mmoja kwa kumwokoa, Aweke mpango kama huo kwa kila karne ili waja wake wasinyimwe kupata madaraja ya yakini ya haki.

Na kusema kwamba Kurani na Hadithi zinatutosha na hatuna haja ya kukaa na wakweli, basi haya ni mafundisho yaliyo kinyume na Kurani. Kwani Mungu

Mwenye enzi Anasema وَكُوْنُوْا مَعَ الصّٰدِقِيْنَ[80] Na ma-saadik ndio wale walioutambua ukweli kwa busara kabisa kisha wakaimarika juu yake kwa moyo na roho. Na busara hii ya hali ya juu haiwezekani pasipo kupata msaada wa kimbingu utakaofikisha mpaka kwenye hali yenye yakini. Basi, sawa na maana hii wakweli hasa ni manabii, mitume, muhaddathina na mawalii wakamilifu watimilifu ambao mwanga wa kimbingu uliwaangukia na ambao wakapata kumwona Mwenyezi Mungu katika dunia hii hii kwa macho ya yakini. Na ndani ya aya iliyotajwa hapo juu kuna ishara inayodhihirisha kuwa dunia haiwi pasipo uwepo wa wakweli, kwani amri ya kudumu ya 'kuweni pamoja na wakeli' yalazimisha uwepo wa wakweli kwa kudumu.

Isitoshe, uchunguzi unahakikisha kuwa watu wanaopitisha umri wao wasipojali kukaa na wakweli,

[80] Tafsiri: Na kuweni pamoja na wasemao kweli, Sura At-Tauba, 9:119. Mwenezi.

katu haziwezi elimu na fani zao kuwatakasa na jazba zao za kimwili, wala hawawezi kujipatia hata kwa uchache ile daraja ya Islam ya kuwa na yakini moyoni kwamba Mungu Yupo. Hao huwa hawanayo yakini juu ya uwepo wa Mungu jinsi wanavyokuwa na yakini juu ya mali yao iliyomo ndani ya masanduku yao, au juu ya nyumba zao wanazomiliki. Wanachelea kula aseneki — sumu ya panya — kwani wanajua sumu hiyo inahilikisha, lakini hawaichelei sumu ya madhambi ilhali kila siku wanasoma ndani ya Kurani:

إِنَّهُۥ مَن يَأْتِ رَبَّهُۥ مُجْرِمًا فَإِنَّ لَهُۥ جَهَنَّمَ لَا يَمُوتُ فِيهَا وَلَا يَحْيَىٰ [81]

Basi ukweli wenyewe ni kuwa yule mtu asiyemtambua Mwenyezi Mungu, huyo hawezi kuitambua Kurani pia. Naam, hii ni kweli kuwa Kurani imeshuka kwa ajili ya mwongozo, lakini miongozo ya Kurani inafungamana na mja yule aliyeteremshiwa Kurani

---

[81] Tafsiri: Hakika atakayekuja kwa Mola wake hali yu mkosefu, basi kwa yakini atapata Jahanamu, hatakufa humo wla hataishi. Sura Twaa Haa, 20:75. Mwenezi.

au yule aliye naibu wake kutoka kwa Mungu. Kama Kurani pekee ingetosha, basi Mwenyezi Mungu Aliweza kuwa Kurani ingeandikwa juu ya majani ya miti ama ingeteremka ikiishaandikwa tayari. Lakini Mwenyezi Mungu Hakufanya hivyo, bali Hakuituma Kurani duniani maadamu Mwalimu wa Kurani hakutumwa. Angalieni mkifungua Kurani Tukufu kuwa ni sehemu ngapi zenye aya za madhumuni haya:

يُعَلِّمُهُمُ الْكِتٰبَ وَالْحِكْمَةَ[82]

Yaani, Mtume[saw] anafundisha Kurani na hekima za Kurani. Tena, sehemu nyingine Anasema:

لَّا يَمَسُّهٗۤ اِلَّا الْمُطَهَّرُوْنَ[83]

yaani, hakika za Kurani na mambo yake yenye keto hufunguliwa kwa wale tu waliotakaswa. Basi, yathibitika kwa uwazi kuwa mwalimu mmoja anahitajika kwa kuielewa Kurani, ambaye

[82] Sura Al-Jumu'ah, 62:3. Mwenezi.
[83] Sura Al-Waqi'ah, 56:80. Mwenezi.

Mwenyezi Mungu Amemtakasa kwa mkono Wake. Kama isingekuwa sasa haja ya mwalimu, basi isingekuwa hata katika siku za awali pia. Na kauli hii kwamba katika siku za awali kulikuwa na haja ya mwalimu ili kutatua matatizo ya Kurani, lakini hayo yalipokwisha elezwa tayari, kuna haja gani, basi jawabu laki ni kuwa yaliyotatuliwa nayo baada ya muda fulani yanastahili kutatuliwa tena. Isitoshe, katika kila zama umati unayakabili pia matatazo mapya. Na Kurani kweli imejikusanyia elimu zote, lakini si lazima elimu zote zidhihirike katika zama moja tu. Bali jinsi yanavyojitokeza matatizo, ndivyo zinavyofunguka elimu za Kurani. Na sawa na matatizo ya kila zama, hutumwa kuyatatua hayo matatizo walimu wa kiroho ambao huwa warithi wa mitume, wanaopta sifa za mitume wakiwa kivuli chao. Na juhudi za mujaddidi fulani zinapofanana sana mno na juhudi za mtume fulani, basi mujaddidi huyo anapewa jina la huyo mtume.

Na kunakuwa na haja ya walimu wapya vilevile, kwani baadhi ya sehemu za Kurani Tukufu zahusikana na hali siyo na kauli. Na Mtume[saw] aliye Mwalimu wa Kwanza na mrithi wa kiti cha enzi aliwafahamisha masahaba kwa hali yake mambo hayo yenye kina, mathalan, kauli hii ya Mwenyezi Mungu kwamba Mimi ni Mjuzi wa mambo ya ghaibu, Mimi Nayaitikia maombi, Mimi ni Mweza, Nakubali dua na Ninawafikisha wtafutaji wa kweli kwenye nuru, Nawafunulia ufunuo waja wangu wakweli, Namtilia Roho yangu yule miongoni mwa waja wangu nimtakaye. Hayo yote ndiyo mambo ambayo hayawezi kufahamika kabisa mpaka mwalimu ayaonyeshe mwenyewe akiwa mfano wake. Basi ni wazi kuwa wanazuoni wa kidhahiri ambao wenyewe ni vipofu hawawezi kufahamisha mafundisho hayo, bali hao kila wakati wanawatilia wanafunzi wao dhana mbaya dhidi ya adhama ya Islam na wanasema hayo mambo hayawezekani

sasa, bali yamebakia nyumba tu. Yafahamika kutokana na maelezo yao kana kwamba Islam hivi sasa siyo dini iliyo hai, wala hakuna njia yoyote iwayo kupata mafundisho yake ya kweli. Lakini ni dhahiri kwamba kama utashi wa Mwenyezi Mungu kwa ajili ya watu wake ni kuwa Awanyweshe sikuzote maji kutoka katika chemchemi ya Kurani Tukufu, bila shaka Yeye Atazichunga kanuni zake za zamani Alivyoendelea kufanya tangu zamani. Na kama mafundisho ya Kurani yanaishia pale tu yaishiapo mafundisho ya mwanafalsafa mwenye fikara ya kina na mwenye uzoefu, na hamna ndani yake mafunzo ya kimbingu yanayofahamishwa kwa kupitia mfano wa hali, hapo — Mungu Apishe mbali — ujaji wa Kurani ni bure tu. Lakini najua kuwa kama mtu akifikiria kidogo tu kwamba ni kitu gani kinachopambanua baina ya mafundisho ya manabii na mafundisho ya wanafalsafa, yote yakiwa ya kweli, basi kipambanuzi chenyewe ni hiki

tu kuwa sehemu kubwa ya mafundisho ya manabii inazidi eneo la akili, isiyoweza kueleweka kwa njia yoyote isipokuwa ifahamishwe na kufundishwa ki-hali. Wale tu wanaweza kuitilia nyoyoni ambao ndio weledi wa hayo mambo. Kwa mfano malaika hutoa roho kwa njia fulani, kisha huipeleka hivi kule mbinguni, tena hesabu huchukuliwa hivi kaburini, Pepo ni hivi, Jahanamu ni hivi, njia nyembamba ipitayo juu ya Jahanamu ni hivi, Arshi ya Mungu wanaibeba malaika wanne na siku ya kiyama wataibeba wanane, Mungu Anawateremshia hivi waja wake wahyi au Anawafungulia milango ya kashfi. Hayo yote ni mafundisho ya ki-hali wala hayawezi kufahamika kwa kuelezwa na maneno pekee. Kama ni hivyo, basi nakariri mara ya pili kuwa ikiwa Mungu Mwenye Enzi Amewanuilia waja wake kwamba sehemu hii ya mafundisho ya Kitabu Chake isikome mpaka kwa zama za awali, basi bila shaka Atakuwa Ameishafanya mpango

kwamba waalimu wa sehemu hii ya mafundisho waendelee kufika daima dawamu, kwani sehemu ya mafundisho ya ki-hali haiwezi kueleweka pasipo kupitia waalimu walio weledi wake wa daraja ya juu. Na dunia hujikwaa sana kwa mambo madogo madogo. Basi, kama ndani ya Islam, baada ya Mtume[saw], hawakutokea waalimu kama hao waliokuwa na nuru ya Unabii kwa njia cha kivuli, hapo kana kwamba Mwenyezi Mungu kusudi Akaipoteza Kurani, kwani Akawaondoa haraka duniani walioifahamu kwa hakika na kwa kweli. Lakini hiyo ni kinyume cha ahadi hii Yake kama Alivyosema:

إِنَّا نَحْنُ نَزَّلْنَا الذِّكْرَ وَإِنَّا لَهُ لَحٰفِظُونَ[84]

Yaani, Sisi Tuliteremsha Kurani na Sisi ndio Tutakaoendelea kuilinda. Sasa siwezi kuelewa kuwa kama hawakubaki waielewao Kurani na wakatoweka wenye kuiamini kwa yakini na

[84] Sura Al-Hijr, 15:10. Mwenezi.

ki-hali, hapo umekuwaje ulinzi wa Kurani! Je ulinzi unamaanisha kwamba nakili nyingi za Kurani zikiandikwa kwa maandishi mazuri zitafungwa masandukuni hadi kiyama kama hazina zilizozikwa, japo hazimfai yeyote lakini zinabaki salama chini ya ardhi? Je yupo mtu awezaye kufahamu kuwa huo ndio utashi wa Mungu katika aya hii? Kama huo ndio utashi, basi ulinzi kama huu si jambo la sifa, bali ni kichekesho. Kueleza ulinzi wa aina hii ndiyo kuwafanya maadui wafanye masihara, kwani kama makusudio hasa hakuna, ulinzi wa kidhahiri utafaa nini? Yawezekana kuwa nakala moja ya Injili au Torati iwepo salama ndani ya shimo fulani. Maelfu ya vitabu vyapatikana vya aina hii duniani ambavyo bila kupungukiwa na kuongezeka vimefahamika kuwa ni utungo wa mwandishi fulani. Basi, ndani yake kuna uzuri gani, na umati ukaipata faida gani hasa? Ijapokuwa sikatai kuwa ulinzi wa kidhahiri wa Kurani pia ni mwingi sana kuliko vitabu vyote

vya dunia, na ni wa kimwujiza pia, lakini Mungu Aangaliaye mambo ya kiroho hatuwezi kumdhania kuwa Alimaanisha ulinzi wa maneno na herufi pekee, ilhali neno *dhikr* — ukumbusho — pia linatoa ushahidi kuwa Kurani ikiwa ukumbusho itahifadhiwa mpaka kiama na wenye kuikumbuka wataendelea kuzaliwa daima dumu dawamu. Na ipo aya nyingine pia iliyo dalili yake bayana, nayo ndiyo hii:

بَلْ هُوَ ءَايَٰتٌۢ بَيِّنَٰتٌ فِى صُدُورِ ٱلَّذِينَ أُوتُوا۟ ٱلْعِلْمَ [85]

Yaani, Kurani ni aya bayana zilizomo ndani ya vifua vya wale waliopewa elimu. Basi, ni dhahiri kuwa aya hii yamaanisha kwamba waaminio wamepewa elimu ya Kurani Tukufu na kujaliwa kutenda sawa nayo. Na kwa kuwa mahali pa Kurani ni vifua vya waaminio, basi aya hii:

إِنَّا نَحْنُ نَزَّلْنَا ٱلذِّكْرَ وَإِنَّا لَهُۥ لَحَٰفِظُونَ [86]

---

[85] Sura Al-'Ankabuut, 29:50. Mwenezi.

[86] Sura Al-Hijr,15:10. Mwenezi.

yamaanisha nini isipokuwa kwamba Kurani haitafutwa vifuani kama Torati na Injili zilivyofutiliwa mbali vifuani mwa Wayahudi na Wakristo. Na ingawaje Torati na Injili zilikuwa mikononi mwao na masandukuni mwao lakini zikafutiliwa mbali nyoyoni mwao, yaani nyoyo zao hazikuimarika juu yao, na hawakuiimarisha Torati na Injili ndani ya mioyo yao wala hawakuzirudisha katika hali yao ya kwanza. Ilmuradi, aya hii inasema kwa kupaza sauti kuwa sehemu yoyote iwayo ya Kurani hatitaangamia wala kupotea, na jinsi tangu siku ya kwanza mmea wake ulivyoimarishwa mioyoni ndivyo itakavyoendelea silsila hii mpaka kiama.

Pili, jinsi ambavyo akili inaliwajibisha jambo hili na kulichukua kuwa ni la lazima kwamba kwa kuvifundisha vitabu vya Mungu na kuvifafanua hakuna budi waendelee kuzaliwa daima mara kwa mara wafunuliwao na Mungu na kuongea na

Mungu na waelimishwao na Mungu kama manabii, ndivyo ambavyo tuiangalipo Kurani na kuitafakari kwa makini tunaikuta kuwa hiyo nayo inasema kwa kupaza sauti kuwa uwepo wa walimu wa kiroho kwa kudumu umekwisha amuliwa katika utashi wa Mungu tangu zamani. Angalieni, Mungu Mwenye Enzi anasema:

وَ اَمَّا مَا يَنۡفَعُ النَّاسَ فَيَمۡكُثُ فِى الۡاَرۡضِ[87]

(Juzuu 13). Yaani, kitu kiwafaacho watu kinabaki ardhini. Sasa ni dhahiri shahiri kuwa duniani humu wanaowanufaisha watu zaidi sana ndio manabii ambao kwa makarama na miujiza na matabiri yao na kweli zao na maarifa na unyofu wao wanaimarisha imani ya watu na kuwanufaisha watafutao haki kidini. Na ni wazi kuwa hao hawakai duniani kwa muda mrefu, bali baada ya kuishi kwa muda kidogo wanaondolewa katika dunia hii. Lakini, hakuna hitilafu katika madhumuni ya aya hii, na

[87] Sura Ar-Ra‘d, 13:18. Mwenezi.

haiyumkiniki hitilafu iwepo katika Neno la Mungu. Basi, kuhusiana na manabii, aya humaanisha kuwa manabii hubakizwa kwa njia ya wale walio mfano wao. Na Mwenyezi Mungu wakati wa kila haja Anamfanya mja wake fulani kuwa mithili na mfano wao ambaye akiwa kama hao anakuwa sababu ya kupata maisha yao ya milele. Na ili kuendeleza uwepo wa mfano huo Mwenyezi Mungu Akawafundisha waja wake dua hii:

اِهْدِنَا الصِّرَاطَ الْمُسْتَقِيْمَ صِرَاطَ الَّذِيْنَ اَنْعَمْتَ عَلَيْهِمْ [88]

Yaani, Ee Mungu wetu, Utuonyeshe ile njia iliyonyoka, iliyo njia ya wale waja wako Uliowaneemesha. Na ni dhahiri kuwa neema Aliyowapatia manabii, ambayo kuiomba imeamrishwa, siyo aina ya dirhamu na dinari, bali ndiyo neema ya nuru na baraka, mahaba na yakini, karama na msaada wa kimbingu, kibali na maarifa matimilifu makamilifu, wahyi na kashfi. Na

---

[88] Sura Al-Faatiha, 1:6-7. Mwenezi.

Mwenyezi Mungu Akauamrisha umati huu kuomba neema hiyo kwani kwanza Alikuwa Ameishanuia kuutolea hiyo neema. Basi, imethibitika waziwazi kutokana na aya hiyo kwamba Mwenyezi Mungu Anafanya umati huu kuwa warithi wa manabii wote ki-kivuli ili uwepo wa manabii ki-kivuli ubaki kwa kudumu na dunia isiwe pasipo uwepo wao. Siyo tu Akaamuru kuomba dua, bali ndani ya aya moja Akatoa ahadi pia, nayo ndiyo hii:

وَالَّذِيْنَ جَاهَدُوْا فِيْنَا لَنَهْدِيَنَّهُمْ سُبُلَنَا[89]

Yaani, wale watakaojitahidi katika njia yetu iliyo njia iliyonyoka, Tutawaongoza kwenye njia zetu. Na ni dhahiri kwamba njia za Mwenyezi Mungu ni zile zile walizoonyeshwa manabii.

Na zipo baadhi ya aya nyingine zithibitishazo kuwa Mungu Mkarimu lazima Amenuia kuwa walimu wa kiroho walio warithi wa manabii waendelee kutokea daima, nazo ni hizi:

89 Sura Al-‘Ankabuut, 29:70. Mwenezi.

وَعَدَ اللّٰهُ الَّذِيْنَ اٰمَنُوْا مِنْكُمْ وَعَمِلُوا الصّٰلِحٰتِ لَيَسْتَخْلِفَنَّهُمْ فِي الْاَرْضِ

كَمَا اسْتَخْلَفَ الَّذِيْنَ مِنْ قَبْلِهِمْ [90]

وَلَا يَزَالُ الَّذِيْنَ كَفَرُوْا تُصِيْبُهُمْ بِمَا صَنَعُوْا قَارِعَةٌ اَوْ تَحُلُّ قَرِيْبًا مِّنْ دَارِهِمْ

حَتّٰى يَاْتِيَ وَعْدُ اللّٰهِ ۗ اِنَّ اللّٰهَ لَا يُخْلِفُ الْمِيْعَادَ [91]

وَمَا كُنَّا مُعَذِّبِيْنَ حَتّٰى نَبْعَثَ رَسُوْلًا [92]

Yaani, Mwenyezi Mungu Amewaahidi, Enyi waaminio wa umati wa Muhammadsaw, kwamba Atawafanyeni Khalifa ardhini kama Alivyowafanya wa kabla yenu. Na sikuzote makafiri wataendelea kusibiwa na misiba ya aina fulani, ikiwa ya kimwili au ya kiroho, au itasogelea karibu na nyumba yao, mpaka itakuja ahadi ya Mungu. Na Mwenyezi Mungu Hafanyi kinyume na ahadi zake. Nasi Hatuiteremshii kaumu yoyote adhabu mpaka Tumepeleka mtume.

Kama mtu azifikirie aya hizo kwa makini na kuzizingatia vizuri, niwezeje kusema kuwa

[90] Sura An-Nuur, 24:56. Mwenezi.

[91] Sura Ar-Ra‘d, 13:32. Mwenezi.

[92] Sura Banii Israiil, 17:16. Mwenezi.

hajafahamu kuwa Mwenyezi Mungu Anaahidi kwa uwazi Ukhalifa wa kudumu kwa umati huu. Kama Ukhalifa haukuwa wa kudumu, basi kuufananisha na makahalifa wa sheria ya Musa ilikuwa na maana gani? Kama Khilafat Rashida baaada ya kuendelea kwa miaka thelathini ikamalizika kwa kudumu, basi inalazimu kuwa Mwenyezi Mungu katu Hakuwa na nia ya kuuwekea wazi umati huu milango ya ustawi kwa kudumu, kwani mauti ya silsila ya kiroho, matokeo yake ya lazima ndiyo mauti ya dini. Na ile dini haiwezi kuitwa kuwa hai ambayo waumini wake wenyewe wakiri kwa midomo yao kwamba tangu miaka elfu moja mia tatu dini hii imekufa na Mwenyezi Mungu Hakukusudia kabisa kwa dini hii kuwa nuru ya uhai wa kweli iliyokuwa kifuani mwa Nabii Mkarimusaw iendelee ndani ya wengine kama urithi.

Nasikitika kwamba wanaoshikilia fikara hii, hawalizingatii neno Khalifa linalofahamika kwama

linatokana na istikhlaf, kwani Khalifa ndiye mrithi. Na mrithi wa Mtume kwa kweli huweza kuwa yule tu ambaye anazo ndani yake sifa za Mtume ki-kivuli. Kwa hiyo, Mtume[saw] hakupenda neno Khalifa litumike kwa wafalme wadhalimu, kwani Khalifa kwa hakika huwa kivuli cha Mtume. Na kwa kuwa mtu haishi milele, hivyo Mwenyezi Mungu Akaukilia kuubakiza ki-kivuli uwepo wa mitume, ambao ndio bora kuliko watu wote, mpaka Kiama. Basi, kwa hiyo, Atafanya mpango wa ukhalifa ili dunia isinyimwe katu baraka za Utume katika zama zozote. Basi, yule auaminiye Ukhalifa mpaka kwa miaka thelathini tu, yeye mtu huyo hajali makusudio hasa ya Ukhalifa wala hajui kuwa utashi wa Mwenyezi Mungu haukuwa asilani kuendeleza baraka za Utume kwa sura ya Makhalifa kwa miaka thelathini pekee baada ya kufariki Mtume[saw], na baada yake kama dunia inaangamia na iangamie tu, haidhuru. Bali, katika siku za awali

uwepo wa makhalifa haukuwa na haja zaidi ya kuzagaza adhama ya Islam, kwani nuru za Utume na ubora wa Unabii ulikuwa ukitapakaa mpya mpya na maelfu ya miujiza ilikuwa imeteremka kama inyeshavyo mvua. Na kama Mwenyezi Mungu Angetaka, basi haikuwa mbali na suna na desturi yake kumwongezea Mtume[saw] umri wake hadi kwa muda wa miaka thelathini wa makhalifa hao wanne, hapo Mtume[saw] angefikia umri wa miaka 93, na kiasi hicho si zaidi ya umri wa kawaida wa zama zile wala si zaidi ya kanuni ya tabia ya asili tunayoona kuhusiana na umri wa biandamu.

Basi, kuwa na fikara hii dhilifu kumhusu Mwenyezi Mungu kuwa Yeye Alifikiria tu miaka thelathini ya umati huu, kisha Akauacha ndani ya upotevu kwa kudumu, na nuru ile Aliyoendelea kuonyesha tangu kale ndani ya umati wa manabii wa zamani katika kioo cha Ukhalifa Hakupenda kuionyesha hiyo kwa umati huu, je akili timamu itakubali hayo mambo

kumhusu Mungu Mrehemevu na Mkarimu? Hata kidogo! Tena aya hii ni shahidi dhahiri juu ya Ukhalifa wa Maimamu:

وَلَقَدْ كَتَبْنَا فِي الزَّبُورِ مِن بَعْدِ الذِّكْرِ أَنَّ الْأَرْضَ يَرِثُهَا عِبَادِيَ الصَّالِحُونَ[93]

Kwani, aya hii inatangaza waziwazi kuwa Ukhalifa wa Kiislamu ni wa kudumu kwa sababu neno Yarithuhaa linahitaji dawamu, maana kama zamu ya mwisho ziwe za mafasiki, basi hao ndio watakuwa warithi wa ardhi, sio watu wema. Na warithi wa wote huwa yule aliye baada ya wote.

Tena, ifikiriwe pia kwamba kwa kuwa Mwenyezi Mungu Alikwisha fahamisha kuwa Mimi Nitaendelea kuleta makhalifa katika umati huu jinsi Nilivyoleta makhalifa baada ya Musa, basi ilipaswa kuangalia kuwa baada ya kifo cha Musa, Mwenyezi Mungu Alifanyaje. Je Akatuma makhalifa mpaka miaka thelathini tu, au Akairefusha silsila hii hadi

[93] Tafsiri: Na hakika Tuliandika baada ya ukumbusho ya kwamba ardhi hii watairithi watumishi wangu walio wema, Sura Al-Ambiyaa, 21:106. Mwenezi.

miaka elfu moja na mia nne? Na kwa kuwa fadhili za Mwenyezi Mungu zilikuwa nyingi zaidi juu ya Nabii wetu s.a.w. kuliko zilizokuwa juu ya Musaas, kwani Mwenyewe Alisema وَكَانَ فَضْلُ اللهِ عَلَيْكَ عَظِيمًا[94] na kadhalika kuuhusu umati huu Akanena: كُنْتُمْ خَيْرَ أُمَّةٍ أُخْرِجَتْ لِلنَّاسِ[95] basi yawezekanaje kuwa silsila ya makhalifa wa Hadhrat Musa ifululize hadi miaka elfu moja na mia nne, lakini hapa ukhalfia ukome hadi miaka thelathini pekee. Tena kama umati huu ni mtupu, hauna nuru za kiroho za Ukhalifa kwa kudumu, basi ina maana gani aya hii أُخْرِجَتْ لِلنَّاسِ[96] aieleze mtu yeyote. Kuna methali mashuhuri: 'Yeye hajijui, atawezaje kuongoza!' Kama makusudio yenyewe ni kuubakiza umati huu kuwa kipofu daima, na lengo lenyewe ni kuiweka dini hii katika hali ya kufa, basi

[94] Tafsiri: Na fadhili za Mwenyezi Mungu zilizo juu yako ni kubwa. Sura An-Nisaa, 4:114. Mwenezi.

[95] Tafsiri: Ninyi ni umati bora mliotolewa kwa ajili ya watu, Sura Aali Imraan, 3:111. Mwenezi.

[96] Tafsiri: Ninyi ni umati bora mliotolewa kwa ajili ya watu, Sura Aali Imraan, 3:111. Mwenezi.

ina maana gani kusema kuwa ninyi ni bora kulilo wote na mmetolewa kwa wema na mwongozo wa watu? Je kipofu atamwongoza kipofu? Basi, Enyi watu mnaoitwa Waislamu, fikirini kwa ajili ya Mungu kwamba aya hii inamaanisha hii tu kuwa daima mpaka Kiama mtakuwa na uzima wa kiroho na macho ya kiroho, na wafuasi wa dini zingine watachukua kutoka kwenu mwanga, na huu uzima wa kiroho na haya macho ya kiroho ambayo yana kipawa cha kuwaita wafuasi wa dini nyingine, hicho ndicho kitu kiitwacho Ukhalifa. Basi, kwa nini mwasema kuwa Ukhalifa baada ya kubaki kwa miaka thelathini ukaadimika kabisa. Mcheni Mungu, Mcheni Mungu, Mcheni Mungu.

Sasa kumbukeni kuwa ingawaje ndani ya Kurani Tukufu kuna aya sufufu zitoazo bishara za Ukhalifa wa kudumu ndani ya Umati huu na Hadithi nazo zipo tele, lakini kuandika kiasi hiki kwatosha kwa watu wanaozipokea kweli zilizothibitika kwa

kuzifahamu ni utajiri mkubwa sana. Na hakuna ukorofi mkubwa zaidi kuliko kuifikiria Islam kuwa dini iliyokufa, na baraka zake zifikiriwe kukoma mpaka kwa karne ya kwanza tu. Je, kile Kitabu kinachofungua mlango wa neema za kudumu, chaweza kufundisha la kuvunja moyo kuwa hakuna baraka yoyote na Ukhalifa wowote unaoendelea bali yote yameishia nyuma.

Manabii hawaji katika umati huu. Sasa, kama makhalifa pia wasije na wasionyesha mara kwa mara miujiza ya uzima wa Kiroho, basi hapo itaishia hali ya kiroho ya Islam, na dini kama hii inawezaje kulingana na shani ya kiroho na jalali ya dini ya Musa ambamo maelfu ya makhalifa waliendelea kuzaliwa mpaka miaka elfu moja na mia nne. Ni masikitiko kuwa wapinzani wetu hawafikirii kabisa kwamba katika hali hii Islam inakuwa duni sana kiroho na Mtume[saw], Mungu Apishe mbali, hathibitiki kuwa mkubwa, wala Kurani nayo haithibitiki kuwa

Kitabu kinachoathiri kwa nguvu sana kwa nuru yake. Na hapo kauli hii kuwa umati huu ni bora kuliko nyimati zote na ni wenye kuzinufaisha nyimati zingine kiroho kwa kudumu, na Kurani hii kwa kulingana na vitabu vyote vya Mungu ni kamilifu timilifu katika sifa zake na athari zake na kadhalika, na Mtume huyu s.a.w. ni mkamilifu mtimilifu kuliko mitume wote katika nguvu zake takatifu na ukamilifu wa hulka, itakuwa ni madai ya kipuzi yasiyo na maana, yasiyothibitika. Tena uharibifu mkubwa utalazimika kwamba ile sehemu ya mafundisho ya Kurani inayotaka kumfanya mtu afanane na manabii katika nuru za kiroho na sifa kamilifu, itafikiriwa kuwa imetanguka kwa kudumu. Kwani, kama umati hauna uwezo wenyewe wa kujipatia sifa kamilifu za kibatini za Ukhalifa, basi mafundisho kama hayo yanayosisitiza kupata daraja hii yatakuwa ni bure. Kwa hakika swali hili pekee kuwa je Islam sasa ni dini iliyokufa kwa kudumu

ambamo hawazaliwi watu ambao karama zao ni badala ya miujiza na ambao ufunuo wao ni badala ya wahyi, linatetemesha mwili licha ya Mwislamu, Mungu Apishe mbali, awe na imani pia kama hii. Mwenyezi Mungu Awaongoze wanaotawaliwa na fikara hizi potofu.

Sasa, ilipokwisha thibitika kutokana na Kurani Tukufu kuwa silsila ya Ukhalifa wa kudumu imewekwa ndani ya umati huu uliorehemiwa kama ilivyokuwa imewekwa katika sheria ya Musa — ni tofauti ya neno tu kuwa manabii wakafika kuisaidia dini ya Musa, lakini sasa Muhaddathina wanafika — basi uthibitisho huu unalazimisha kukubali kuwa jinsi katika zama za mwisho za sheria ya Hadhrat Musa akaja nabii mmoja aliyeitwa jina Isa katika wakati ambapo hali ya khulka za Wayahudi iliharibika kabisa na wakaenda mbali kabisa na ucha Mungu wa kweli, uaiminifu, huruma ya kaumu, umoja na hofu ya Mungu, na kikomo cha elimu na fikara

yao kikawa ni maneno matupu na kushikamana na maneno tu, na kidunia wakakawa wanyonge na dhalili, ndivyo inavyolazima kutokea katika umati huu pia Muhaddath mmoja afananaye na nabiii huyo, katika wakati ambapo umati huu uwe umeharibika kama Wayahudi walivyoharibika katika zama za Hadhrat Isa[as]. Na inapoangaliwa kwa makini na kufikiriwa kwa mtazamo wa uchunguzi, yajulikana waziwazi kwamba zama ambamo mithili ya Hadhrat Masihi[as] anatakiwa kutokea katika umati huu pia, kwa sababu ya kufanana kitimilifu kikamilifu kwa silsila ya makhalifa wa Musa[as] na makhalifa wa Muhammad[saw], ni zama hizi hizi tuliomo humu, kwani muda uliokuwa baina ya Hadhrat Musa an Hadhrat Isa ulikuwa miaka elfu moja na mia nne takriban, na sasa pia baada ya Nabii wetu s.a.w. mpaka wakati huu ndiyo karne ya kumi na nne. Na umati wa Hadhrat Musa uliharibika sana katika karne ya kumi na nne hata kwamba ucha Mungu na

unyofu ukapotea moja kwa moja na wanazuoni wa Wayahudi wakashughulikia hitilafu zisizo za haki na magomvi ya kinafsi, ufasiki na uovu ukaenea baina yao na hali yao ya kidunia nayo ikawa mbovu sana. Kadhalika ndiyo hali ya umati huu katika zama hizi. Matukio tunayoona kwa macho yetu yanashuhudia kwa uwazi kuwa kwa kweli umati huu na wanazuoni wa umati huu wamekanyaga katika nyayo za Wayahudi waliokuwa katika zama za Hadhrat Masihi[as]. Na si tu kwamba wakafanana na Wayahudi wa zama zile katika kuondokewa na unyofu, ucha Mungu, hali ya kiroho na utambuzi wa hakika, bali vivyo hivyo wakasibiwa na maafa ya kidunia pia yaliyokuwa katika zama zile. Na jinsi wafalme wa Kirumi walivyoziangamiza tawala zao na wakawa kama ilivyoelezwa katika ضُرِبَتْ عَلَيْهِمُ الذِّلَّةُ وَالْمَسْكَنَةُ[97] na Wayahudi wakijikuta wanyonge wasio

[97] Tafsiri: Ikapigwa juu yao dhila na umaskini, Sura Al-Baqara, 2:62. Mwenezi.

na msaidizi wakamsubiri Masihi ambaye aje akiwa mfalme na awaue Warumi, kwani mwishoni mwa Torati ahadi hii ilitolewa, ndivyo kaumu ya Waislamu inavyoonekana mara nyingi kuangukia maafa. Kama wanayo sehemu fulani ya utawala wao, huo umedhoofishwa na unafiki wa mawaziri na uhaini wa wafanyakazi na uzembe wa wafalme na uvivu wao na ujinga wao, ukosefu wa ujuzi wao, anasa zao na starehe zao, hata utawala huo unaonekana karibu kwisha. Watu hao walikuwa wanamsubiri kama Wayahudi kwamba Masihi atateremka kwa kuwasaidia kwa jalali kubwa kama wafalme.

Sasa macho yale yawezayo kuona, na nyoyo ziwezazo kufanya uadilifu, na akili iwezayo kufikiria viangalie hapa na kupima na kuzingatia kuwa hali hii na hali ile, zote mbili, zinafanana au hapana. Hebu, achilieni mbali kwa muda kidogo habari za matabiri, tazameni mkiwa kama mhakiki kuwa je hali za Waislamu wa zama hizi na Wayahudi wa

zama za Hadhrat Masihi zafanana jinsi kiatu kimoja kifananavyo na kiatu cha pili au hapana. Zisomeni Injili kwa makini na zingatieni kuwa habari za masheikh na wanasheria wa Wayahudi alizoandika Hadhrat Masihi[as] na kudhihirisha hiana zao, je hizo zinapatikana ndani ya masheikh wa Waislamu au hapana? Je ni kweli ama hapana kuwa masheikh wetu pia kama wanasheria wa Wayahudi wanashughulikia usiku na mchana katika magomvi yasiyo na maana, na wameondokewa na ile hali ya kiroho kabisa, na wanajibidiisha kuwakufurisha wengine na wenyewe hawajui Islam ni kitu gani. Wanatoa nasaha ambazo wao wenyewe hawazitekelezi. Na ili kujipatia riziki wanashika kazi ya kutoa mawaidha na kwenda mbali sana, na kwa kusema maneno yao yasiyo na msingi wanawafurahisha watu na kula mali ya haramu. Na hawako nyuma kuliko Wayahudi katika ulaghai, udhanganyifu na uayari. Kadhalika ndiyo hali ya waipandao dunia, kwani wengi wao

wanaona kuwa kila hiana na uwongo ni halali kabisa kwa kujichumia riziki. Wanaoitwa watemi wenye tawala ndogo ndogo, hao wameangamizwa na anasa zao. Miongoni mwao wapo wanaokunywa kileo kama maji, hawakirihi katu uzinzi, hofu ya Mungu haiwasogelei katika sehemu yoyote ya mchana wala usiku. Sasa shikeni mkononi historia ya Wayahudi na kuona kuwa hao Waislamu katika kuangamia kidini na kidunia wanafanana sana mno na Wayahudi. Kulikuwa na utabiri ndani ya Torati kuwahusu Wayahudi kwamba maadamu haji Shilo, ufalme wa Wayahudi hautatoweka. Muradi wa Shilo ulikuwa ni Hadhrat Masihi. Na kweli ikawa hivyo kwamba muda kiduchu kabla ya Hadhrat Masihi kuzaliwa tawala ndogo ndogo za Wayahudi zilishambuliwa vikali na Serikali ya Kirumi. Na kwa kuwa Wayahudi kama Waislamu wa zama hizi walikuwa wamedhoofika kwa sababu ya unafiki baina yao na magomvi ya kile siku na uzembe na

ujahili, na hali ya ndani mwao ilikuwa inawatolea habari ya fali mbaya, hivyo Wayahudi kabla kidogo ya zama za Hadhrat Masihi wakajisalimisha kwa serikali ya Rumi. Na kwa sababu ya kushabihiana kwa silsila hizi mbili, katika umati huu pia Shilo mmoja alilazimika kuja katika zama hasa za maangamio ya kidini na ya kidunia.

Na kwa hakika Kurani Tukufu pia ilitoa utabiri kama huo kuhusiana na zama hizi za Waislamu, zilizofanana na zama za Hadhrat Masihi kwa jiha ya muda na mengineyo, kama isemavyo:

مِّنْ كُلِّ حَدَبٍ يَّنْسِلُوْنَ[98]

Aya hii yamaanisha hii tu kuwa kaumu ya Wakristo walio kundi la Yajuja na Majuja toka kila mahali pa juu watakwenda mbio mbio kuelekea nchi za Kiislamu, nao watakuwa washindi, na wataendelea kuzibana nchi za Kiislamu mpaka serikali ya Kiislamu itabaki ya jina tu kama ilivyo siku hizi.

[98] Sura Al-Ambiyaa, 21:97. Mwenezi.

Angalieni jinsi matukio yanavyolingana kwamba zama za shida za Islam na maangamio ya kidini na ya kidunia ya Waislamu zimeunganaje na zile zama za Wayahudi zilizokuwa wakati wa Hadhrat Masihi. Kisha angalieni utabiri wa Kurani kuhusu unyonge wa utawala wa Kiislamu na ushindi wa wapinzani ulilinganaje na ule utabiri uliofanywa ndani ya Torati kuhusu kuharibika kwa utawala wa Kiisraeli. Naam, katika bishara ya Mujaddidina kuna tafauti ya namna ya kueleza tu baina ya utabiri wa Torati na utabiri wa Kurani. Yaani, katika Torati, wakati wa kuvunjika nguvu ya Kiisraeli na kutoweka kwa fimbo — iliyomaanisha kuharibika kwa utawala — ilitolewa bishara ya ujaji wa Shilo, lakini ndani ya Kurani, wakati wa kudhoofika nguvu ya Kiislamu na kuibuka mawimbi ya fitina — iliyomaanisha udajali wa wahubiri wa Kikristo — ilitolewa bishara ya kupigwa parapanda. Kupigwa parapanda siyo maana yake kutokea Kiama, kwani tangu yazuke

mawimbi ya fitina za Wakristo sasa miaka mia imeishapita lakini Kiama hakikutokea, bali muradi wake ni kupiga parapanda kwa kutuma Mahdi na Mujaddidi na kuwapulizia roho ya uzima wafu wa kiupotevu, kwani parapanda haipigwi tu kwa kuhuisha na kufisha kimwili, bali hata kuhuishwa kiroho na kufishwa pia hutokana na kupiga parapanda. Na kama ambavyo ndani ya Kurani kupigwa parapanda muradi wake ni kumtuma Mujadidi ili avunje nguvu ya Wakristo, ndivyo mawimbi ya fitina yanavyomaanisha ule udajali ulioelezwa ndani ya Hadithi kwa jina dajali aliyeahidiwa. Na Mwenyezi Mungu hakutaja ndani ya Kurani dajali aliyeahidiwa wala Masihi Mau'udi kama walivyotajwa ndani ya Hadithi, bali badala yake mambo yaliyojaa fitina za dajali wa Wakristo yameelezwa. Ndani ya مِنْ كُلِّ حَدَبٍ يَّنْسِلُوْنَ[99] pia imeashiriwa habari hii. Kadhalika katika Kurani

[99] Sura Al-Ambiyaa, 21:97. Mwenezi.

Tukufu hakutajwa Mujadidi ajaye kwa neno Masihi Mau'udi, bali kwa neno 'kupigwa parapanda' imeashiriwa kwenye ujaji wake, ili ijulikane kuwa Masihi Mau'udi hatadhihiri akiwa na silaha za kiardhi na kidunia bali heshima yake na utukufu wake utategemea kupigwa parapanda ya kimbingu, na atawavutia watu kwa nguvu ya maneno ya hekima na ishara za kimbingu kwenye haki na ukweli, kwani atafika katika wakati wa fitina za kiakili, si katika wakati wa fitina za upanga. Na hakika yenyewe ni kuwa Mwenyezi Mungu hutuma nabii na mujadidi kuafikiana na namna ya fitina iliyopo. Basi, jinsi ambavyo katika wakati wa Hadhrat Isa[as] nguvu zote za Wayahudi zilikuwa zimetwaliwa, na mkononi mwao mlikuwa hamna kitu isipokuwa ujanja, ulaghai na maneno matupu, na kwa sababu ya maovu yao na uongozi mbovu wakaja wenyewe chini ya utawala wa Kirumu, Warumi hawakukosea kuwatawala, hali hiyo ndiyo iliyoandikwa ndani

ya Kurani Tukufu kuhusiana na zama za Masihi Mau'udi. Mathalan, hali ya Waislamu wabovu wa India ni kuwa akitokea Muslih — mrekebeshaji — hawawezi kumwasi kwa upanga, kwani hawanazo panga. Na Waingereza wakachukua utawala wa Delhi hivi hivi tu jinsi Serikali ya Kirumi ilivyochukua utawala wa Wayahudi, yaani kwa sababu ya maovu ya wafalme tu na utovu wa kipawa.Waingereza hawakukosea kuchukua utawala hata kwamba wainuliwe upanga, bali hapa kauli hii inaafikiana na hali hii: 'Kilichotusibu, kimetoka kwetu'. Ndiyo sababu Mujadidi wa Karne hii amekuja akiwa na tabia za Hadhrat Masihi, na kwa kushabihihana naye sana mno akaitwa Masihi Mau'udi, na jina hili si la kubuni, bali kwa kuafikiana na hali zilizopo jina hili lilihitajika.

Na ikumbukwe kuwa ndani ya Kurani Tukufu, mahala fulani neno Rusul[100] pia limetumika kuashiria

[100] Sura Al-Mursalaat, 77:12. Mwenezi.

kwenye Masihi Mau'udi. Lakini, swali ni hili kuwa kwa nini ndani ya Kurani Tukufu habari hii haikutajwa kwa maneno yaliyotumika katika Hadithi. Jawabu lake ni kuwa ili wasomaji wasifahamu vibaya na kufikiria kuwa Masihi Mau'udi ndiye Hadhrat Isa[as] hasa aliye kuwa ameteremshiwa Injili, na kwamba dajali ndiye mharibifu fulani mahususi. Basi Mwenyezi Mungu ndani ya Kurani Tukufu Ameondolea mbali shaka zote hizo. Kadhalika, kwanza Akatoa habari ya kifo cha Hadhrat Isa[as] kwa uwazi kabisa kama ilivyo dhahiri kutokana na aya:

فَلَمَّا تَوَفَّيْتَنِيْ كُنْتَ اَنْتَ الرَّقِيْبَ عَلَيْهِمْ [101]

na kisha Akadhihirisha pia kuwa Mtume wetu s.a.w. ni Khatamul Ambiyaa kama Alivyosema:

وَلٰكِنْ رَّسُوْلَ اللّٰهِ وَخَاتَمَ النَّبِيّٖنَ [102]

kisha kwa kutaja maasi mengi ya Wayahudi mahali

---

101 Na Uliponifisha Ukawa Mchungaji juu yao. Sura Al-Maaida, 5:118. Mwenezi.

102 Bali yeye ni Mtume wa Mungu nani Khatamun Nabiyyina. Sura Al-Ahzaab, 33:41. Mwenezi.

mabalimbali Akafululiza kuashiria kwamba hiyo itakuwa ni hali ya mwisho ya Waislamu na wanazuoni wa Waislamu. Kisha Akaeleza kuwa katika zama za mwisho Wakristo watakuwa na nguvu, na kwa mikono yao machafuko ya aina aina yataenea, na kutoka kila upande mawimbi ya fitina yatazuka. Watakuja mbio mbio toka kila mahali pa juu, yaani kwa njia yoyote watadhihirisha nguvu yao na utukufu wao na upeo wao. Watakuwa juu kabisa katika nguvu ya dhahiri na utawala, na serikali na vijiserikali vidogo vidogo vitadhoofika mbele yao, nao watakuwa juu kabisa katika elimu na fani, nao watavumbua elimu na fani na kufanyiza sanaa za nadra na za ajabu. Watakuwa na mbinu na tadbiri na usimamizi bora wa hali ya juu. Katika mambo muhimu ya kidunia na kujipatia hayo watakuwa na hima kubwa, na katika juhudi na bidii za kueneza dini yao pia watawapita wote. Kadhalika katika mambo yao ya jamii, biashara, maendeleo ya kilimo,

ilmuradi katika kila jambo watalipita kila taifa. Hiyo ndiyo maana ya مِنْ كُلِّ حَدَبٍ يَنْسِلُونَ[103] kwani حَدَب kwa fat'ha ya daal yamaanisha mahali palipoinuka na nasal maana yake kuwapita wengine na pia kwenda mbio. Yaani, watalipita kila taifa katika kila jambo lihusikanalo na heshima na uzuri wa hali ya juu sana. Na hiyo ndiyo alama kubwa ya taifa hili la mwisho liitwalo Yajuja na Majuja, na hiyo ndiyo alama ya kundi lile la mapadre lenye fitina linaloitwa Dajali aliyeahidiwa. Na kwa kuwa Hadab yamaanisha ardhi iliyoinuka, basi ndani yake mna dokezo kuwa maendeleo yote ya kidunia wataipata, lakini maendeleo ya kimbingu — ya kiroho — hawatakuwa na hadhi yake. Hapa panathibitika kuwa taifa hili la Yajuja na Majuja laitwa jina Yajuja na Majuja kwa sababu ya maendeleo yao ya hali ya juu kiutawala, na miongoni mwa taifa hili wapo pia

[103] Watakuja mbio mbio kutoka kila mahali pa juu. Sura Al-Ambiyaa, 21:97. Mwenezi.

wale watu waliofikisha juhudi zao za kutapakaza upotevu mpaka mwisho na wakaitwa Dajali Akbar — Dajali Mkuu. Na Mwenyezi Mungu Akitaja upotevu wa hali ya juu Akasema kuwa wakati huo itapulizwa ndani ya parapanda na madhehebu yote yatakusanywa mahali pamoja. Baada ya aya hizi, zipo habari za Jahanamu, na hizo habari ni mbali sawa na njia ya Kurani Tukufu ya kueleza, kwani ni njia ya kawaida ya Kurani Tukufu kuwa wakati mwingine ikitaja tukio fulani la kidunia inataja pia habari za Akhera kwa sababu fulani, na wenye kutalii Kurani Tukufu kwa makini wanaielewa sana. Sehemu ya tatu ya mazungumzo yetu ilikuwa kwamba ni dalili gani ya kuwa mimi ndimi Masihi Mau'udi aliyetajwa kwa njia mbalimbali ndani ya Kurani na Hadithi. Nionavyo, haina haja ya kurefusha kuandika dalili za sehemu hii. Katika kijitabu hiki hiki tumeisha thibitisha kuwa hakuna budi kuja kwa mtu mmoja kwa jina la Masihi[as]

kutoka katika umati huu. Kwa nini yalazimu? Kwa sababu tatu.

Kwanza, kufanana kitimilifu kikamilifu kwa Nabii wetu s.a.w. na Hadhrat Musa[as] kunakofahamika kutokana na aya كَمَآ اَرْسَلْنَآ اِلٰى فِرْعَوْنَ رَسُوْلًا[104] kunalihitaji jambo hili. Kwani aya:

اِنَّآ اَرْسَلْنَآ اِلَيْكُمْ رَسُوْلًا شَاهِدًا عَلَيْكُمْ كَمَآ اَرْسَلْنَآ اِلٰى فِرْعَوْنَ رَسُوْلًا[105]

yaeleza bayana kuwa jinsi Hadhrat Musa alivyokuwa shahidi juu ya mema na maovu ya umati wake, ndivyo alivyo Nabii wetu s.a.w. Lakini ushuhuda huu haukuwezekana kwa kudumu kwa Hadhrat Musa isipokuwa kwa sababu ya Ukhalifa. Yaani, Mwenyezi Mungu, ili kutimiza hoja, Akaweka silsila ya kufululiza makhalifa baada ya Hadhrat Musa kwa miaka 1400, ambao kwa hakika wakaja kuitilia nguvu sheria ya Hadhrat Musa ili Mwenyezi

---

104 Kama Tulivyompeleka Mtume kwa Firauni. Sura Al-Muzzammil, 73:16. Mwenezi.

105 Tumewatumieni Mtume aliye shahidi juu yenu, kama Tulivyompeleka Mtume kwa Firauni. Sura Al-Muzzammil, 73:16. Mwenezi.

Mungu kwa njia ya makhalifa hao Akamilishe silsila ya ushuhuda wa Hadhrat Musa, naye aweze kustahili siku ya Kiama kuota ushahidi kuhusiana na wana wa Israeli wote mbele ya Mwenyezi Mungu. Kadhalika Mwenyezi Mungu Akamfanya Nabii wetu s.a.w. kuwa shahidi kwa watu wote wa umati wa Kiislamu, na Akasema إِنَّآ أَرْسَلْنَآ إِلَيْكُمْ رَسُولًا شَاهِدًا عَلَيْكُمْ[106] na Akasema وَجِئْنَا بِكَ عَلَىٰ هَٰٓؤُلَآءِ شَهِيدًا[107] Lakini, ni dhihiri kuwa Mtume[saw] akawa ndani ya umati wake kwa miaka ishirini na mitatu, basi anawezaje kuwa shahidi kwa kudumu juu ya umati wake? Jibu lake ni kwamba kwa njia ya Ukhalifa. Yaani, sawa na mfano wa Musa[as], Mwenyezi Mungu Akaweka makhalfia kwa ajili ya Mtume[saw] pia mpaka siku ya Kiama, na ushuhuda wa makhalifa ukachukuliwa kuwa ushuhuda wa Mtume[saw]. Kwa njia hii, madhumuni

---

106 Tumewatumieni Mtume aliye shahidi juu yenu. Sura Al-Muzzammil, 73:16. Mwenezi.

107 Tutakuleta wewe uwe shahidi juu ya hawa. Sura An-Nisaa, 4:42. Mwenezi.

ya aya إِنَّآ أَرْسَلْنَآ إِلَيْكُمْ رَسُولًا شَاهِدًا عَلَيْكُمْ[108] yakawa sawasawa kwa kila jiha. Gharadhi, itikadi ya ushuhuda wa daima unaofululiza kuthibitika kutokana na Kurani na imekubaliwa na Waislamu wote yathibitika hapo tu ambapo Ukhalifa wa kudumu ukubaliwe. Na hili lahakikisha utashi wetu. Basi, na utafakari!

Pili: Kufanana kitimilifu kikamilifu kwa Ukhalifa wa Muhammad[saw] na Ukhalifa wa Musa[as] kunalazimisha ujaji wa Masihi Mau'udi, kama inavyofahamika kutokana na aya ifuatayo, yaani aya:

وَعَدَ اللّٰهُ الَّذِيْنَ اٰمَنُوْا مِنْكُمْ وَعَمِلُوا الصّٰلِحٰتِ لَيَسْتَخْلِفَنَّهُمْ فِي الْاَرْضِ
كَمَا اسْتَخْلَفَ الَّذِيْنَ مِنْ قَبْلِهِمْ[109]

yaeleza waziwazi kuwa Mujadidi mmoja kwa jina la Hadhrat Masihi hakuna budi kuja katika karne ya

---

108 Tumewatumieni Mtume aliye shahidi juu yenu. Sura Al-Muzzammil 73:16. Mwenezi.

109 Tafsiri: Mwenyezi Mungu Amewaahidi wale walioamini miongoni mwenu na kufanaya vitendo vizuri, bila shaka Atawafanaya makhalifa katika ardhi kama Alivyowafanya makhalifa wale wa kabla yao. Sura An-Nuur, 24:56. Mwenezi.

kumi na nne, kwani Ukhalfia wa Muhammadsaw unaweza kufanana na Ukhalifa wa Musa kikamilifu kitimilifu hapo tu ambapo zama zao za awali na za mwisho zinashabihiana sana mno. Na kufanana kwa zama za mwisho kulikuwa katika mambo mawili. La kwanza, hali ya umati kuwa mbovu, ustawi wa kidunia kufifia, kutokea tofauti katika uaminifu wa kidunia na unyofu na ucha Mungu. Pili, kuzaliwa katika zama kama hizi Mujadidi ajaye kwa jina la Masihi Mau'udi na kurudisha imani katika hali ya awali. Sasa ile alama ya kwanza siyo tu wanaikubali ndugu zetu Waislamu, bali wanajionea wenyewe kwa macho yao uharibifu wao na ustawi wa taifa jingine ambalo linaichukulia dini yao kuwa hakiri na dhalili kama ambavyo Majusi baada ya kuwashinda Wayahudi katika zama za Hadhrat Masihi waliwafahamu kuwa hakiri na dhalili. Na wanaona pia hali ya ndani ya wanazuoni wa Islam, na Waislamu wa kawaida wanaoshughulikia dunia

siyo afadhali kuliko hali za Wayahudi, bali ni mbovu zaidi mara kumi. Tusomapo katika juzuu ya kwanza ya Kurani zile aya zinazohusikana na masheikh wa Wayahudi kuwa mnawasihi watu kufanya wema na mambo ya heri, lakini mwajisahau nafsi zenu, na hamwachi nafasi ya kuwasumbua ndugu zenu, na mmeshughulikia katika tamaa za namna namna na maovu, ufuska, kula njama na kutafuta manufaa ya dunia kwa njia za ulaghai, hapo mara moyo unasema kuwa alama hizi zote zinapatikana ndani ya masheikh wetu wengi.

Sasa, ikiwa kupatikana katika zama hizi kwa alama mojawapo ya alama za lazima wameisha kubali ndugu zetu, basi kuhepa kukubali alama ya pili ndiyo sawasawa na mtu kusema kuwa jua bila shaka limeishachomoza, lakini mchana bado. Kwa vyovyote, mwadilifu mwenye busara hana budi kukubali kwamba yathibitika baada ya kuzifikiria aya za Kurani kwa makini kuwa silsila ya Ukhalifa

wa Muhammadsaw inastahili kuafikiana kabisa na silsila ya Ukhalifa wa Musa kama inavyofahamika kutokana na Kama. Na ikiwa kuafikiani ni kikamilifu, basi ndani ya umati huu pia katika zama za mwisho zilizo zama za ukaribu wa Kiama, anatakiwa kuja Khalifa mfano wa Hadhrat Isa ambaye atimize hoja si kwa upanga bali kwa mafundisho ya kiroho na baraka. Na kwa kuwa Hadhrat Masihi akaja miaka 1400 baada ya Musa, basi yalazimu kukubali kudhihiri Masihi Mau'udi katika zama hizi, na Mwenyezi Mugnu Hafanyi kinyume na ahadi zake. Sasa yapasa kuangalia kuwa ni watu wangapi waliodai kuwa Masihi Mau'udi katika zama hizi. Hata ikifikiriwa kwamba, mathalan, watu kumi wamedai katika zama hizi, basi hakuna budi mmojawapo miongoni mwa hao kumi atakuwa mkweli na Masihi Mau'udi, kwani alama zilizowekwa na Mwenyezi Mungu zahitaji awepo mkweli. Lakini katika hali ambapo kutoka miongoni

mwa Waislamu milioni mia mbili waishio nchini Shamu, Uarabu, Iraki, Misri, India na kadhalika, mtu mmoja tu miongoni mwa Waislamu amedai kuwa Masihi Mau'udi katika zama hizi zilimotimia alama, ambazo ni zama za kudhihiri Masihi Mau'udi sawa na Kitabu cha Mungu na Hadithi, basi kumkadhibisha mdai kama huyu aliyedhihiri katika wakati wake ndiyo kuikadhibisha bishara yenyewe. Kadri inavyothibitika kuja kwa Masihi Mau'udi mwanzoni mwa karne ya kumi na nne kutokana na Hadithi na Kurani na kashfi za mawalii, haina haja kueleza. Tena kuyakataa madai yaliyo sawasawa na mahali pake kunatetemesha mwili wa mtu mcha Mungu. Ilmuradi, dalili ya kwanza ya ukweli wangu ni kudai kwangu katika wakati hasa aliouteua Bwana wa mitume wote s.a.w., Kurani Tukufu na kashfi za mawalii. Kwa kuwa Nabii wetu s.a.w. ni Nabii wa zama za mwisho, kisha miaka elfu moja mia tatu imekwishapita baada ya Nabii wa zama za mwisho,

basi fikirieni ile Hadithi ambamo madaraja saba ya mimbari yaliyoonwa katika ruya yalielezwa kuwa ni miaka elfu saba ya dunia. Fikirieni kwa makini kuwa je zama hizi sawa na Hadithi lazima ni kwa ajili ya Masihi Mau‘udi au hapana! Tena zingatieni pia Hadithi

الآيات بعد المأتين[110]

ambayo wanazuoni wamefahamu kuwa alama kubwa za Kiama zitaanzia tangu karne ya kumi na tatu. Kwani, kama ‘alama’ zamaanisha alama ndogo, hapo sharti ya ‘baada ya miaka mia mbili’ haina maana. Hata uwepo wa Nabii wetu s.a.w. wenyewe ni miongoni mwa alama za Kiama. Sasa kama Hadithi ifasiriwe kuwa baada ya miaka mia mbili alama kubwa zitaanza, hiyo itakuwa si sawa kabisa, kwani alama yoyote haikuanzia baada ya miaka mia mbili. Kwa hiyo, wanazuoni wamechukua ile miaka mia mbili iliyo baada ya elfu, yaani miaka elfu

---

[110] Tafsiri: Alama baada ya miaka mia mbili. Mwenezi.

moja na mia mbili. Maelezo ya wanazuoni ndiyo barabara, kwani hamna shaka kuwa fitina kubwa kubwa zimedhihiri katika karne ya kumi na tatu na tufani ya Udajali ikatapakaa ndani ya karne hii hii, na tamasha la مِنۡ كُلِّ حَدَبٍ يَّنۡسِلُوۡنَ nalo likashuhudiwa katika karne hii. Mamia ya serikali ndogo ndogo za Kiislamu zikaangamia na Wakristo wakapata adhama kubwa.

Na sehemu hii ya tatu inayotakiwa kujadiliwa ni kuwa kama kwa kweli Masihi Mau'udi yeyote anatakiwa kuja ndani ya umati huu, basi ni dalili gani ya kuhakikisha kuwa Masihi huyo ndiye mimi? Tumekwisha andika sasa hivi baadhi ya dalili zielekazo kwenye ukweli ulivyo; hizo haina haja kuzirudia. Lakini zikihitajika dalili za aina mahususi, basi mwulizaji apaswa kusubiri kidogo ili Mwenyezi Mungu Mwenyewe Aziteremshe dalili za kumsaidia mja wake. Hakika yenyewe ni kuwa madai kama hayo hayawezi kuthibitishwa kikamilifu kwa hoja

za kiakili na kimaandiko pekee mpaka zithibitike baraka za mdai kwa misaada ya kimbingu, na hiyo ndiyo suna ya Mwenyezi Mungu tangu kale kuhusiana na manabii a.s. Mathalan, ingawaje kumhusu Seyidna na Maulana Nabii wetu s.a.w. zilitolewa bishara ndani ya vitabu vya zamani, tena Mtume[saw] mwenyewe alifika katika zama zilizohitaji ujaji wa mtume mmoja mtukufu sana, hata hivyo Mwenyezi Mungu hakutosheka na bishara za zamani wala Hakufikiria kuwa baada ya mambo ya kuelekeza kwenye ukweli wake yanatosha, bali ishara sufufu za kumsadikisha Nabii huyu mtukufu Akaziteremsha, hata kwamba ukweli wa nabii huyu mkarimu akabainika na nuru ya ukweli ikang'ara kama jua.

Kadhalika yapasa ifahamike kuwa kama mimi nimetoka kwa Mwenyezi Mungu, na ni mkweli katika kauli yangu, basi Mwenyezi Mungu Atadhihirisha ukweli wangu kwa misaada yake mahusus na

kuibainishia dunia kuwa mimi nimetoka Kwake, siyo kutokana na hila zangu. Kisha ukithibitika ukweli wangu kwa njia ya ishara za kimbingu, haiwezi kubaki sababu yoyote ya kukataa. Kwani ishara za kimbingu ni njia ambayo ukathibitika kwayo Unabii mkubwa mkubwa, ukathibitika Utume mkubwa mkubwa, vikathibitika Vitabu kuwa Neno la Mungu, basi kwa nini isiweze kuthibitika kuwa mithili ya Masihi! Ilmuradi, namna Mwenyezi Mungu Alivyoendelea kuhakikisha ukweli wa waja wake wakweli, ndivyo kwa njia iyo hiyo Atakavyohakikisha ukweli wangu pia. Yapasa kuangaliwa kuwa Wayahudi walipatwa na shida nyingi kiasi gani katika kuamini Unabii wa Hadhrat Masihi[as]. Ilikuwa imeandikwa katika vitabu vya zamani kuwa Isa atakuja akiwa mfalme, lakini Masihi akazaliwa akiwa maskini. Vitabu vya zamani viliandika kwamba kwa ujaji wake siku za ustawi wa Wayahudi zitarudi tena. Wayahudi wakadhani kuwa yeye atapigana na ufalme wa Rumi na

kuimarisha ufalme wa Israeli, lakini mambo yakawa kinyume na Wayahudi wakazidiwa taabu na dhilla. Kadhalika ilikuwa imeandikwa kuwa yeye hatakuja mpaka atakapoisha kuja nabii Eliya. Basi Wayahudi walikuwa wakisubiri lini atashuka Eliya kutoka mbinguni, lakini Eliya hakushuka, na Hadhrat Isa[as] akadai kuwa mimi ndimi Masihi Mau'udi. Na akasema pia kuwa nabii Yahya ndiye Eliya. Lakini maelezo hayo hayakuwapendeza Wayahudi, bali hao walimsubiri Eliya kushuka kama siku hizi Waislamu wanavyomsubiri Hhadhrat Isa ashuke. Lakini juu ya vizingiti hivyo vyote vilivyokuwa kwa hakika vizingiti vikubwa sana, Mwenyezi Mungu Hakumpoteza bure nabii wake mkweli na Akahakikisha kwa ishara nyingi sana kuwa yu mkweli, jambo ambalo likalazimisha kufikia natija kuwa yu Masihi Mau'udi na hatimaye akakubaliwa kuwa mkweli.

Basi, wapenzi, fahamuni kwa yakini kwamba kwa

kudhihirisha ukweli wa mkweli kuna njia moja tu katika kanuni ya kale ya Mwenyezi Mungu nayo ndiyo hii kwamba kwa ishara za kimbingu Ahakikishe kabisa kuwa Mwenyezi Mungu Yu pamoja naye, na amekubaliwa kwake. Sasa zingatienei kuwa madai yangu ya kuwa Masihi Mau'udi siyo makubwa zaidi kuliko madai ya Hadhrat Musa na Hadhrat Isa, kisha fikirieni hao manabii watawa wakakubaliwaje duniani. Je, kwa baraka na misaada ya kimbingu, au kulikuwa na njia nyingine? Basi, tambueni kuwa hamna mageuko wala mabadiliko katika suna ya kale ya Mwenyezi Mungu. Kama mimi sikutumwa na Mwenyezi Mungu, bali huu ni uzushi tu na ughushi, hapo mwisho hautakuwa mwema na Mwenyezi Mungu Atanihilikisha kwa dhila, kisha kwa milele atanifanya lengo la laana. Kwani, hakuna dhambi kubwa kuzidi hii kuwa mtu aseme nimetumwa na Mungu ilhali hakutumwa kwa hakika, na aseme napata kuongea na Mwenyezi Mungu na maneno Yake yananiteremkia moyoni mwangu na ninatamkishwa hayo kwa ulimi

wangu, ilhali hakuwahi kuongea na Mwenyezi Mungu wala maneno Yake hayakumteremkia moyoni mwake wala hakutamkishwa hayo katu.

الا لعنة الله على الكاذبين الذين يفترون على الله وهم فى الدنيا
والأخرة من المخذولين[111]

Lakini, kama mimi ni kutoka kwa Mwenyezi Mungu, na Ndiye Aliyenituma, na kutoka Kwake ndiyo yale maneno ninayofunuliwa, basi sitapotezwa bure wala sitaangamizwa, bali Mwenyezi Mungu Atamhilikisha yule atakayeinuka dhidi yangu na kuwa kikwazo njiani mwangu. Nashangaa kwa nini watu wanastaajabia neno Masihi Mau'udi na kwa nini wananiomba uthibitisho wake, ilhali kiakili jambo hili si miongoni mwa mambo yasiyowezekana kuwa azaliwe mtu kama Masihi katika umati huu pia ulio mithili ya umati wa Musa.

Wanafalsafa pia wamekubali kuwa uwepo wa wana

---

[111] Tafsiri: Sikilizeni, laana ya Mungu iwawie waongo wamzuliao Mungu uwongo, nao ndio watupiliwao mbali katika dunia na Akhera. Mwenezi.

Adamu ni wa kiduara. Na hii ndiyo imethibitika kutokana na suna ya Mungu na kanuni ya tabia ya asili kuwa katika dunia hii baadhi ya watu wanazaliwa wakishabihiana na baadhi wengine. Washabihianao na watu wema pia wanaendelea kuzaliwa na wanaoshabihiana na waovu vilevile. Naam, yapasa kuomba uthibitisho kuwa ametoka kwa Mungu. Katika uthibitisho huo uthibitisho wote unajumuika. Angalieni, Nabii wetu s.a.w. alipowadhihirishia watu kuwa mimi ni mithili ya Musa na ni Mtume wa Mwenyezi Mungu, hapo wale waliokuwa wameishathibitishiwa Utume wa Mtume[saw] wakawa hawanayo shaka katika Mtume[saw] kuwa mithili ya Musa pia, na jinsi walivyouamini Utume wa Mtume[saw], ndivyo walivyomwamini kuwa mithili ya Musa. Basi, uthibitisho wa kuwa kutoka kwa Mungu na kuwa mkweli mwenye kupata ufunuo ni mzizi wa uthibitisho wote. Mathalan, Kitabu kinachomteremkia Nabii, hakuna anayeuliza

uthibitisho wa kila sentensi yake, bali kwa utibitisho wa utume, hayo mengine yanathibitika yenyewe. Wapenzi, siyo kwamba Mwenyezi Mungu Anataka kuunda kanuni ya pekee kwa ajili yangu. Angalieni kanuni ya zamani, na ulizeni swali sawa nayo.

Isitoshe, hadi leo hii iliyo tarehe 11 Rabii Al-Awwal 1311 Hijriyyah iliyo sawa na 22 Septemba 1893 ambayo yaafikiana na tarehe 8 Asooj 1950 ya kalenda ya Kibaniani, na ni siku ya Ijumaa, ishara zangu kuzidi elfu tatu zimekwisha dhihirika tayari ambazo mamia ya watu ndio mashahidi wake, bali kuhusikana na kutimia kwa baadhi ya bishara wapo mashahidi maelfu ya Mabaniani, Wakristo na wengine waipingao dini. Kama ikichunguzwa, itaonekana kuwa ziko baadhi ya ishara ambazo malaki ya maadui wa dini ya Kiislamu wamekwisha shuhuda kwa macho yao. Na wapo hai hadi sasa watu wale walioshuhudia ishara nyingi sana zilizozidi uwezo wa binadamu. Na wapo mamia

yao waliosikia habari za maombi kupokolewa kabla ya wakati wake na kisha wakajionea kutokea kwa mambo yaliyoelezwa mapema. Na pia wapo watu wapatao kumi na sita elfu katika India, Uingereza, Ujerumani, Ufaransa na Rumi, walio Mapandit na viongozi wa Wayahudi, wanasheria na Majusi, na mapadre, makasisi na maaskofu wa Wakristo ambao walipelekewa barua za rejista zenye madhumuni kwamba kwa hakika dini ya Kiislamu ndiyo ya kweli na dini nyinginezo zimekwisha enda mbali na asili yao na ukweli. Kama yeyote miongoni mwa wapinzani anashuku, basi akabiliane nami, na akikaa nami kwa mwaka mmoja ashuhudie kwangu ishara za dini ya Kiislamu. Kama ikionekana nina hatia, achukue kwangu fidia ya mwaka wake mmoja kwa hisabu ya Rupia 200 kila mwezi. Mimi simwombi kitu ila tu akubali dini ya Kiislamu. Na kama yeye akipenda anaweza kuwekewa fedha hizo ndani ya banki yoyote. Lakini mtu yeyote hakuelekea

upande huu. Sasa mwenye busara aweza kufikiria kwamba kama nisingekuwa na yakini kamilifu juu ya msaada wa Mwenyezi Mungu, inayokuwa baada ya kufululiza kushuhudia na baada ya tajiriba za binafsi, ingewezekanaje kwangu kujitokeza peke yangu kuwakabili wapinzani wote, yaani dhidi ya wale ambao juu ya uso wa ardhi walikuwa wapinzani mashuhuri wa dini na walikuwa viongozi wa kaumu zao. Ni dhahiri kuwa binadamu dhaifu hana uwezo kama huu nafsini mwake kuwa akabiliane na ulimwengu mzima. Basi, kulikuwa ni kitu gani, minghairi ya yakini yangu kamili na tajiriba za binafsi, kilichonifanya nithubutu kuchukua hatua hii. Si tu kwa maneno, bali vipeperushi vilivyochapishwa kwa Kiingereza na Kiurdu na kadhalika kuzituma barua kwa rejesta zilizopelekwa kwa nchi za Bara Hindi na Ulaya, vyote hivyo viligharimu Rupia karibu elfu mbili, lakini hakuna aliyejasiri kujitokeza kunikabili. Nyoyo za maadui

kutawaliwa na hofu ilikuwa ni ishara pia. Ili kuchunguza tu, mwulizeni padre yeyote wa zama zile kwamba je barua ya rejesta ya mwito wa Islam haikumfikia? Sasa, fikirini kuwa yule mtu anayetoa gharama ya maelfu ya Rupia kwa kuchapisha vipeperushi pekee na gharama ya kuvituma, na kumwekea zawadi ya fedha nyingi adui apatapo kushinda, yeye mtu huyo aweza kutegemea batili, uongo na uzushi? Je, hadi leo duniani amepata kusomeka ndani ya vitabu au kusikika ama kuoneka mzushi kama huyo. Hebu tajeni mfano wowote. Wapenzi, fahamuni kwa yakini kuwa kama Mungu Hayupo pamoja na mtu, uimara huu na ushujaa huu na utoaji huu wa mali hauwezi kutokea. Je, mtu yeyote amemwona sheikh yeyote au kumsikia katika zama hizi kuwa yeye amepata kuandika hata barua tu moja kumwita kwenye Islam Kamishna Msaidizi Mwingereza? Lakini, hapo siyo tu kiasi hiki, bali vipeperushi na barua za kuita kwenye Islam

zilipelekwa kwa Bunge la London, mwanamfalme atakayerithi ufalme, Malkia muadhamu na mwanamfalme wa Bismarck, ambazo zipo risiti zake mpaka sasa. Katika vipeperushi hivyo vilivyotolewa tangu miaka kumi iliyopita iliandikwa pia kuwa mimi nashabihiana na Hadhrat Masihi bin Mariamu katika sifa zake. Na kwa mwenye kuzingatia, hii ndiyo dalili nyingine ya ukweli wangu, kwani kama madai ya kuwa mithili ya Masihi Mau'udi yangekuwa ni mpango tu wa binadamu wala usingekuwa ufunuo kutoka kwa Mwenyezi Mungu, isingewezekana kufululiza kueneza ufunuo wa kuyasaidia madai hayo miaka kumi, bali kumi na miwili, mapema. Kwa sababu kila mtu anaweza kufahamu kuwa binadamu kitabia hawezi kutangulia kujihadhari kiasi hiki kuwa kazi au madai yanayotakiwa kufanywa miaka kumi na miwili baadaye, msingi wake uimarishwe hapo kabla. Tena ajabu juu ya ajabu ni kuwa Mwenyezi Mungu Ampe

huyo mdhalimu muda mrefu ambao hadi leo miaka 12 imeishapita. Na mzushi ajasiri katika uzushi wake, amabye mapema akanuia kuwa baada ya miaka 12 atadai hivyo, na akaweka msingi wa madai yake mapema miaka kumi na miwili kuwa mimi lazima ni mithili ya Masihi. Na si tu hivi hivi, bali kwa kutaja ufunuo akadai kuwa yu mithili ya Masihi na katika sifa zake akasema yu mithili yake, na akajifahamu yu kipande cha asili yake ya dhati. Tena siyo hiyo tu, bali akaandika kidhahiri na waziwazi miaka kumi na miwili ndani ya kitabu chake (yaani katika Baraahine Ahmadiyya) kabla ya madai yake ya Masihi kwamba Mwenyezi Mungu Amenipatia jina Isa na ameniahidi kuwa Nitakufisha kifo cha ajali, kisha Nitakunyanyua kwangu, na Nitakutakasa na masingizio ya waliokukataa, na Nitawaweka wafuasi wako juu ya maadai zako mpaka Kiyama. Na Mwenyezi Mungu si tu Ampe muhula, bali na Amsaidie pia kwa ishara za kiufunuo, na

kumtayarishia Jumuiya moja, ilhali Mwenyewe Anasema ndani ya Kurani Tukufu kuwa Simsaidii mzushi, naye anaangamia haraka na Jumuiya yake inafumukanishwa. Bali, Akamwambia Bwana wa Mitume s.a.w. kwamba kama ungelizua hata sawa na chembe, ungelikatwa mshipa mkubwa wa moyo. Kama si kweli kwamba Mwenyezi Mungu Anamshika haraka mzushi anayetaka kuwapoteza viumbe wa Mungu kwa kujifanya mtume, hapo — Mungu Apishe mbali — dalili hii haiwezi kuwa sahihi kuhusiana Mtume[saw] kwamba kama angelikuwa mzushi, Mwenyezi Mungu Angelimkamata. Isitoshe, juu ya muhula huu mrefu na misaada mamia ya Mwenyezi Mungu na mamia ya ishara zake, wapinzani nao wakafanya maelfu ya maombi ili adhabu initeremkie, na katika Mubaahala[112] wao pia wakaomba kulialia sana ili adhabu inishukie,

---

[112] *Mubahala* ndiyo mashindano baina ya makundi mawili ya kuomba dua kwa unyenyekevu kwamba kundi lisemalo uwongo lipate laana ya Mungu. Mwenezi.

lakini hawakupata kitu ila fedheha na aibu. Na Mwenyezi Mungu Mtukufu Anajua kuwa sisi katika Mubaahala wowote hatukumtakia adui yeyote kushukiwa adhabu, wala hatukumwombea Abdul Haq Ghaznawii kifo ambaye alifanya Mubaahala mjini Amritsar, lakini yeye alipiga kelele sana. Makusudiao yetu ya Mubaahala yalikuwa na hata wakati huu ndiyo kuwa zidhihirike kwa jumla ishara za kimbingu kwa wingi ili kunisaidia, na itatosha kwa kudhalilika na kufedheheka kwa mpinzani afanyaye mubaahala kuwa Mwenyezi Mungu kila mahala Adhihirishe ushindi wetu. Ilmuradi, hizo ndizo ishara za ukweli lakini kwa yule azingatiaye. Nasikitika kuwa naulizwa mara kwa mara kwamba ni dalili gani juu ya wewe kuwa Masihi Mau'udi. Lakini, watu hao hawafahamu kuwa ilikuwa dalili gani juu ya Hadhrat Isa[as] kuwa Mau'udi na juu ya Mtume[saw] kuwa Khatamun Nabiyyina. Je, siyo tu kuwa Mwenyezi Mungu akahakikisha ukweli wao

kwa ishara nyingi sana. Na ingawaje Wayahudi hawakumkubali Hadhrat Masihi na hadi leo wanasema kuwa yeye hakuwa Masihi Mau'udi, lakini kwa miujizia yake na ishara zake ikathibitika kwamba yeye alikuwa kutoka kwa Mungu.[113] Mahitaji

---

[113] Tanbihi: Bwana mmoja, jina lake Hidayatullah akinishutumu kuwa naikana miujiza ya nabii Isa, ameandika kijitabu pia. Yeye anatoa baadhi ya ibara za kitabu change, Izala Auhaam, akidhania mimi — Mungu Apishe mbali — naikana moja kwa moja miujiza ya Hadhrat Masihi[as]. Lakini ibainike kuwa hili ni kosa la mtazamo na fahamu ya hao watu. Mimi sikatai miujiza ya Hadhrat Masihi[as]. Bila shaka yeye pia alionyesha baadhi ya miujiza. Ingawaje kwa kuangalia Injili, miujiza yake inatiliwa doa sana, kama kilivyo kisa cha 'Birika' na kukataa kwake mara kwa mara kuwa mimi si mwenye kuonyesha miujiza. Lakini hatuishughulikii Injili. Kwa vyovyote kutokana na Kurani Tukufu yathibitika kuwa yeye alijaliwa baadhi ya ishara. Naam, ni kosa la wanazuoni wetu wasiozingatia vizuri kuwa wanadhani kana kwamba yeye pia kama Mwumbaji wa walimwengu alikuwa anaunda mfano wa mwili wa ndege fulani, akampulizia naye akihuika akaenda kuruka. Na alikuwa anaweka mkono wake juu ya maiti naye akahuika na kutembea. Na alikuwa mjuzi wa mambo ya ghaibu, yeye hajafa mpaka sasa na yupo mbinguni pamwe na mwili wake. Kama hayo mambo yanayonasibishwa kwake ni sahihi, basi inabaki shaka gani katika jambo hili kuwa yu mwumbaji wa ulimwengu, mjuzi wa mambo ya ghaibu na mhuishaji wa wafu! Hapo kama Mkristo yeyote akihoji kuwa

ya lazima huwa kuhakikisha yu mkweli na ametoka

---

uwepo wa sifa za kitu fulani ni uthibitisho wa uwepo wa kitu chenyewe, ndugu zetu Waislamu watajibuje? Wakisema kwamba kwa dua miujiza kama hiyo hudhihirika, hiyo itakuwa ziada juu ya Neno la Mungu, kwani yafahamika kutokana na Kurani Tukufu kwamba, mathalan, kwa kukipulizia kitu kilichokuwa kinatengenezwa kwa sura ya ndege kikaanza kuruka. Haikutajwa habari ya dua ndani ya Kurani Tukufu, wala haikutajwa kuwa sura hiyo ya ndege ilikuwa inahuika. Haifai kuongeza chochote ndani ya Neno la Mungu. Hiyo ndiyo kubadili maneno iliyosababisha Wayahudi kupta laana. Katika hali ambapo haithibitiki kitu kile kuhuika, bali yathibitika kutokana na Ma'alimut Tanzil na vitabu vingi vya maelezo ya Kurani kwamba hiyo sura baada ya kuruka kwa kitambo kidogo tu kilikuwa kinaanguka ardhini kama udongo, basi itafahamika nini isipokuwa kwamba huo udongo ulikuwa ni udongo tu. Na jinsi vidude vya udongo vya kuchezea watoto vinavyoenda kwa mitambo itengenezayo na mtu, sura hizo zilikuwa zinaruka kwa kuingiwa na roho ya Nabii, waila kukubali uumbaji hasa huleta uchafuzi mkubwa na kusababisha ushirikina. Makusudio ni mwujiza tu, na kitu kisicho kuwa hai kuruka pasipokuwa na uhai ni mwujiza mkubwa. Naam, kama katika kiraa fulani cha aya hiyo lipo neno 'Basi ikahuika' au kihistoria imethibitika kuwa hizo sura za ndege kweli zilikuwa zinahuika na kutaga na hadi sasa ndege wengi wapo walio vizazi vyao, basi uhakikisho wake uletwe. Mwenyezi Mungu Anasema ndani ya Kurani kwamba kama dunia nzima ikitaka kuumba nzi tu mmoja, haiwezi, kwani hapo itakuwa kushabihiana na uumbaji wa Mungu. Na kusema kuwa Mwenyezi Mungu Mwenyewe Amewaidhinisha kuumba, basi huu ndio uzushi. Hamna

kwa Mungu, na uthibitisho wa kuwa mithili huingia mumo humo. Juu ya hayo, mambo yote ya lazima yanapaza sauti kwamba Mujadidi wa karne hii awe Masihi Mau'udi, kwani alama za zama za Masihi Mau'udi zilizotajwa ndani ya Neno Tukufu la Mwenyezi Mungu zimeishatimia katika zama hizi. Je hamwoni kuwa ufalme wa Kikristo unaendelea kumeza serikali za dunia nzima, na umepata ustawi wa kila namna na umeafikiana na مِنۡ كُلِّ حَدَبٍ يَّنۡسِلُوۡنَ[114] Na hali ya kidini na ya kidunia ya Islam imeharibika kama ilivyokuwa hali ya Wayahudi katika wakati wa Hadhrat Masihi[as]. Na jinsi Masihi alivyokuja katika wakati ambapo kunyanyua upanga hakukustahili kwani Wayahudi kwa sababu ya maovu yao walikuwa

---

upingamizi katika Neno la Mungu. Mwenyezi Mungu Hampi yeyote idhini kama hiyo. Mwenyezi Mungu Hakumpa Mtume[saw] idhini hata kuumba nzi mmoja, basi mwana wa Mariamu alipataje idhini hii. Mcheni Mwenyezi Mungu, msiichukulie majazi kuwa hakika. Mwandishi.

[114] Tafsiri: Toka kila mahali pa juu watakuja mbio mbio. Sura Al-Ambiyaa, 21:97. Mwenezi.

wamepoteza utawala wao, na ufalme wa Kirumi haukukosea hata unyanyuliwe upanga, ndivyo ilivyo hali hivi leo kwamba wafalme wa Waislamu kwa sababu ya kupita kiasi na kushughulikia anasa wakapoteza utawala wao, bali hawakubakiwa na ujuzi wa kutawala, basi Mwenyezi Mungu Akawajalia Waingereza utawala, nao hawakudhulumu kwa kuchukua utawala. Hawakumzuia mtu kusali na kufunga saumu, hawakumzuia mtu kwenda kuhiji, bali wakaimarisha amani. Hapo, basi, kwa nini Mungu Mkarimu na Mrehemevu Angetoa fatuwa ya kunyanyua upanga. Je Alikuwa na upanga wa kidhahiri tu kwa kueneza dini, hakuwa na upanga wa kiroho? Juu ya hayo, wakati huu imani ya upanga haitegemewi. Waingereza hawakuwaingiza watu katika dini yao kwa upanga ili upanga ulipwe kwa upanga. Bali watu wakaangamia kwa wasiwasi wa falsafa mpya, sayansi mpya na mapadre. Kwa hiyo jibu lake ni kuhakikisha ukweli wa Islam, siyo

kuwapiga watu upanga. Basi, Mwenyezi Mungu sawa na hali ya Waislamu, Akawapelekea Muslih bila upanga na mkuki, mfano wa Hadhrat Masih na Akampatia silaha ya kimbingu tu kwa kuondolea mbali udajali. Na kama inavyofahamika idadi ya 1400 kutokana na maneno عيسىٰ عند منارة دمشق, Masihi Mau'udi huyu amekuja mwanzoni mwa karne ya kumi na nne, na kwa kuwa idadi ya وَاٰخَرِيْنَ مِنْهُمْ لَمَّا يَلْحَقُوْا بِهِمْ[115] ni 1275, basi katika zama hizi hizi yeye akatayarishwa. Na kama ilivyobashiri Kurani Tukufu kuwa wakati wa mawimbi ya fitina za Wakristo parapanda itapigwa, ndivyo alivyodhihiri, na waja wengi wa Mungu wakifunuliwa na Mungu wakatoa habari za ujaji wake kabla hajadhihiri. Bali baadhi yao wakatoa jina lake kabla ya kudhihiri kwake na wakasema huyo ndiye Masihi Mau'udi, na Isa mwenyewe amekwisha fariki. Wengi waonao kashfi wakasema

---

[115] Tafsiri: Kwa wengine miongoni mwao walio bado kuungana nao. Sura Al-Jumu'ah, 62:4. Mwenezi.

kuwa karne ya 14 ni zama za ujaji wa Masihi Mau‘udi na wakaandika ufunuo wao. Sasa, baada ya hayo, ndani ya habari kama hizi ambamo yapaswa kuwekwa pia nafasi kidogo ya imani ya ghaibu, yaweza kuwa na uthibitisho gani?

Mbali na hayo, zipo baadhi ya ishara nyingine zenye shani kubwa zilizo katika hali ya majaribio. Kwa mfano, bishara kumhusu Munshi Abdullah Atham wa Amritsar, ambayo muda wake ni miezi kumi na mitano kuanzia 5 Juni 1893, na bishara kuhusu mauti ya Pandit Lekhramu wa Peshawar ambayo muda wake ni miaka sita kuanzia mwaka 1893, kisha kuna bishara kuhusu mauti ya mkwe wa Mirza Ahmad Beg wa Hoshiarpur aliyekuwa mkazi wa Patti wilaya ya Lahore, muda wake uliobaki ni karibu miezi kumi na mmoja kuanzia leo iliyo tarehe 21 Septemba 1893. Mambo hayo yote yazidiyo kabisa nguvu za binadamu yanatosha kumtambua mkweli au mwongo, kwani kuhuisha

na kufisha ni hiari ya Mwenyezi Mungu. Maadamu mtu si mwenye kukubaliwa na Mungu kwa daraja ya juu kabisa, Mwenyezi Mungu kwa dua yake hawezi kumwangamiza adui wake, hususan mtu huyo anapodai ametoka kwa Mungu na akaiweka karama yake kuwa dalili ya ukweli wake. Basi kutoa matabiri si jambo dogo, si jambo lilio katika hiari ya mtu, bali hayo ndiyo katika hiari ya Mungu Mwenye enzi. Basi, kama yupo atafutaye haki, azisubiri nyakazi za kutimia matabiri hayo. Matabiri hayo matatu yanahusikana na mataifa matatu ya India na Panjab. Yaani, mmoja unawahusu Waislamu, mmoja na Mabaniani na mmoja na Wakristo. Ule utabiri unaowahusu Waislamu ni wenye shani kubwa sana, kwani sehemu zake ni hizi: (1) Kwamba Mirza Ahmad Beg wa Hoshiarpur atakufa katika muda wa miaka mitatu kamili (2) Na mkwewe aliye mumewe bintiye mkubwa atakufa ndani ya muda wa miaka miwili na nusu. (3) Tena Mirza Ahmad Beg asife

hadi siku ya kuolewa kwa binti yake mkubwa. (4) Na kwamba huyo binti pia hadi kuolewa na hadi kuwa mjane asife (5) Na mimi nami nisifie hadi mambo hayo yote yatimie. (6) Na kisha nipate kumwoa. Na ni dhahiri kuwa matukio hayo yote siyo ndani ya uwezo wa mtu.

Na kama bado uthibitisho huu wote haumtoshelezi Mian Ataa Muhammad, basi njia rahisi ni hii kuwa baada ya kukisoma kwa makini kijitabu hiki anipashe habari kwa njia ya kipeperushi kilichochapishwa kuwa sijatosheka na mambo hayo yote, bado naona huo ni uzushi tu, nami nataka ishara yoyote idhihiri kunihusu mimi. Hapo mimi, Mungu Akipenda, nitaelekea kwa Mungu kuhusiana na habari zake, nami nina yakini kuwa Mwenyezi Mungu Hatanifanya nishindwe dhidi ya mpinzani yeyote, kwani nimetoka kwake na nimekuja kwa amri yake ili kujadidisha dini yake. Lakini yapasa yeye katika kipeperushi chake aniruhusu kwa jumla

kwamba ufunuo wowote nikifunuliwa kumhusu yeye, niuchapishe. Nastaajabu kuwa katika hali ambapo Waislamu walipaswa kufurahi wakati wa Mujadidi kudhihiri, kwa nini wamefyeruka na kwa nini wakaona vibaya kwamba Mwenyezi Mungu Amemtuma mtu kwa kutimiza hoja ya dini yake. Lakini najua kuwa hali ya imani ya Waislamu wengi wa siku hizi imekwisha haribika sana, na sumu ya falsafa imeng'olea mbali mzizi wa itikadi yao. Midomoni mwao pasipo shaka mna Islam, lakini nyoyo zimekwenda mbali sana na Islam. Neno la Mungu na kudura za Mungu ni vichekesho machoni mwao. Ndivyo ilivyo hali ya Mian Ataa Muhammad. Nakumbuka huko Amritsar nilipomwambia Bwana Abdullah Atham bishara ya kifo chake, basi Mian Ataa Muhammad akaja pale nilipokaa na akanisimulia kama mfano kuwa daktari fulani aliniambia nitakufa katika muda fulani, lakini muda huo ukapita, nami baadaye nikaenda kwa

daktari huyo na kumsalimu. Kauliza, u nani wewe? Nikasema, ni yule Ataa Muhammad uliyemtabiria kifo chake. Alimaanisha kuwa hayo yote ni uwongo na upuuzi. Lakini Mian Ataa Muhammad akumbuke kutoa mfano wa daktari hapa kwathibitisha tu kwamba wewe huna habari ya mwanga wa kimbingu. Yupo bila shaka Yule Dhati Aitwaye Mungu, naye Huonyesha ishara za kimbingu kuisaidia dini yake ya kweli, si tu mpaka kwa zama maalumu bali sikuzote wakati wa haja, na Huimarisha upya imani ya dunia. Ni dhahiri kutokana na kueleza mfano wa daktari kuwa ni kiasi gani imani yako juu ya Mungu Huyu. Naona, sasa, nikimalize hapa kijitabu hiki.

فَالْحَمْدُ لِلّٰہِ اَوَّلًا وَّ اٰخِرًا وَّظَاهِرًا وَّبَاطِنًا هُوَ مَوْلَانَا نِعْمَ الْمَوْلٰى وَنِعْمَ النَّصِيْرُ[116]

Mtungaji
Mnyenyekevu Ghulam Ahmad Qadiani
22 Septemba 1893, mjini Qadian, siku ya Ijumaa

---

[116] Tafsiri: Sifa zote njema zamhusu Mungu, mwanzoni na mwishoni, kwa dhahiri na batini. Yu Mola wetu, ni Mola Mwema Aliyoje na Msaidizi Mwema Aliyoje! Mwenezi.

## SEREKALI YASTAHILI KUYAANGALIA HAYA

Mimi mnyenyekevu naeleza kwa uwazi na kwa kifupi kwamba kwa kuwa hisani za serikali ya Kiingereza zipo juu ya ukoo huu tangu baba yangu marehemu mzee Mirza Ghulam Murtadha hadi sasa, hivyo shukurani ya serikali hii yenye heshima imo ndani ya tabia yangu hasa wala siyo kwa kujikalifisha. Zile huduma alizoitolea babangu marehemu serikali hii kwa kuitakia heri kwa ikhalsi ya moyo haziwezi kutengwa na historia ya maisha ya baba yangu. Yeye daima sawa na hali yake na uwezo wake akaonyesha ukweli na unyofu katika kuihudumia serikali, ambao mtu hawezi kuuonyesha asipokuwa mwenye kumtakia mwingine heri kwa moyo wa kweli na kwa dhati. Katika machafuko ya mwaka wa 57[117] ambapo mafidhuli kwa kukabiliana na serikali wakaleta fujo, mzee wangu akaitolea

[117] Yaani, Mwaka 1857. Mwenezi.

serikali farasi hamsini akinunua kutoka katika mfuko wake na kutoa pia watu 50 wapanda farasi. Tena safari nyingine akaitolea serikali wapanda farasi kumi na wanne. Kwa sababu ya huduma hizi akawa amependwa na serikali. Basi, katika baraza la Gavana Mkuu alikuwa anapatiwa kiti kwa heshima sana, na maafisa wa serikali wa kila ngazi walikuwa wanamheshimu sana. Yeye akamtuma ndugu yangu aende katika baadhi ya mapigano kwa kuitumikia serikali. Katika kila jambo akapata ridhaa ya serikali na akaishi maisha yote kwa sifa njema mpaka akaaga dunia hii isiyo ya kudumu. Baadaye, kaka yangu Mirza Ghulam Qadir akafuata katika nyayo za marehemu mzee muda wote alioishi na kushughulikia kutumikia serikali kwa ikhlasi kwa moyo mkunjufu, kisha yeye naye akaondoka dunia hii. Natumai, mpaka sasa wapo hai baadhi ya maafisa Waingereza waliomwona mzee wangu na kushuhudia kwa macho yao huduma zake zenye

ikhlasi. Miongoni mwao kuna Bwana Griffin ambaye ameandika kitabu kuhusiana na Machifu wa Panjab na ndani yake amemtaja baba yangu kwa maneno mazuri.

Sasa, hali yangu ni hii kwamba baada ya kufariki jamaa na wazee hao, Mwenyezi Mungu Akaelekeza moyo wangu mbali na dunia, nami nikapenda uhusiano wangu na Mwenyezi Mungu uwe wa kweli, wa haki, wa mahaba kikamilifu. Basi, Akaujaza moyo wangu mahaba yake, si kwa juhudi zangu, bali kwa fadhili yake. Ndipo nikataka nipate maendeleo katika maarifa na mapenzi ya Mungu kadiri iwezekanavyo kwangu, na nitambue barabara kuwa Mungu Yu nani, na radhi yake imo katika mambo gani. Basi, nikatakasa moyo, na kuchukia kupendelea bila sababu, na nikaona kwa kunadhifisha jicho na kila uchafu, na kumwomba Mwenyezi Mungu msaada, ndipo nikafunukiwa na kuarifiwa na Mwenyezi Mungu kwa ufunuo wake

mtakatifu kwamba Mungu ni Yule Dhati Aliye Mkamilifu katika sifa zake zote na Anaendelea tangu azali kwa namna moja na njia moja. Siyo kwamba zamani Hakuwepo na baadaye Akawa Amekuwepo. Yeye Hazaliwi wala Hafi. Azaliwaye na afaye hana ule uhusiano naye — pasipo uhusiano wa utumishi — unaofahamika kuwa huyo anashirikiana naye katika Uungu wake, bali wazo lenyewe hili ni baya zaidi kuliko kumkana Yeye uwepo wake, na ni wazo ovu la hali ya juu kuliko maovu ya binadamu. Ni kweli, na kweli kabisa, kuwa miongoni mwa waja wa Mwenyezi Mungu waliokubaliwa naye ambao wana daraja kubwa kuliko wote ni wale wanaoitwa Manabii na Mitume. Bila shaka hao ndio wapendwa wa Mwenyezi Mungu, wamekubalika kwake, ni wenye heshima ya hali ya juu, wamejipoteza ndani Mwake, wakawa mfano wake, na jalali ya Mungu ikadhihiri ndani yao, Mungu yumo ndani yao, nao wamo ndani Yake, lakini hata hivyo hatuwezi

kwa hakika kumwita yeyote kuwa Mungu wala mwana wa Mungu. Pasipo shaka katika hitilafu hii Waislamu ndio juu ya haki na Wakristo wamekosea. Lakini kosa hili halionekani kudumu ndani ya Wakristo katika zama hizi. Waingereza ni watu ambao Mwenyezi Mungu Anataka kuwavutia siku hadi siku kwenye ustawi, dola, akili na busara, nao ndio wanaosogelea mbele kila siku katika ukweli na adili, na ndio chemchem ya elimu mpya na za zamani. Kwa hiyo, natarajia sana kuwa Mwenyezi Mungu Atawajalia mali hii pia, bali nafikiri Ameisha wajalia ndani kwa ndani. Kwa vyovyote, kwa kuwa Mwenyezi Mungu Ametuimarishia serikali kutoka miongoni mwa taifa hili, nasi tumejionea hisani za serikali hii ambazo kuzitolea shukurani si kazi rahisi, hivyo twaiyakinisha serikali yetu iheshimikayo kwamba sisi ni wenye ikhlasi na wenye kuitakia heri serikali hii kama walivyokuwa wazee wetu. Mkononi mwetu mna nini pasipo dua. Basi twamwomba

Mwenyezi Mungu Ailinde serikali hii na kila ubaya na kumfanya adui wake ashindwe akidhalilika. Mwenyezi Mungu Ametufaradhisha kuishukuru serikali hii mhisani kama kumshukuru Yeye. Basi tusipoishukuru serikali hii mhisani, au tukinuia kufanya shari, hapo hatukumtolea Mwenyezi Mungu pia shukurani, kwani kumshukuru Mwenyezi Mungu na kuishukuru serikali mhisani Aliyowapatia waja wake kama neema ni kitu kimoja, kila kimoja kinaambatana na kingine, kukiacha kimojawapo kwalazimu kukiacha na cha pili. Baadhi ya majahili na wajinga wanauliza, je kufanya jihadi dhidi ya serikali hii ni sawa au la? Basi ikumbukwe kuwa swali hili lao ni la kipumbavu, kwani serikali ile ambayo kuishukuru ni faradhi hasa na ni wajibu, iweje kupigana jihadi dhidi yake? Nasema kweli kabisa kuwa kumtakia vibaya mhisani ni kazi ya mwanaharamu na mwovu. Hivyo, imani yangu ni kuwa Islam inazo sehemu mbili. Moja ni

kumtii Mwenyezi Mungu, na pili kuitii ile serikali iliyoimarisha amani, ambayo imetupatia usalama dhidi ya wadhalimu. Na hiyo ndiyo serikali ya Kiingereza. Ingawaje ni kweli kuwa tunahitilafiana na mataifa ya Ulaya katika dini, nasi hatupendi yale mambo wanayopenda hao, lakini mambo hayo ya kidini hayafungamani katu na uhusiano wa raia na serikali. Mwenyezi Mungu Anatufundisha kwa uwazi kumshukuru na kumtii Yule mfalme ambaye chini ya kivuli chake tunaishi kwa amani. Basi tukiiasi serikali ya Kiingereza, twaasi Islam na Mungu na Mtume[saw]. Katika hali hii nani atakuwa mtovu wa unyofu kuliko sisi, kwani tumeachana na kanuni na sheria ya Mwenyezi Mungu. Hatuwezi kukataa kuwa wapo wengi kati ya Waislamu ambao chuki yao ya kidini imeushinda uadilifu wao na insafu yao, hata kwamba kwa sababu ya ujahili wao wanamngojea Mahdi mwenye hamu ya kumwaga damu, kana kwamba ataifanya ardhi kuwa nyekundu kwa damu

za wapinzani. Si hii tu, bali wanadhani pia kuwa Hadhrat Masihi[as] vilevile atashuka kutoka mbinguni kwa shabaha hii hii ya kumwaga damu ya wale Wayahudi na Wakristo walioponea chupuchupu kuuawa kwa mkono wa Mahdi. Lakini mawazo hayo ya baadhi ya Waislamu, mathalan ya Sheikh Muhammad Husain Batalawii na Jumuiya yake ni batili na kinyume cha Kitabu cha Mungu. Hao majahili wanapenda kumwanga damu, hawanayo mapenzi na huruma ya viumbe wa Mungu hata kidogo, lakini dini yetu ya kweli na sahihi ambayo kwa sababu yake watu hao wanatukufurisha ni kwamba hakuna ajaye kwa jina la Mahdi. Naam, Masihi Mau'udi amekwisha fika, lakini hautatumika upanga, bali kwa amani na ukweli na mapenzi zama zitageuka kwenye Umoja wa Mungu. Unawadia wakati, bali u karibu ambapo ardhini hataabudiwa Ram Chandra wala Krishan wala Hadhrat Masihias, na waabuduo wa kweli wataelekea kwenye Mungu

wao wa kweli. Na kumbukeni kuwa yule mfalme ambaye chini ya kivuli chake tunaishi kwa amani, kutunza haki zake ndiyo kutoa kwa hakika haki za Mungu. Na tunapomtii kwa moyo mfalme kama huyo, kana kwamba wakati huo tunafanya ibada. Je, mafundisho ya Islam yaweza kuwa haya kwamba tumfanyie mhisani wetu maovu, na yule ambaye atupatie kivuli baridi kwa kukaa tufululize kumtupia moto, au yule ambaye atupe mkate tumtupie mawe. Nani atakuwa mwovu zaidi kuliko mtu kama yule ambaye afikirie hata moyoni kumtenda vibaya mhisani!

Makusudio ya utangulizi huu ni kuwa serikali ipate kukumbuka kuwa sisi twaitolea shukurani kwa kiini cha moyo na tunashughulikia kuitakia heri kwa uwezo wetu wote. Nimewahi kusikia kwamba kuna mtu mmoja mkazi wa Batala, wilaya ya Gurdaspur anayejiita Sheikh Abu Said Muhammad Husain, kwa sababu ya kuhitilafiana nami katika

rai kuhusiana na maelezo ya baadhi ya maswala anaiandikia serikali mambo yasiyo ya kweli dhidi yangu kwa sababu ya uadui wake mkali na pasipo uadilifu kabisa kwa harara ya ukatili kwa shabaha ya kuwa serikali inidhanie viovu. Na anabatilisha uhusiano wenye ikhlasi na wema wa ukoo wangu kwa serikali na kuuficha na kuuzika chini ya uzushi wake, na kwa uadui tu na husuda yake anakazania kuwa mimi — Mungu Apishe mbali — kana kwamba si mwenye kuitakia heri serikali. Jahili huyu hafikirii hata kidogo kuwa miundombinu ya uwongo na uzushi usio na msingi haunayo ile nguvu ambayo huwepo kitabia ndani ya ukweli. Dhihirisho moja la nguvu ya ukweli huuponda mlima tikitiki. Isitoshe, ule uvundo wa ukaidi na ulaghai uliomo ndani ya uwongo hauwezi kufichikana kwa hisia ya kunusa iliyojaliwa na Mungu kwa maafisa wa serikali. Ingawaje uzushi wote huo wake ulikuwa wa aina ile ambayo kwa sababu ya kunivunjia heshima

ingefaa ujanja wake wote uondolewe mbali kwa njia ya mahakama, lakini ilionekana yafaa kuiarifu serikali yenye heshima kuhusu uzushi wa mtu huyo. Natumai serikali yenye busara haraka itatambua masingizio yake, na kuyapima na kutambua kuwa yalazimu kuyafutilia mbali ili baadaye habithi yeyote asijasiri kutenda matendo machafu kama hayo. Serikali yetu yenye busara na adili siyo kwamba haijui kuwa ingekuwa faradhi ya kila mtoa habari anayearifu serikali kuhusu jambo fulani na kutoa rai yake halisi ya kwamba awe ameisha chunguza barabara. Sasa serikali adilifu ikipenda yaweza kujisumbua kwa ajili ya ukoo ambao imekwisha upatia hati za ridhaa yake kwamba imwite mtoa habari huyo mwongo ambaye anaifikishia serikali habari kinyume cha ukweli dhidi yangu kwa kuchapa ndani ya gazeti lake, na kumtaka alete uhakikisho kwamba ni kwa dalili na sababu gani yeye ameniita kuwa mfisadi katika serikali ya Kiingereza. Na kama

asiweze kutoa dalili za kutosha, hapo imwonjeshe kidogo adhabu ya kisheria ipasavyo, kwani hiyo ndiyo busara na kuufariji ukoo uitakiao serikali heri kikweli. Ingawaje, hamaki kama hiyo inapatikana katika maandishi ya baadhi ya wapinzani wengine wa kidini pia kama vile Padre Imaduddin na wengineo, lakini hao wana udhuru kidogo kwa sababu ya ukosefu wa ujuzi na harara ya dini na chuki isiyogangiki nao hawawezi kutongoa ukweli, lakini huyu Sheikh Batalawii kwa hakika amepita mipaka. Serikali adilifu iangalie pia maandishi yake ya mwaka 1884 yaliyopo ndani ya gazeti lake la Isha'atus Sunna pamwe na maandishi yake ya mwaka 1892-1893, ili ijulikane kuwa mtu huyu ni mnafiki, mficha haki na ni ndumakuwili. Ijapokuwa twajua kuwa mbele ya serikali yenye busara, akili, adili na elimu pana, hila kama hizo haziwezi kufua dafu na serikali hii yenye busara kali inatambua mwelekeo wa mambo toka mbali, na kuzichukulia

ripoti za chuki kuwa duni na zenye husuda yenye aibu, lakini hata hivyo, serikali haiteremshiwi wahyi, na yawezekana ipate kudanganyika kwa sababu ya washari wachache kunena kwa kauli moja, na hapo binadamu awezavyo kudanganyika. Kwa hiyo ililazimu kueleza kidogo hali kiasi fulani.

Sasa, kwa ajili ya serikali kuangalia, twanukuu kutoka katika Isha'atus Sunna la mwaka 1884, yaani Na 6, J 7, ibara kiasi fulani ya gazeti la mtu huyu juu ya maoni yake kuhusu Baraahine Ahmadiyya ili serikali yenye busara iangalie binafsi kuwa mtu huyu zamani aliandika nini kunihusu mimi, na sasa anaandika nini. Na ibara ile ndiyo hii:

## Jibu la Ukosoaji wa Kisiasa

Kadiri tunavyojua hali na fikara za mwandishi wa Baraahine Ahmadiyya, watakuwa ni wachache miongoni mwa wenzetu wazijuao kadiri hiyo. Mwandishi ni ndugu wa kwetu, bali alikuwa mwenzetu shuleni katika ujana (tulipokuwa twasoma *Qutbi* na *Sharha Mulla*). Tangu wakati huo hadi leo twaandikiana na kulakiana na kuwasiliana barabara. Kwa hiyo, yafaa kauli yetu kuwa sisi twazijua sana hali na fikara zake isichukuliwe kuwa ni kupiga chuku. Wazo la kuipinga serikali ya Kiingereza hata halikumsogelea karibu na mwandishi. Licha ya huyu, hata katika ukoo wake mzima hakuna mtu wa wazo hilo. Bali, baba yake mzee Mirza Ghulam Murtadha akahakikisha kimatendo kuwa mwaminifu aitakiaye seikali heri katika zama za ghasia (uasi wa mwaka 1857). Katika uasi huo, wafisadi waovu walipolishambulia gati la Trimmu linalopakana na Gurdaspura, babake mtukufu, ingawaje hakuwa kabaila na chifu mkubwa,

akatoa kutoka katika mfuko wake hasa mafarasi hamsini pamwe na wapanda farasi chini ya uongozi wa mwanaye mpendwa marehemu Mirza Ghulam Qadir, kwa kuisaidia serikali, na serikali ikamtolea shukurani na tuzo pia kiasi kadha. Isitoshe, kwa ajili ya huduma hizo marehemu Bwana Mirza (babake mwandishi) sikuzote alifadhiliwa na serikali na katika baraza la Gavana akapewa kiti kwa heshima. Na maafisa wakuu wa Wilaya na Qismat[118] (yaani naibu wa Kamishna na Kamishna), wakampa mara kwa mara hati za ridhaa ambazo baadhi ya hati hizo zipo mbele yetu wakati huu. Kutokana na hati hizo inabainika kuwa zimeandikwa kwa jazba kubwa ya moyo, ambazo haziwezi kuandikwa kwa jazba hiyo kwa mtu yeyote isipokuwa kwa ajili ya yule aliye mwaminifu wa kweli na hasa mwenye kuitakia heri serikali. Mara nyingi Kamishna na naibu wa Kamishna katika siku za matembezi yao waliendelea kumtembelea Bwana Mirza

[118] 'Qismat': Zamani katika Bara Hindi, eneo la mkoa lenye wilaya mbili au zaidi liliitwa Qismat, nalo lilikuwa chini ya Kamishna. Mwenezi.

nyumbani kwake kwa khulka njema na mahaba na kumfariji. Na alipofariki, mabwana Kamishna, Kamishna wa fedha na Luteni Gavana wakadhihirisha masikitiko yao sana ndani ya barua zao na wakaahidi kwa siku zijazo kuthamini fadhila za ukoo huu na kuuangalia na kuutunza. Kwa sababu ya heshima hii ya ukoo na kuwa wenye kuitakia heri serikali tangu zamani, Kamishna wa Fedha amempendekeza kwa nguvu siku hizi Mirza Sultan Ahmad (mwanaye mwandishi) kwa cheo cha kuwa Mkuu wa tarafa, na taarifa yake imekwisha tumwa kwa wilaya ili kutekelezwa. Ilmuradi, ukoo huu tangu zamani ndio wenye kuitakia heri serikali na unatendewa vizuri na serikali. Ili kusadikisha habari hizo na matukio hayo twazinukuu katika maelezo ya pembeni[119] barua

[119] **Tafsiri ya Hati Ya J. Nickolson kwa Mirza Ghulam Murtadha, Chifu wa Qadian.**

Nimesoma kwa makini barua yako ya kunikumbusha huduma zako za zamani na za ukoo wako na haki zenu. Naelewa sana kuwa tangu mwanzo wa serikali ya Kiingereza wewe na ukoo wako kwa kweli mmekuwa raia wenye kujitolea, wanyofu na imara, na kwamba haki zenu zinastahili kuheshimika.

Kwa vyovyote, usiwe na shaka na utulie kwamba serikali ya

tatu miongoni mwa zile barua zilizo mbele yetu wakati huu ili mahasidi wasio na busara waitambue heshima na cheo cha ukoo huu machoni mwa serikali ya Kiingereza na kuachana na utashi mbaya na nia mbovu, na ili Waislamu wa kawaida wasitishike kwa kitabu hiki na mwandishi wake kwa sababu ya kudanganyika.

Ingawaje, hususan kwa sababu ya hali ya utaalamu na udaruweshi wa mwandishi wa kitabu (Bwana Mirza Ghulam Ahmad) haijatokea hivyo, lakini kadiri ifaavyo kwa wanachuoni na madaruweshi kuitakia heri serikali na kadiri wawezavyo, yeye hakusita kuifanya. Upanga wa wataalamu ni kalamu, na silaha ya madaruweshi ni dua. Mwandishi hakusita kutumia silaha hizo kwa kuitakia heri serikali na kuisaidia. Yeye ameisha andika mara nyingi kwa kalamu yake, na ndani ya kitabu hiki hiki ambacho kukieneza ni faradhi yake usiku na

---

Kiingereza haitazisahau katu haki na huduma za ukoo wako ambazo zitafikiriwa barabara pindi uwadiapo wakati ufaao. Mwendelee kuwa raia waaminifu na wenye kujitolea, kwani ndani yake umo utulivu wa serikali na ustawi wenu. 11.6.1849.

mchana ameeleza bayana[120] kuwa serikali ya Kiingereza

**Tafsiri ya Hati Ya Bwana Robert Casts**
**Kwa Mirza Ghulam Murtadha,**
**Chifu wa Qadian.**

Kwa kuwa umetoa msaada mkubwa wa wapanda farasi na mafarasi katika siku za uasi wa mwaka 1857 na kudumisha uaminifu tangu mwanzo wake hadi sasa, na kwa sababu hii umepata fadhila za serikali, basi joho la heshima lenye thamani ya Rupia 200 unatolewa kwa kuzitambua huduma zako njema na kuwa zawadi kwa uaminifu wako.

Isitoshe, sawa na utashi wa Kamishna Mkuu, kama ilivyojulishwa ndani ya Na. 576, ya tarehe 10 Agosti 1858, unaandikiwa barua hii ikiwa ni alama ya ridhaa ya serikali kwa uaminifu wako na kusifika kwako.

**Tafsiri ya Barua ya Sir Robert Egerton, Kamishna wa Fedha, Panjab.Tarehe 29 Juni 1876**
**Rafiki yangu mpendwa Ghulam Qadir,**
**Chifu wa Qadian.**

Barua yako iliyoandikwa tarehe ya pili mwezi huu imeniwasilia. Nimesikitika sana kwa kifo cha baba yako, Mirza Ghulam Murtadha ambaye alikuwa Chifu mnyofu na mwenye kuitakia sana heri serikali ya Kiingereza.

Kwa kuzizingatia huduma za ukoo wako, nitakuheshimu vile alivyokuwa anaheshimiwa baba yako mwaminifu. Ikipatikana nafasi ifaayo nitafikiria ustawi wa ukoo wako na kufidi.

Imeandikwa 29 Juni 1876

Mwandishi: Sir Robert Engerton, Kamisha wa Fedha wa Panjab.

120 Maneno yenyewe ya mwandishi ni haya yanayonukuliwa

kimuhutasari kutoka katika sehemu ya tatu na nne ya kitabu hiki. Ndani ya kurasa za mwanzo za sehemu ya tatu anasema kwamba mambo wanayolazimika Waislamu kutekeleza kwa bidii na jitihada kwa kurekebisha hali yao watayajua watakapoyafikiria na kuzingatia hayo, hayana haja ya kuyaeleza na kubainisha. Lakini hapa yafaa kutaja jambo hili miongoni mwa mambo hayo, ambalo hisani na maelekeo ya serikali ya Kiingereza yanalitegemea, ni kwamba serikali ihakikishiwe barabara kabisa kuwa Waislamu wa Bara Hindi ni raia waaminifu. Kwani baadhi ya Waingereza wasio na ujuzi, hususan Dkt Hunter aliye mwenyekiti wa Tume ya Elimu hivi sasa amekazania sana madai yake ndani ya Kitabu Chake mashuhuri kuwa Waislamu hawaitakii heri serikali ya Kiingereza na wanafahamu kupigana jihadi dhidi ya Waingereza ni faradhi. Ingawaje wazo hili baada ya kuangalia sheria ya Islam litathibitika kuwa halina msingi na ni kinyume cha ukweli, lakini ni masikitiko kuwa matendo mabovu ya baadhi ya wakaa mlimani wajinga wasio na adabu yanalipa nguvu wazo hilo, na labda kwa kushududia matendo yao wasiwasi wa bwana daktari aliyetajwa umepata kuimarika. Kwani majahili huwa wanatenda matendo kama hayo mara kwa mara, lakini habari hii haiwezi kufichika kwa mchunguzi kuwa watu kama hao wako mbali sana na dini ya Kiislamu. Hao ndio Waislamu kama alivyokuwa Mclain Mkristo. Basi, ni dhahiri kuwa hayo ndiyo matendo yao wenyewe wala siyo sawa na sheria. Yafaa kuangalia dhidi yao maelfu ya Waislamu walioendelea kuitakia heri serikali ya Kiingereza na bado wanaendelea. Mnamo mwaka wa 1857 machafuko yaliyofanyika, hakuna Mwislamu mwema mwenye bahati

ni neema mojawapo miongoni mwa neema za Mungu.

---

njema aliyekuwa mwenye elimu na mstaarabu aliyeshiriki katika ufisadi isipokuwa wale tu waliokuwa majahili na waovu. Bali katika Panjab pia Waislamu wenye hali ndogo wakaisaidia serikali zaidi ya uwezo wao. Baba yangu marehemu pia juu ya kuwa mwenye uwezo mdogo akaisaidia serikali kwa kutoa mafarasi hamsini kwa kununua kutoka katika mfuko wake kwa ikhlasi na jazba kwa kuitakia heri, na pia akatoa maaskari hamsini thabiti hodari na kuonyesha zaidi ya uwezo wake kuwa anaitakia heri serikali. Waislamu matajiri nao wakatoa huduma kubwa sana. Sasa twaelekea tena kwenye madhumuni yenyewe kuwa mifano mikubwa mikubwa ya ikhlasi na uaminifu imekwisha dhihirika kutoka kwa Waislamu, lakini Bwana Daktari kwa sababu ya bahati mbaya ya Waislamu hakuujali uaminifu huo wote na wakati wa kutoa natija hakuvijali vigezo mantiki katika hitimisho lake. Kwa vyovyote, yawalazimu ndugu zetu Waislamu kudhihirisha sana mno kuwa wanaitakia heri serikali kabla serikali haijaathirika na udanganyifu wa hao watu. Katika hali ambapo ni wazi sana swala hili la sheria ya Kiislamu ambalo limekubaliwa na Waislamu wote kuwa ni haramu kupigana jihadi dhidi ya serikali ambayo chini yake Waislamu wanaishi kwa amani, afya na uhuru, na ambayo inawafanyia hisani kwa tunu, na ambayo inawasaidia kikamilifu kueneza hidaya, basi ni jambo la kusikitisha sana kuwa wanazuoni wa Islam kwa kuafikiana wasilieneze vizuri swala hili na waendelee kushutumiwa kwa midomo na kalamu ya wasio na ujuzi kwa shutuma zielezazo uzembe wao wa kidini na wadhurike kidunia pasipo haki. Basi nionavyo mimi, yafaa Anjuman Islamiyya ya Lahore, Calcutta, Bombay na kadhalika zifanye mpango kuwa wateuliwe wanazuoni

Hii ndiyo rehema kubwa. Serikali hii kwa ajili ya

---

wachache maarufu ambao fadhila zao na elimu, na kujitenga kwao na dunia na ucha Mungu wao uwe unakubaliwa na watu wengi. Na wale wataalamu walio mashuhuri kiasi fulani pembezoni mwa maskani yao waandike makala zao za kielimu ambamo iwe imeelezwa bayana kuwa sawa na sheria ni mwiko kupigana jihadi dhidi ya serikali ya Kiingereza ambayo ni mlezi na mhisani wa Waislamu. Hao Wataalamu walete maandishi yao hayo kwa kupiga mihuri yao kwa wale wanazuoni walioteuliwa na Anjuman. Barua za maandishi hayo zikikusanyika zote pamoja ambazo zaweza kuitwa 'Barua za wanazuoni wa Bara Hindi', zichapishwe katika matbaa ambayo ichape kwa maandishi safi na sahihi. Kisha nakala zake kumi au ishirini zipelekwe kwa serikali, na nakala zilizobakia zigawanywe katika sehemu mbalimbali za Panjab na India, na hususan katika nchi za mipakani. Ni kweli kuwa Waislamu wenye uchungu wameandika majibu ya mawazo ya Dakta Hunter, lakini kanusho la Waislamu wawili, wanne, haliwezi kuwa badala ya kanusho la Waislamu wote kwa jumla. Bila shaka kanusho la watu wote litakuwa na athari imara na yenye nguvu na kwa sababu yake maandiko mabovu ya bwana daktari yatatokomea, na baadhi ya Waislamu wasiojua wataelewa vizuri kanuni yao ya kweli na takatifu, na usafi wa moyo wa Waislamu na wema wa raia hawa utakuwa wazi kwa serikali ya Kiingereza ipasavyo. Isitoshe, mawazo ya baadhi ya wakazi majahili wa mlimani yataendelea kurekebika kwa mawaidha na nasaha ya kitabu hicho. Hatimaye, twaona ni wajibu wetu kudhihirisha kuwa ingawaje inawajibika kwa Bara Hindi zima kuifahamu serikali ya Kiingereza kuwa neema ya Mwenyezi Mungu kwa kuangalia hisani za serikali zilizo juu ya watu wote na hekima zake na

Waislamu ni baraka ya kimbingu. Mungu Mwingi kuishukuru mithili ya neema nyingine za Mungu, lakini Waislamu wa Panjab watakuwa watovu wa shukurani wasipokuwa na yakini kuwa serikali hii iliyo rehema kubwa ya Mungu ni neema kubwa kabisa. Wanapaswa kufikiria kuwa kabla ya serikali hii walikuwa katika hali mbaya namna gani, kisha wakawa namna gani katika usalama na amani. Basi, kwa hakika serikali hii ni kama baraka ya kimbingu ambayo kwa ujaji wake taabu zote zikatoweka na tumesalimika katika dhuluma na mabavu ya kila aina. Tukaondolewa kila kizuizi na kizingiti kisichokuwa kinajuzu. Hakuna chochote cha kutuzuia tusiweze kufanye jambo jema au kiweze kutuharibia raha yetu. Basi, kwa hakika Mungu Mkarimu Mrehemevu Ameileta serikali hii ikiwa ni mvua ya rehema ambayo mmea wa Islam unaendelea kwayo kustawi tena katika Panjab, na ambayo kukiri manufaa yake ndiyo kwa hakika kukiri hisani za Mungu. Hii ndiyo serikali ambayo uhuru ilioutoa ni dhahiri na unajulikana hata kwamba Waislamu waliodhulumiwa wa nchi zingine wanapenda sana kuhamia nchi hii. Jinsi chini ya himaya ya serikali hii inavyowezekana kwa njia bora sana kazi ya kutoa mawaidha kwa kuwarekebisha Waislamu na kuondoa bidaa zilizokwisha ingia, na mambo yanayoamsha jazba katika wanazuoni wa Islam kueneza Islam ndani ya serikali hii, na kazi bora ya kutafakari na kuhakiki inafanyika, na hoja zinatimizwa juu ya wapinzani wa Islam kwa kutunga vitabu baada ya kufanya uchunguzi kuisaidia dini hii imara haiwezekani, sawa na ujuzi wangu, kufanyika siku hizi katika nchi yoyote nyingine. Hii ndiyo serikali ambayo chini ya himaya yake adilifu wanazuoni wakapata baada ya miaka mamia fursa ya kuwaambia bila hofu wasio na ujuzi, uchafu wa bidaa na

wa ukarimu Amewaletea Waislamu serikali hii kama ubaya wa ushirikina na uharibifu wa kuabudu viumbe, na kuwaeleza waziwazi njia iliyonyoka ya Mtume[saw]. Je, kuitakia maovu serikali kama hii yajuzu, ambayo chini ya kivuli chake Waislamu wanaishi kwa uhuru na amani na kutekeleza ipasavyo faradhi za dini na kushughulikia kueneza dini zaidi sana kuliko katika nchi zingine? La, hasha! Haijuzu katu, wala mtu mwema na mtawa hawezi kuwaza moyoni wazo chafu kama hili. Tunasema kweli kabisa kuwa leo katika dunia ni serikali hii tu ambayo chini ya kivuli cha ukarimu yapatikana baadhi ya makusudio ya Kiislamu yasiyowezekana kupatikana katika nchi zingine. Ukienda katika nchi za Washia, huko wanaghadhibika kwa mawaidha ya Wasuni; na nchini mwa Wasuni, wanaogopa Washia kueleza maoni yao. Kadhalika Muqallidina hawawezi kujieleza mijini mwa Muwahhidina**, wala Muwahhidina ndani ya biladi za Muqallidina. Ingawaje wajionee wenyewe kwa macho yao bidaa fulani, lakini hawanayo nafasi ya kusema. Hatimaye, hii hii ndiyo serikali ambayo chini ya himaya yake kila dhehebu linatongoa rai yake kwa amani na utulivu. Na jambo hili ndilo liwafaalo wenye haki, kwani katika ile nchi ambamo hamna nafasi ya kusema, hamna ushujaa wa kutoa nasaha, humo ukweli unawezaje kuenea! Kwa kueneza ukweli, ile nchi tu inafaa ambamo wenye ukweli wanao uhuru wa kutoa mawaidha. Pia ifahamike kuwa shabaha hasa ya jihadi za kidini ilikuwa ni kuimarisha uhuru na kuondoa dhuluma. Jihadi za kidini zilifanyika dhidi ya zile nchi ambamo wenye kutoa mawaidha walikuwa na hofu ya kuuawa wakati wa kutoa waadhi, ambamo kutoa mawaidhi kwa amani ilikuwa

**[Muqallidina ni wafuasi wa maimamu wanne wa Masuni, na Muwahhidina ndio Ma-Ahle Hadith. Mwenezi]

mvua ya rehema. Kupigana na serikali kama hii na

---

muhali kabisa, na mtu alikuwa hawezi kusalimika na mabavu ya kaumu yake kwa kujichagulia njia ya haki. Lakini uhuru wa serikali ya Kiingereza hauna mabaya haya, bali unayasaidia maendeleo ya Kiislamu na kuyatilia nguvu. Waislamu wanalazimika kuithamini neema hii iliyoletwa na Mungu na kwa njia hii wakanyage mbele katika maendeleo yao.

Na ndani ya kurasa za mwanzo za sehemu ya nne anasema kuwa muda kidogo umepita, baadhi ya mabwana miongoni mwa Waislamu wameleta upingamizi dhidi ya madhumuni yaliyojumuishwa pamoja na sehemu ya tatu kuhusiana na kuitolea shukurani serikali ya Kiingereza, wengineo wameleta barua na wengine wameandika maneno makali pia kwamba kwa nini utawala wa Kiingereza umepewa kipaumbele kuliko serikali zingine. Lakini ni dhahiri kuwa ile serikali inayotangulia kwa ustahifu wake na uongozi bora, tunawezaje kuificha! Ubora nido ubora tu hata kama uwepo ndani ya serikali yoyote iwayo. Hekima ni mali ya mwaminio iliyokuwa imepotea. Na izingatiwe pia kuwa hii siyo fundisho la Islam kwamba ile serikali ambayo Waislamu wakikaa chini yake wafanyiwe hisani na wapate riziki yao waliyokadiriwa katika himaya yake kwa amani na utulivu, na wapate kulelewa kwa neema zake zifulilizazo, kisha wageuke na kuiuma, na wasitoe shukurani hata chembe kwa wema na ukarimu waliofanyiwa. Bali, Mungu wetu Mkarimu Ametufunza kwa njia ya Mtume wake s.a.w. kuwa tulipe wema kwa wema mwingi sana na kumshukuru aliyetupa neema, na tupatapo nafasi tuitendee serikali kama hii kwa moyo wa kweli na huruma nyingi na kuitii kwa furaha na njia bora, na kwa kuona ni wajibu. Basi, ile sukurani niliyotoa kwa serikali ya Kiingereza katika tolea la sehemu ya tatu,

kufanya jihadi ni haramu kabisa. Kanuni ya Islam siyo hii kuwa ile serikali ambayo Waislamu wakiishi chini yake wafanyiwe hisani na wajipatia hadhi yao ya riziki na wapate kulelewa kwa neema zifululizo, kisha waiume kama nge. Na pia akaiombea serikali hii mara nyingi. Na katika dua yake ya mwisho yameandikwa maneno haya ndani ya kipeperushi kilichochapishwa katika Matbaa ya Riyadh Hind Amritsar, ambacho ametaka nakala zake elfu ishirini kueneza ndani ya India na Uingereza: "Waingereza ambao serikali yao jamala iliyostaarabika na yenye huruma, kwa kutufanyia hisani na kututendea kama marafiki imetupatia jazba kwamba tuwatakie kwa harara ya moyo ustawi wa dini na dunia yao ili nyuso

---

sikuitoa kwa fikara yangu binafsi, bali masisitizo makubwa ninayozingatia ya Kurani Tukufu na Hadithi yamenilazimisha kutoa shukurani hii. Basi ni kupita kiasi kwa baadhi ya ndugu zetu wasiofahamu ambao kwa sababu ya utovu wa busara na ubahili wa kitabia wamelifikiria kuwa ni sehemu ya Islam.
(Ubeti): E dhalimu, kutoa udhuru siyo tabia ya wapenzi.
Bure unawaharibu jina waja wema wachache.
(Baraahine Ahmadiyya)
Imechapwa katika Panjab Press, Sialkot

zao nyeupe ziwe zenye nuru na zing'ae huko akhera pia jinsi zilivyo nzuri katika dunia. Basi, twawaombea kwa Mwenyezi Mungu heri yao katika dunia na akhera. Ee Mungu, waongoze na wasaidie kwa roho itokayo kwako, na wajalie hadhi nyingi katika dini yako.

Basi, kumsingizia mtu huyo kwamba yeye ni mpinzani wa serikali ya Kiingereza, na kukidhania kitabu chake kuwa kinaipinga serikali, kama si udanganyifu na shari ya kishetani, ni nini basi! Waitakiao heri serikali na wafuasi wa dini ya Kiislamu wasisikilize maneno kama hayo ya mahasidi wala wasiwe na dhana mbaya kuhusu kitabu hicho na mwandishi wake. Mapema tumeisha tulia kwa mintarafu ya serikali kuwa haitatia maanani maneno hayo dhidi ya mwandishi, bali atakayeyafikisha maneno kama hayo kwa serikali, serikali itamkemea kwa uongo wake.

## KUAHIRISHA KWA MKUTANO WA 27 DESEMBA 1893

Kwa masikitiko twaandika kuwa zimeibuka sababu chache zilizoelekeza rai yetu kwamba safri hii mkutano huu uahirishwe. Na kwa kuwa baadhi ya watu watashangaa ni sababu gani ya kuuahirisha, hivyo kwa kifupi sababu hizi zinaandikwa kiasi fulani.

Mosi, mkutano huu makusudio na lengo lake lilikuwa ni kuwa wanajumuiya wetu kwa njia yoyote wapate mabadiliko ndani mwao kwa kuonana nami mara kwa mara hata kwamba nyoyo zao zielekee kikamilifu kwenye akhera na ndani yao izalike hofu ya Mwenyezi Mungu, nao wawe mfano kwa wengine katika utawa, ucha Mungu, hofu ya Mungu, wema, upole, mahaba baina yao na udugu, na kwamba uwepo ndani yao unyenyekevu na ukweli, na wayashughulikie mambo ya dini kwa jazba kubwa. Lakini baada ya mkutano huu wa kwanza matokeo kama haya hayakuonekana, bali katika siku zenyewe za mkutano ikasikika kwamba baadhi yao

wanalalamikia tabia mbovu ya baadhi ya ndugu, na baadhi yao katika mkusanyiko huu mkubwa wanadhihirisha khulka mbaya kwa raha zao wenyewe. Kana kwamba mkusanyiko wenyewe ukawa sababu ya majaribio kwa ajili yao. Isitoshe, naona kuwa baada ya mkutano athari njema na bora bado hazijaonekana mpaka sasa katika baadhi ya watu. Hayo nimejua kwa sababu kutokea siku zile hadi leo wageni wengi sana wanakaa kwangu, baadhi yao wanaondoka na wengine wanakuja, wakati mwingine idadi ya wageni ikafikia mia, na pengine walipungua kidogo. Lakini katika mkusanyiko huu, wakati mwingine, kwa sababu ya upungufu wa nafasi na uhaba wa vifaa kwa ajli ya wageni yamesikika maneno makali baina ya baadhi ya wageni kwa na hasira isiyostahili na uchoyo jinsi wasafiri wa garimoshi wagombanavyo kwa sababu ya upungufu wa nafasi. Na kama mtu, pindi garimoshi linapokurubia kabisa kuondoka, anafika mbiombio pamwe na mzigo wake kwa hofu na kuwafikia, wanamfukuza na kufunga

mlango wakisema hamna nafasi kwetu, ilhali nafasi yaweza kutolewa, lakini wanaonyesha moyo mgumu. Huyo akishika tiketi na kubeba kifurushi chake anahangaika huko na huko, na hakuna anayemhurumia, hatimaye wafanyakazi katika garimoshi wanampatia nafasi kwa nguvu. Basi ndivyo uonekanavyo mkutano huu pia kuwa ni njia ya kuharibu hali za khulka. Maadamu vifaa vya kuwahudumia wageni havipatikani kikamilifu na maadamu Mwenyezi Mungu Haijalii Jumuiya yetu kwa fadhili yake mahususi upole, uraufu, huruma, moyo wa kuhudumia na kuvumilia shida, mpaka hapo mkutano huu hauonekani sawa na masilahi, ilhali moyo wangu unapenda kuwa wafanyao baiati waje wakisafiri kwa ajili ya Mungu na kukaa nami na baada kupata mabadiliko kidogo waondoke, kwani kifo hakitegemewi, chaweza kuja wakati wowote. Wafanya baiati hunufaika kwa kuniona, lakini yule tu ananiona kikweli aitafutaye dini kwa subira, na makusudio yake ni dini tu. Basi ujaji wa watu kama hao wenye nia safi unafaa

siku zote, sio tu kwenye mkutano, bali katika nyakati nyingine wanaweza kupata fursa na faragha ya kuongea nami vizuri. Na mkutano huu sio kama sherehe za kidunia hata kuufanya kwa kudumu kuwe lazima. Bali, kuufanya hutegemea nia njema na matokeo mema; la sivyo, ni bure kabisa. Na maadamu haijulikani na tajiriba haitoi ushuhuda kuwa mkutano huu umeleta faida hii ya kidini na unaiathiri hivi mienendo na khulka za watu, mkutano huu si tu ni bure bali baada ya kuelewa kuwa mkutano huu hauleti natija njema, mkutano huu ni uasi na njia ya upotevu na bidaa mbovu. Sipendi katu kuwa mimi kama baadhi ya ma-Pirzada wa siku hizi niwakusanya wafanyao baiati yangu kwa kuonyesha shani ya kidhahiri tu. Bali lengo langu ninalofanyia juhudi ni marekebisho ya viumbe wa Mungu. Basi, kama jambo au mpango fulani lisilete marekebisho, bali usababishe uharibifu, hapo hakuna aliye adui wake kama mimi katika mahuluku. Na ndugu yangu Hadhrat Maulawii Nuruddin, Mungu amweke salama, mara

nyingi aliniambia kuwa wengi kati ya Jumuiya yetu hawajajipatia ustadi, ustaarabu, utakaso wa moyo, utawa na kupendana kwa ajili ya Mungu. Naiona kauli ya Bwana Maulawii kuwa ni kweli kabisa. Natambua kuwa baadhi ya mabwana baada ya kujiunga katika Jumuiya na kufanya baiati yangu na kuahidi kufanya toba halisi, bado ni wenye nyoyo kupindika, wanawaona wanajumuiya wao wanyonge kama mbwamwitu. Kwa kiburi hawawezi kutoa salamu kwa adabu, licha ya kuonyesha khulka njema na huruma. Nawaona wabovu na wachoyo kiasi hiki kwamba wanagombana juu ya mambo madogo madogo ya ubahili na kusukumana na kushambuliana kwa mambo mabovu. Wakati mwingine wanafikia kutukana na kuzalisha inadi nyoyoni. Wanajadiliana kwa tamaa za nafsi juu ya namna za vyakula na vinywaji. Na ingawaje waungwana na wenye bahati njema pia wapo wengi katika Jumuiya yetu, bali kwa yakini wapo zaidi ya mia mbili ambao wanayo fadhili ya Mwenyezi Mungu, wanaolia kwa kusikiliza

nasaha, na wanatanguliza akhera, na nasaha zinawaathiri ajabu mioyoni mwao, lakini wakti huu nataja watu wenye mioyo iliyopindika, nami nashangaa, ni hali gani hii! Ee Mungu, ni Jumuiya gani hii iliyo pamoja nami! Kwa nini nyoyo zao zaangukia tamaa za nafsi, kwa nini ndugu mmoja anamsumbua ndugu mwenzake na anataka kumpita yeye. Nasema kweli kabisa kuwa imani ya mtu haiwezi kuwa sawa mpaka awe ametanguliza, awezavyo, raha ya nduguye juu ya raha yake. Kama ndugu yangu mbele yangu analala chini ilhali yu dhaifu na mgonjwa, nami juu ya kuwa mwenye siha na afya nakitwaa kitanda ili huyo asipate kujikalia hicho, basi ni masikitiko kwa hali yangu kama nisiinuke na nisimpe kitanda change kwa mahaba na huruma wala nisijipendelee kulala chini. Kama ndugu yangu ni mgonjwa na hajiwezi, basi ni masikitiko kwa hali yangu kama mbele yake nilale kwa amani na nisimtafutie njia ya kumpatia raha sawa na uwezo wangu. Na kama ndugu yangu katika dini anitolee ukali kidogo kwa kiburi, basi

ni masikitiko kwa hali yangu kama nimtendee vikali makusudi, bali yanipasa nivumilie maneno yake na kumwombea katika sala zangu kwa uchungu, kwani yu ndugu yangu na anaugua kiroho. Kama ndugu yangu ni punguani au hana ujuzi au kwa kupungukiwa busara apate kukosea, basi haifai nimdhihaki au kukunja kipaji na kumtolea ukali na kumwaibisha, kwani hizo zote ni njia za kuangamiza. Mtu hawezi kuwa mwaminio wa kweli maadamu si mpole wa moyo na hajioni duni kuliko wote, na majivuno yote hayatoweki. Kuwa hadimu wa kaumu ndiyo alama ya kuwa Bwana. Kuongea na wenye hali ndogo kwa upole na unyenyekevu ni alama ya kukubaliwa na Mungu, na kutoa jawabu la maovu kwa mema ni alama za bahati njema. Kuzuia ghadhabu na kuvumilia maneno makali ni ushujaa wa daraja ya juu. Lakini naona mambo hayo hayamo ndani ya baadhi ya wanajumuiya wetu. Bali baadhi yao wanakosa ustaarabu kiasi hiki kuwa kama ndugu mmoja amejikalia kitanda cha nduguye kwa ukaidi, yeye anataka kumwondoa,

lakini haondoki, basi huyo anapindua kitanda na kumtupa chini.[121] Kisha yule wa pili pia anarudisha maovu kwa kumtolea matusi machafu na kujituliza. Hizo ndizo hali ninazoshuhudia katika mkusanyiko huu, hapo moyo huudhika kupata uchungu na mara naona afadhali kukaa baina ya wanyama mbuai kuliko wanadamu hawa. Basi kwa kutarajia furaha gani nikusanye watu kwa kuiitisha mkutano! Hili si tamasha katika matamsasha ya dunia. Mpaka sasa najua niko peke yangu isipokuwa ninao marafiki wachache ambao kama mia mbili na kitu ambao juu yao kuna rehema mahususi ya Mungu. Miongoni mwao kwenye daraja ya kwanza ni rafiki yangu halisi mpenzi Maulawii Hakim Nurruddin na marafiki wachache wengine niwajuao kuwa kwa ajili ya Mwenyezi Mungu tu wanao uhusiano nami wa upendo na wanaoona nasaha zangu kwa mtazamo wa

[121] Mambo hayo kuhusu Jumuiya yetu azizi ni kama nasaha kutoka kwangu. Mwingine yeyote haruhusiwi kuyazungumzia kwa kumtaja mwingine jina lake, waila yeye atashika njia ya dhambi na fitina zaidi kulko wengine wote.

taadhima, wanalenga akhera. Basi hao, insha Allah, wapo pamoja nami duniani na akhera, na mimi nipo pamoja nao. Niwafahamuje pamoja nami wale watu ambao nyoyo zao haziko pamoja nami ambao hawamtambui Yule niliyemtambua mimi, wala hawaimarishi nyoyoni mwao adhama Zake, wala hawazingatii wakati wa kudhihaki na kutenda maovu kuwa Yeye Anatuona, wala hawafikirii tunakula sumu ambayo matokeo yake ya lazima ni kufa. Kwa hakika hao ndio wasiotaka kuachana na njia za kishetani. Kumbukeni, asiyetaka kufuata njia yangu, hatokani nami, na yu mwongo katika madai yake. Hataki kukubali dhehebu langu, bali analipenda dhehebu lake. Yu mbali nami jinsi magharibi ilivyo mbali na mashariki. Amekosa, yuafahamu nipo pamoja naye. Nakariri kusema, takaseni macho yenu, yang'arisheni kiroho jinsi yang'aavyo kidhahiri. Kuona kidhahiri, hata wanyama wanaona; lakini binadamu anasemwa mwenye kuona anapoona kibatini, yaani anapata hadhi ya kupambanua baina ya mwema na mbaya, kisha anaelekea

kwenye wema. Basi msijitafutie macho ya kuonea ya wanyama tu bali tafuteni macho ya kikweli. Tupilieni mbali kutoka ndani ya nyoyo zenu masanamu ya dunia, kwani dunia ni adui wa dini. Haraka mtakufa na mtaona kuwa wokovu ndio kwa ajili ya wale waliochukia maono ya kidunia nao walikuwa wenye nyoyo safi zisizo na ila. Nimechoka kusema hayo mambo mara nyingi. Kama hali zenu ni hizi, basi kuna tofauti gani baina yenu na baina ya wengine. Lakini hii ndiyo mioyo isiyozingatia. Sitazamii macho yao yatapata kuona, ispokuwa Mungu Akipenda. Nami nawachukia duniani na huko Akhera. Kama ningelikuwa peke yangu katika pori, ingelikuwa afadhali kwangu kuliko kukaa nao wasioziheshimu amri za Mwenyezi Mungu wala hawatetemeki mbele ya jalali na heshima Yake. Kama mtu aseme tu mdomoni pasipo ukweli kuwa mimi ni Mwislamu, au kama mwenye njaa atamke tu mdomoni neno 'mkate', itamfaa nini? Kwa njia hizo hataokoka wala hatashiba. Je Mwenyezi Mungu Haziangalii nyoyo? Je mtazamo wake wa kina haufiki

mpaka ndani sana ya tabia ya mtu?

Basi, Enyi msiofahamu, fahamuni vizuri, Enyi mlioghafilika, zingatieni barabara kuwa hamwezi kuachiliwa pasipo utakaso wa kweli wa kiimani na wa kikhulka na kiamali. Na yule akibaki mchafu kwa kila jiha, kisha anajifahamu kuwa yu Mwislamu, yeye hamdanganyi Mwenyezi Mungu, bali anajidanganya yeye mwenyewe. Nahusianaje na wale wasiojitwika amri za dini kwa moyo wa kweli wala hawashikamani na ukweli, wala hawapendi kuzichukia tabia za kifasiki, wala hawatengani na vikao zinamofanywa dhihaka, wala hawaachani na mawazo machafu, wala hawashikamani na utu, ustaarabu, subira na upole; bali wanawasumbua wenye hali ndogo na kuwafukuza wanyonge, wanatembea masokoni kwa maringo, wanajikalia vitini kwa kiburi na wanajifahamu wao ndio wakubwa, lakini hakuna mkubwa ila yule ajifahamuye yu mdogo. Wamebarikiwa wale wanaojiona hakiri na wadogo na wanazungumza kwa haya na wanawaheshimu wenye hali ndogo na

maskini na kuwastahi wanyonge, hawadhihaki kwa ujeuri na majivuno, na wanamkumbuka Mola wao Mkarimu na hutembea juu ya ardhi kwa unyenyekevu. Basi, nakariri kusema kuwa hao ndio watu waliotayarishiwa Pepo. Na yule ambaye duniani humu hayuko nje ya jahanamu ya jeuri, kiburi, majisifu, majivuno, anasa za dunia, uchoyo na maovu, katu hatakuwa nje yake huko Akhera pia. Nifanyeje, na kutoka wapi nilete yale maneno yatakayoziathiri nyoyo za kundi hilo. Ee Mungu, nijalie yale maneno na nifunulie zile hotuba ambazo zitilie mioyo yao nuru yake na kuiondolea mbali sumu yao kwa athari ya sifa yake ya kiuasumu. Roho yangu inashumbuka kwa shauku ya kuwa iwadie ile siku ambapo niwaone katika Jumuiya yangu watu wengi waliokwisha achana na uwongo kikweli na kufunga ahadi ya kweli na Mungu wao kwamba wataepukana na kila shari na kutengana kabisa na kiburi kilicho asili ya jeuri zote, na watadumu kumcha Mola wao. Lakini hadi sasa sioni sura kama hizi isipokuwa watu wachache mahususi. Naam, wanasali

wasijue sala ni kitu gani. Mpaka moyo ufanye sijida ya unyenyekevu, kuzitegemea sijida za dhahiri ni tamaa ya bure. Kama damu na nyama za dhabihu zisivyomfikia Mungu, bali utawa pekee unamfikia, ndivyo hivyo rukuu na sijida za kimwili zilivyo bure maadamu rukuu na sijida za moyo hakuna. Moyo kusimama katika ibada ni kutekeleza amri za Mungu, rukuu ni kuelekea Kwake na sijida ndiyo kutengana na nafsi yake. Basi, ni masikitiko, masikitiko elfu, ya kwamba sioni ndani yao athari yoyote ya maneno haya, lakini naomba dua, na nitadumu kuomba maadamu nipo hai, na dua yenyewe ndiyo hii hii kuwa Mwenyezi Mungu Azitakase nyoyo za Jumuiya yangu hii, na kwa kurefusha mkono wa rehema yake Azielekeze nyoyo zao Kwake na kuziondelea mbali nyoyoni mwao jeuri zote na inda na kuwajalia wapendane kikweli. Ninayo yakini dua yangu hii wakati fulani itapokelewa na Mungu Hatapoteza bure dua zangu. Naam, naomba pia kuwa kama yupo ndani ya Jumuiya yangu mtu aliye mwenye bahati mbaya kwa kudumu

katika elimu na nia ya Mungu, ambaye hana bahati ya kujipatia utakaso wa kweli na hofu ya Mungu, basi, Ee Mungu, Umgeuze kwangu aende upande mwingine jinsi alivyogeuka Kwako, na badala yake Umlete mwingine aliye mpole wa moyo ambaye roho yake inakutafuta Wewe. Hali yangu sasa ni kuwa namwogopa mwenye kufanya baiati jinsi mtu amwogopavyo simba, kwani sitaki mtu akiwa kidudu cha dunia aungane nami. Basi, hii ndiyo sababu mojawapo ya kutofanya mkutano niliyoieleza.

Pili ni hii kuwa bado vifaa havipo kikamilifu, na wenye bidii ya kweli wapo wachache, na kazi nyingi kuhusiana na uenezi wa vitabu zinabaki kwa sababu ya uhaba wa wenye ikhlasi. Basi katika hali hii, sina mimi wala marafiki zangu wenye ikhlasi uwezo wa kuitisha mkutano unaohitaji kufanywa mpango mkubwa sana kwa ajili ya mamia ya watu mahususi na wa kawaida ambao waje kukaa kwa siku kadha, na sawa na desturi ya mkutano uliopita baadhi ya wasafiri wa mbali wenye hali

ndogo wasaidiwe kutolewa masurufu ya safari, na kwa siku kadha mamia ya wageni wakaribishwe ipasavyo, na mamia ya watu wafanyiwe mpango wa kuwapatia vitanda, na kutengeneza makazi ya kutosha kwa kukaa kwao. Na ni dhahiri kuwa vitu hivyo vyote vinahitaji maelfu ya Rupia. Na tukikopa kwa ajili ya mpango huu, hili ni jambo la dhambi kubwa, kwani mahitaji ya lazima ya dini hayajaliwi, lakini kwa kujichukulia jukumu la gharama zile ambazo hazikumbukwi baadaye tujitwishe karadha ya fedha nyingi bila sababu. Hata sasa, ingawaje hakuna mkutano, kazi ya kupokea wageni imezidi kiasi hiki kwamba tangu mwaka mmoja kila siku pengine wageni thelathini, arobaini na pengine mia wanawasili ambao kati yao wengi huwa wenye hali ndogo wa sehemu za mbali sana wanaopewa masurufu wakati wa kuwasindikiza. Shughuli hii inaendelea kila siku barabara, na kuisimamia mhashamu Maulawii Hakim Nuruddin anajibidiisha kwa moyo wote na anawapatia masurufu kutoka katika mfuko wake wasafiri wengi wa

mbali. Akawapa baadhi yao Rupia 30 kila mmoja na baadhi wengine Rupia 40 kila mmoja, na kutoa Rupia mbili mbili au nne nne ni kawaida yake. Siyo hii tu bali akatoa pia siku hizi Rupia karibu mia tatu, mia nne, kwa kutumikia wageni kwa moyo wake mkubwa na ukarimu wa nafsi yake, na hiyo ni mbali na misaada ya hapo kabla. Isitoshe, jukumu la kutoa gharama nyingi za uchapishaji wa vitabu akajichukulia, kwani uchapaji wa vitabu pia unaendelea barabara. Ingawaje, kwa sababu ya matumizi ya lazima bado mpango wa kujipatia matbaa yetu wenyewe haujaweza kufanyika, lakini Bwana Maulawii msifika anashughulikia huduma hizi kwa moyo wote na roho yote. Na baadhi ya marafiki wengine nao sawa na uwezo wao na nguvu yao wanaendelea kutumikia, lakini mpaka lini yawezekana kuvumilia gharama kiasi hiki kutoka katika mapato mapungufu. Ilmuradi, kwa sababu hizo naona yafaa kuahirisha mkutano mwaka huu. Na mbele itakuwa kama utakavyokuwa utashi wa Mwenyezi Mungu, kwani utashi Wake unaushinda utashi

wa binadamu mnyonge. Sielewei itafanyika nini, nami sijui utashi wa Mwenyezi Mungu unaafikiana na maandishi yangu haya ama katika takdiri yake kuna jambo ambalo sijalijua hadi sasa.

وافوض امری الی اللہ و اتوکل علیہ ھو مولانا نعم المولی و نعم النصیر[122]

Mirza Ghulam Ahmad wa Qadian

[122] Nami ninamkabidhi Mwenyezi Mungu jambo langu, na ninamtegemea Yeye. Yu Mola wetu. Ni Mola Mwema Aliyoje, na Msaidizi Mwema Aliyoje! Mwenezi.

# KASIDA

## Kumsifu Hadhrat Mtukufu Maulana na Mwongozi wetu Masihi Mau‘udi, Mwenyezi Mungu Amweke Salama

ای ذات تو کان گوہرِ علم | دانی تو بہائے جوہرِ علم

Ewe uliye mgodi wa elimu, unatambua thamani ya johari ya elimu.

از علم دلِ تو گنج بر گنج | و ز خامہ کشادۂ درِ علم

Kwa sababu ya elimu, moyo wako ukawa hazina kubwa, na kalamu yako imefungua mlango wa elimu.

علمست بذات روح پرور | تو آمدی روح پرورِ علم

Elimu ipo kwa yule aileaye roho. Umewasili, Ewe uileaye roho ya elimu.

تو نافہ کشائے پردۂ راز | تو نشر شمیم عنبرِ علم

U mfungua mfuko wa miski, wa pazia la siri. U mwenezi wa marashi ya ambari ya elimu.

در دیدہ نشین تو مردم آسا | ای صدر نشین و سرورِ علم

Umejikalia jichoni kama mboni, Ewe chifu na mwongozi wa elimu.

تو نورِ چراغِ دینِ احمد | تو شمع منار و منبرِ علم

U mwanga wa taa ya dini ya Ahmad[saw]. U mshumaa wa mnara na mimbari ya elimu.

ایمان ز تو جیغہ جیعۂ ابرو | تو غازۂ روئے دلبرِ علم

Imani imepambika kwa sababu yako, U poda ya uso wa mpendwa wa elimu.

تو مظہر آخرین منہم | تو اوّل حرفِ آخرِ علم

U dhihirisho la *Akharina Minhum*, U wa kwanza katika elimu.

بر تُست رہِ ہُدیٰ نمودن | امروز توئی چو رہبرِ علم

Ni juu yako kuonyesha njia ya mwongozo, kwani leo wewe ndiwe kiongozi wa elimu.

اکنون تو کلاہ ناز بر کن | ای تاجِ مزین سرِ علم

Sasa ujiwike kilemba cha jamala, Ewe taji lipambwalo la kichwa cha elimu.

دادی خبرِ وفاتِ عیسیٰ | کو بود نہان بدفترِ علم

Umetoa habari ya kifo cha nabii Isa[as] iliyokuwa imefichika ndani ya daftari ya elimu.

فرخندہ بمان کہ تازہ کردی | زیبندہ لباس دربرِ علم
آن وعدہ کہ عالمِ زمانہ | کردست بما زِ داورِ علم

Ufurahi, Ewe uliyejivalia mavazi mazuri ya elimu kwani umejadidisha ile ahadi Aliyotuahidia Mjuzi wa zama kwa njia ya mwamuzi wa mambo ya elimu.

بینم بہ رخت نشان موعود | گونیست مرا بصائرِ علم

Naiona usoni mwako alama iliyokuwa imeahidiwa, ingawaje sina busara sana ya elimu.

تو مہدی و ہادئ زمانے | تو عیسیٰ و خوش پیمبرِ علم

U Mahdi wa zama na Mwongozi . U Isa, na mjumbe mpendwa wa elimu.

در دست پئ گلوی دجال | داری تو کشیدہ خنجرِ علم

Unayo hanjari mkononi iliyochomolewa ili kumpiga dajali shingoni.

بر روہمہ عالمان صورت | دارند حجاب اکبرِ علم

Wajifanyao wanazuoni wanayo usoni hijabu kubwa ya elimu.

آنرا کہ ہدایت ازل ہست | آرند کشان کشان برِ علم

Wale waliobahatika tangu azali kuongoka, malaika wanawaleta kwa kuwavuta, kwenye mapajani mwa elimu.

برمن نظرے زِ چشم رحمت | ای روئے تو نیک منظرِ علم

Nitupie jicho la rehema, Ewe ambaye uso wako ni onyesho zuri la elimu.

من تشنہ لب و فتادہ در رہ | تو ساقی آب کوثرِ علم

Nasikia kiu sana, nami ni mnyonge kabisa, nawe ndiwe mwenye kunywesha maji ya kauthar ya elimu.

للہ تو مکن زِ من دریغے | نورے زِ مہ منوّرِ علم

Kwa ajili ya Mungu usinikatalie nuru kutoka kwa mwezi ung'aao wa elimu.